# TATHIMINI YA MAUDHUI KATIKA TAMTHILIA TEULE ZA KISWAHILI ZINAZOTAHINIWA SHULENI ZA UPILI NCHINI KENYA: *MSTAHIKI MEYA (2009)* NA *KIGOGO (2016)*.

NA


**EVELYN KAKIVI MUTHUI**

**C410/KIT/20670/2015**


**TASNIFU HII IMEWASILISHWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI**.


**IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA**

**CHUO KIKUU CHA SOUTH EASTERN KENYA**


**2019**

## UNGAMO

### Ungamo la Mwanafunzi

Tasnifu hii ni kazi yangu asili na haijawahi kuwasilishwa kwa madhumuni ya shahada yoyote katika chuo kikuu kingine nchini Kenya.

EVELYN KAKIVI MUTHUI

C410/KIT/20670/2015

Sahihi______________________________Tarehe___________________________

### Ungamo la Wasimamizi

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha South Eastern Kenya kwa madhumuni ya kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili katika Kiswahili.

DKT. ESTHER NJOKI CHOMBA

Sahihi_______________________________Tarehe__________________________

Mhadhiri, Idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika

Chuo Kikuu cha South Eastern Kenya

DKT. MUSYOKA FRANCIS MWANGANGI

Sahihi________________________________Tarehe_________________________

Mhadhiri, Idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika

Chuo Kikuu cha South Eastern Kenya

# SHUKURANI

Safari hii ya kiakademia imekuwa ndefu na ya kufikirisha zaidi. Shukrani zangu ni kwa Maulana kwa kuniwezesha kiafya, kihela, amani na ushirikiano wa kimazingira nilioupata wakati wa zoezi hili. Asante Maulana kwa kuwa mwanga na kinga dhabiti kuhakikisha kwamba nimefikia tamati salama.

Wasimamizi wangu Dkt. Esther Chomba na Dkt. Francis Musyoka, asanteni kwa usimamizi wenu na ushauri wenu. Mmekuwa wenye subira na wenye uelekezi wa kupigiwa mfano. Bila kukoma mliusukuma utafiti wangu na kufanikisha elimu yangu. Maulana tu ndiye anaweza kuwalipa. Kwa wahadhiri wangu, Dkt. Stephen Kamau na Dkt.Titus Kaui asanteni sana kwa mafunzo na ushauri wenu mlionipa. Mliupa msingi utafiti wangu kwa uelekezi wenu wa busara.

Zaidi ninamshukuru mpenzi Peter Ndichu, mama mzazi Ann Syokau, ndugu zangu, mwanangu mpendwa Javier Muthui na marafiki wa dhati Catherine Mbusya, Muthama Matsitsi kwa heri njema walizonitakia na kunitia motisha nilipoelekea kukwama. Asanteni sana. Maombi yenu yaliniwezesha kufanikisha utafiti huu.

# TABARUKU

Kwa familia yangu na marafiki wapendwa.

# MAELEZO YA ISTILAHI

**Maudhui**: Jumla ya mawazo yote yanayozungumzwa pamoja na mtazamo wa mwandishi kuhusu mawazo hayo.

**Tamthilia tahiniwa**:Ni tamthilia ambazo zinateuliwa kutahiniwa katika shule za upili.

**Ujarabati**:Ni ufafanuzi wa ujuzi unaotokana na mambo halisi yanayoshikika, kuonekana na kuhisika katika fikra na mishipa ya binadamu.

**Kutathimini**:Kuhakiki, kueleza, kuainisha na kutoa maoni juu ya kazi fulani ya kifasihi kwa kuongozwa na kaida maalum.

## MAELEZO YA VIFUPISHO

**KISCOL**: Kwale Interntional Sugar Company Limited. Kiwanda cha Sukari cha Kwale

**CDF:**(CONSTITUENCY DEVELOPMENT FUND) Hazina ya Ustawi wa Maeneo Bunge.

**EACC:**(ETHICS AND ANTI-CORRUPTION COMMISSION) Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi.

**KRA:** (KENYA REVENUE AUTHORITY) Mamlaka ya Kukusanya Ushuru Nchini Kenya.

**KBS:** (KENYA BUREAU OF STANDARDS) Shirika la Kukadiria Ubora wa Bidhaa Nchini Kenya.

**Bw:**Bwana.

**Dkt:** Daktari.

**Nk:** Nakadhalika.

**K.V:** Kama vile.

# IKISIRI

Utafiti huu uliongozwa na lengo la kutathimini maudhui kwenye tamthilia tahininiwa za karne ya ishirini na moja na kuyalinganisha na matukio halisi katika jamii.Mtafiti pia alitakikana kubaini ufaafu na uhalisi wa maudhui ya tamthilia tahiniwa za karne ya ishirini: tamthilia za *Mstahiki Meya (*Arege, 2009) na *Kigogo* (Kea, 2016). Tatizo kuu la utafitihuu lilikuwa kuwepo kwa ukuruba wa maudhui katika kazi za waandishi tofauti kwa nyakati tofauti na hata jinsia tofauti. Kuteuliwa kwa kazi za tamthilia zenye maudhui sawa katika vipindi tofauti vya utahini piakulichochea mtafiti kutaka kubaini ufaafu wa tamthilia tahiniwa.Utafiti uliongozwa na maswali yafuaatayo: ni maudhui yapi makuu yanayojitokeza katika tamthilia za *Mstahiki Meya (*Arege, 2009) na *Kigogo.* (Kea, 2016)?Ni masuala yapi makuu ya kijamii yaliyosheheni katika kipindi cha kuidhinishwa kutahiniwa kwa tamthilia hizi?Je, kuna ulinganifu wa uhalisi wa maudhui ya kazi hizi na uhalisi wa kijamii?Utafiti huu ulitegemea zaidi data iliyokusanywa kutoka kwa usomaji wa maktabani na hojaji kwa walimu na wanafunzi katika shule za upili kwenye kata ndogo ya Nzambani kaunti ya Kitui. Mtafiti pia alisoma na kubaini maudhui kaitka tamthilia teule. Baada ya kusoma, mtafiti aliyaandika maudhui yale kama data ya utafiti akitoa mifano mwafaka ili kusisitiza ukweli kuwa maudhui ya waandishi tofauti na nyakati tofauti ni sawa. Uchanganuzi wa madhui kwenye tamthilia ulikuwa wa kimaelezo tu kuonyesha ukuruba na uhalisi wa maudhui.Ilikupata maudhui ya kijamii, mtafiti alikusanya data kutoka kwa vyombo vya habari kama vile magazeti, kusoma majarida na ripoti mbali mbali. Mtafiti pia alipata data jumuishi kutoka kwa hojaji za walimu na wanafunzi wa kidato cha tatu na nne ili kuwa kiwakilishi cha jamii. Data hiyo iliwasilishwa katika jedwali kupata idadi ya waliotoa jibu la ndio au la kutegemea swali. Idadi ya waliojibu ndio au la zaidi iliwasilishwa katika mchoro wa kisayansi kwa kutumia mbinu ya *OriginPro*ili kupata picha kamili.Matokeo ya utafiti yalikuwa kwamba tamthilia zinaendeleza maudhui makuu sawa na yaliyo wazi katika jamii. Ilibainika wazi kuwa maudhui ya tamthilia yanaifaa jamii kwa kuendeleza elimu na maadili kwa mujibu wa mtaala wa elimu. Tafiti zaidi zinaweza kufanywa kwa tanzu zingine za fasihi andishi kama vile kulinganisha maudhui katika riwaya na hadithi fupi, au pia

kutumia nadharia zingine kama vile uhalisia wa kijamaa ili kuchunguza naudhui na vigezo vingine vya uteuzi wa tamthilia.

## YALIYOMO

UNGAMO ........................................................................ i

SHUKURANI ........................................................................ ii

TABARUKU ........................................................................ iii

MAELEZO YA ISTILAHI ........................................................ iv

MAELEZO YA VIFUPISHO ...................................................... v

IKISIRI ........................................................................ vi

SURA YA KWANZA ............................................................... 1

1.0 Utangulizi ........................................................................ 1

1.1 Usuli wa Mada ........................................................................ 1

1.2 Tatizo la Utafiti ........................................................................ 3

1.3 Madhumuni ya Utafiti ........................................................................ 4

1.4 Maswali ya Utafiti ........................................................................ 4

1.5 Upeo na Mipaka ........................................................................ 4

1.6 Sababu za Kuchagua Mada ........................................................................ 5

1.7 Umuhimu wa Utafiti ........................................................................ 6

**SURA YA PILI ........................................................................ 7**

**MAPITIO YA MAANDISHI ................................................... 7**

2.0 Utangulizi. ........................................................................ 7

2.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ........................................................................ 7

2.2 Yaliyoandikwa kuhusu Maudhui ........................................................................ 10

2.3 Nadharia ya Uhalisia ........................................................................ 12

2.4 Misingi ya Kinadharia ........................................................................14

**SURA YA TATU ......................................................... 16**

**MBINU ZA UTAFITI ..................................................... 16**

3.0 Utangulizi ........................................................... 16

3.1 Muundo wa Utafiti ................................................................................16

3.2 Eneo la Utafiti ......................................................................................17

3.3 Sampuli Lengwa......................................................................................17

3.4 Uteuzi wa Sampuli ................................................................................18

3.5 Ukusanyaji wa Data ..............................................................................19

3.6 Uchanganuzi wa Data.............................................................................19

3.7 Maadili katika Utafiti ...........................................................................20

**SURA YA NNE ......................................................... 21**

**MAUDHUI MAKUU KATIKA TAMTHILIA TEULE.......... 21**

4.0 Utangulizi ........................................................... 21

4.1 Maudhui Makuu katika Mstahiki Meya (2009) ..........................................21

4.1.1 Maudhui ya Uongozi Mbaya ...............................................................21

4.1.2 Maudhui ya Ufisadi...............................................................................24

4.1.3 Maandamano na Migomo ya Wafanyikazi ..........................................25

4.1.4 Maudhui ya Unafiki .............................................................................26

4.1.5 Uchafuzi wa Mazingira.........................................................................27

4.1.6 Ukoloni Mamboleo ...............................................................................27

4.1.7 Ukiukaji wa Haki za Kibinadamu.........................................................28

**4.2 MAUDHUI MAKUU KATIKA TAMTHILIA YA *KIGOGO*.................28**

4.2.1 Uongozi Mbaya.......................................................................................29

4.2.2 Maudhui ya Umaskini...........................................................................31

4.2.3 Ukatili na Udhalimu..............................................................................33

4.2.4 Unafiki na Propaganda ........................................................................34
4.2.5 Ubadhirifu ..................................................................................................35
4.2.6 Uchafuzi wa Mazingira ..............................................................................36
4.2.7 Tamaa na Ubinafsi .....................................................................................38
4.2.8 Maudhui ya Ufisadi ....................................................................................39
4.2.9 Ukiukaji wa Haki za Binadamu ................................................................40
**4.3 MAUDHUI MAKUU KATIKA JAMII ...................................................41**
4.3.1 Maudhui ya Ukoloni Mamboleo ................................................................41
4.3.2 Maudhui ya Uongozi Mbaya ......................................................................43
4.3.3 Kupanda kwa Gharama ya Maisha ............................................................44
4.3.4 Unyakuzi na Matumizi Mabaya ya Mali ya Umma ...................................46
4.3.5 Tamaa na Ubinafsi .....................................................................................46
4.3.6 Ufisadi ........................................................................................................47
4.3.7 Uchafuzi wa Mazingira ..............................................................................49
4.3.8 Migomo na Maandamano ..........................................................................50
**4.4 UCHANGANUZI WA DATA .....................................................................51**
4.4.1 Utangulizi ...................................................................................................51
4.4.2 Uchanganuzi wa Hojaji za Wanafunzi .......................................................51
4.4.3 Kigezo cha Uelewa wa Maudhui ...............................................................55
4.4.4 Manufaa ya Maudhui ya Tamthilia ............................................................60
4.4.5 Kigezo cha Tofauti za Kimaudhui Katika Kazi za Fasihi Teule ...........61
4.4.6 Kigezo cha Uhalisi wa Maudhui ................................................................63
4.4.7 Uchanganuzi wa Hojaji za Walimu ...........................................................67
4.4.8 Kigezo cha Miaka ya Kufunza ...................................................................73
4.4.9 Kigezo cha Changamoto za Kufunza Tamthilia za Utahini Shuleni. ....75
4.4.10 Kigezo cha Ufaafu wa Maudhui ...............................................................78
4.4.11 Kigezo cha Uhalisia wa Maudhui .............................................................79
**4.5 Hitimisho ....................................................................................................80**
**SURA YA TANO ...................................................................................... 80**

MUKHTASARI, MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........................................................... 80

5.0 Utangulizi .......................................................................... 80

5.1 Mukhtasari ..................................................................................... 81

5.2 Matokeo ya Utafiti ......................................................................... 83

5.3 Mchango wa Utafiti ........................................................................ 84

5.4 Matatizo ......................................................................................... 84

5.5 Mapendekezo ................................................................................. 85

MAREJELEO .................................................................. 85

VIAMBATISHO .............................................................. 89

**ORODHA YA MAJEDWALI**

Jedwali 3.1: Wahojiwa ........................................................................................ 17

Jedwali 4.1: Kupanda kwa Gharama ya Maisha .................................................... 44

Jedwali 4.2: Madai ya Ufisadi miaka 2009-2018 .................................................. 48

Jedwali 4.3: Kidato cha Mtafitiwa ........................................................................ 52

Jedwali 4.4: Matokeo ya Jinsia ya Mtafitiwa ........................................................ 54

Jedwali 4.5: Kidato cha Tatu ................................................................................ 56

Jedwali 4.6: Kidato cha nne .................................................................................. 58

Jedwali 4.7: Jinsia za Wanafunzi .......................................................................... 68

Jedwali 4.8: Kigezo cha Uelewa wa Maudhui na Wanafuzi ................................. 70

Jedwali 4.9: Jukumu la jinsia katika kutambua Maudhui ...................................... 72

Jedwali 4.10: Jedwali ya Majibu ya Miaka ya Kufunza ........................................ 74

Jedwali 4.11: Majibu ya Changamoto za Kufunza Tamthilia ................................ 76

Jedwali 4.12: Kulinganisha na Kulinganua Maudhui ya Tamthilia ....................... 77

**ORODHA YA MICHORO**

Mchoro 1: Majibu ya Kidato cha Wanafunzi ........................................................ 53

Mchoro 2: Matokeo Kuhusu Kigezo cha Jinsia ya Mtafitiwa ................................ 55

Mchoro 3: Idadi ya Wanafunzi ........................................................................57
Mchoro 4: Idadi ya Wanafunzi Kidato cha Nne ..........................................................59
Mchoro 5: Manufaa ya Maudhui ya Tamthilia ............................................................61
Mchoro 6: Tofauti Za Kimaudhui Katika Kazi Za Fasihi Teule .................................62
Mchoro 7: Uhalisi wa Maudhui ....................................................................................66
Mchoro 8: Jinsia za Wanafunzi.....................................................................................69
Jedwali 9: Uelewa wa Maudhui na Wanafuzi..............................................................71
Mchoro 10: Jukumu la Kijinsia Katika Kutambua Maudhui.......................................73
Mchoro 11: Majibu ya Miaka ya Kufunza...................................................................75
Mchoro 12: Kulinganisha na Kulinganua Maudhui ya Tamthilia ...............................78

## ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatisho:1: Kibali cha Kutafiti ..............................................................................89
Kiambatisho 2: Fomu A ya Kukubali Kushiriki Utafiti...............................................90
Kiambatisho 3: Fomu B ya Kukubali Kushiriki Utafiti:..............................................91
Kiambatisho 4: Mfano (A) wa Majibu ya Hojaji za Walimu ......................................92
Kiambatisho 5: Mfano (A) wa Majibu ya Hojaji za Walimu - Unaendelea ................93
Kiambatisho 6: Mfano (B) wa Majibu ya Hojaji za Walimu.......................................94
Kiambatisho 7: Mfano (B) wa Majibu ya Hojaji za Walimu - Unaendelea ................95
Kiambatisho 8: Mfano (A) wa Majibu ya Hojaji za Wanafunzi..................................96
Kiambatisho 9: Mfano (A) wa Majibu ya Hojaji za Wanafunzi - Unaendelea ...........97
Kiambatisho 10: Mfano (B) wa Majibu ya Hojaji za Wanafunzi................................98
Kiambatisho 11: Mfano (B) wa Majibu ya Hojaji za Wanafunzi - Unaendelea..........99
Kiambatisho 12: Ratiba ya Kazi ..................................................................................100
Kiambatisho 13: Shule Zilizohojiwa ..........................................................................101
Kiambatisho 14: Makisio ya Bajeti.............................................................................102

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

## 1.1 Usuli wa Mada

Kulingana na Msokile (1992) fasihi ni sanaa inayotumia lugha kiubunifu ili kueleza tajriba mbalimbali za maisha ya wanajamii. Kulingana na Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kuwa fasihi inawasilisha hali, maingiliano, mivutano na mikinzano miongoni mwa binadamu na mazingira yake. Fasihi inawasilisha maudhui yenye mguso kwa wanajamii kupitia kwa lugha. Fasihi inatumiwa kupitisha hisia za mwandishi juu ya mambo yanayomwathiri yeye au jamii yake kwa lengo la kustarehesha au kufunza hadhira yake. Tamthilia ni mojawapo ya vipengele vya fasihi na maudhui yake yanastahili kuonyesha hali ya halisi katika jamii. Utafiti huu ulilenga kubaini halisi wa maudhui katika tamthilia na iwapo vitabu vya tamthilia vinafaa katika shule za upili.

Njogu na Chimera (1999) wanafafanua kuwa msanii ni zao la jamii na anajaribu kuwasilisha matukio ya jamii katika uhalisia wake. Msanii anachota maudhui yake kutokana na hali halisi zinazomzunguka za kitamaduni, kiuchumi, kijamii na kisiasa. Kupitia kwa kazi za fasihi tunapata picha kamili ya jamii ya kisasa kwa kuwa hakuna fasihi inayoibuka katika ombwe tupu. Kila kazi ya fasihi ni zao halisi la jamii na inaonyesha kuwepo kwa jamii kupitia kwa masuala halisi yayoendelezwa na wanajamii. Maudhui ambayo Arege (2009) na Kea (2016) wanaibua ni tajriba yao ya kijamii na yanaeleza ukweli kuhusu maisha ya jamii. Kwa dhana hii ya kuwa msanii ni zao la kijamii, utafiti ulipata msukumo wa kutaka kujua uhalisi wa matukio makuu katika jamii kupitia wasanii tofauti wa kazi za tamthilia.

Ni kwa sababu hii basi utafiti ulilenga kutathimini uhalisi wa maudhui makuu kwa vile fasihi ni zao la wakati na kadiri jamii inavyobadilika ndivyo kazi ya fasihi inavyobadilika zikiwemo tamthilia za kiswahili. Sababu hii ya mabadadiliko ya fasihi kutegemea wakati iliyotupa mwelekeo wa usuli wa mada yetu kutathimini maudhui ya tamthilia tahiniwa katika shule za upili kwa kipindi kati ya miaka ya 2013 na 2018.

Utafiti uliwatumia wanafunzi wa kata ndogo ya Nzambani kaunti ya Kitui ambalo ndilo eneo la utafiti kama kiwakilishi cha jamii nzima ya Kenya, kuangalia ufaafu wa maudhui makuu kwa jamii na uhalisia wake katika jamii ya sasa.

Tamthilia za kisasa kwanza, zinaibua hali halisi; taratibu za maisha kama vile siasa, ufisadi, ukoloni mamboleo, umaskini, miongonimwa masuala mengine yanachunguzwa kwa jicho la ukali na udhaifu wake unafichuliwa bila uoga. Haya ni masuala halisi ambayo ni wazi katika jamii ya leo na ambayo hata wanajamii wa elimu ya chini wanaweza kuyatambua. Pili, wahusika katika tamthilia za kisasa wanaingiliana na jamii pana kwa kuendeleza maudhui halisi katika jamii. Vilevile, wahusika halisi wanatumiwa kinyume na wahusika wanyama waliotumiwa awali uhalisia wa wahusika unatokea kupitia kwa, maudhui ambayo wanaendeleza na ambayo baada ya wanajamii kusoma kazi za tamthilia za karne anaweza kutoa mifano halisi katika jamii. Kwa vile tamthilia zinazoandikwa zinalenga halisi wa jamii utafiti utalithimini ufaafu na halisi wa maudhui katika jamii kwa kuangalia maudhui makuu katika tamthilia za *Mstahiki Meya* ( Arege, 2009)na *Kigogo* ( Kea, 2016)na zaidi kuchunguza Maudhui halisi katika jamii wakati wa kusomwa na kufunzwa kwa tamthilia hizi.

Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu fasihi ya Kiswahili haswa tamthilia. Suala la maudhui limeshughulikiwa kwa wingi japo kwa namna nyingi watafiti wa awali wameshughulikia uwasilishaji wa maudhui katika tamthilia tofauti na utafiti huu ambao ulishughulikia maudhui makuu pekee katika tamthilia teule za *Mstahiki Meya* (Arege, 2009)na *Kigogo* (Kea, 2016) kwa nia ya kutaka kujua iwapo tamthilia zinazoteuliwa kufunzwa na kutahiniwa katikashule za upili zinaangazia hali halisi ya maudhui ya jamii. Kulingana na maelezo kuwa msanii hupitisha hisia juu ya mambo yanayomwathiri yeye au jamii nzima akilenga kustarehesha au kufunza wasomaji wake. Utafiti uliweza kubaini ufaafu wa tamthilia ya *Mstahiki Meya* ( Arege, 2009)na *Kigogo* ( Kea, 2016) ili kujibu swali la ni kwa nini kazi za tamthilia za utahini huwa na maudhui sawa tofauti ikiwa mtindo wa uwasilishaji. Kwa kuchunguza ufaafu wa maudhui mtafiti alibaini kuwa licha ya burundani kutoka kwa uelendi wa matumizi ya lugha, waandishi Arege (2009) na Kea (2016) wamefanikiwa pakubwa kuelimisha jamii kuhusu maudhui ya kijamii.

Mtafiti alisoma na kuchambua maudhui katika sampuli ya tamthilia za karne ya ishirini na moja *Mstahiki Meya* (Arege, 2009)na *Kigogo* (Kea, 2016). Zaidi alichunguza halisi wa maudhui ya tamthilia hizi katika jamii haswawakati wa utahini wa tamthilia. Walimu na wanafunzi wa shule za upili kidato cha tatu na cha nne walitumiwa kama kiwakilishi cha jamii kupata hali halisi ya mambo yanayomwathiri mwanajamii.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Kulingana na ripoti iliyotolewa na Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi(Ethics and Anti-corruption Commission) (2018), kati ya asilimia sitini na tatu ya wahojiwa waliotafuta huduma katika maofisi ya umma, asilimia thelathini na nane nukta tisa walihusika katika ufisadi kwa hiari au kwa kushinikizwa. Mojawapo ya mapendekezo yaliyotolewa na tume hii ni pamoja na kuimarishwa kwa nyenzo za uhamasishaji umma. Ni wazi kuwa njia mojawapo ya kuwahamasisha wanajamii wachanga kuhusu ufisadi na maovu mengine ya jamii ni kuoanisha suala hili na masomo katika mtaala. Utafiti ulitaka kudhihirisha iwapo maudhui yanayoshughulikiwa na vitabu hivi teule yanaakisi hali halisi ya jamii. Bali na ufisadi, visa vya mauaji na dhuluma kwa wasichana na wanawake vimekithiri.

Kulingana na ripoti iliyotolewa na *Global Study of Homicide* (United Nations Office on Drugs and Crime [UNDOC], 2018), asilimia thelathini na nane nukta tano ya wasichana na wanawake walio na umri wa kati ya miaka kumi na mitano hadi arobaini na tisa nchini Kenya wamedhulumiwa angalao mara moja katika maisha yao. Ni muhimu basi kuchunguza iwapo masuala haya yanayoikumba jamii yanaibuliwa na waandishi wa fasihi ili kujaribu kukielekeza kizazi kichanga katika mkondo wa kimaadili unaokubalika. Ibainike kuwa mtaala unapaswa kukidhi mahitaji ya jamii kwani kwa mujibu wa ruwaza ya 2030, masuala muhimu yanayopaswa kuzingatiwa na mfumo wa elimu ni yale yanayomkuza mhusika kijamii.

Kuwepo kwa maudhui sawa katika kazi za wasanii tofauti, wasanii wa jinsia tofauti na wasanii ambao miaka yao ya uandishi ni tofauti ndilo tatizo kuu la kazi hii. Lengo la kutaka kutathimini halisi wa maudhui katika tamthilia zilizoteuliwa kutahiniwa katika shule za upili Kwa vipindi tofauti ambazo ni tamthilia ya *Mstahiki Meya*

(Arege, 2009) na *Kigogo* (Kea, 2016) ilisaidia kutatua tazizo la mtafiti. Sampuli hii ya tamthilia za karne na kazi za wandishi chipukizi zilitumika kuwakilisha tamthilia ambazo zinateuliwa kutahiniwa katika shule za upili katika karne ya ishirini na moja. Maudhui sawayanayojitokeza ni kama vile maudhui ya ukoloni mamboleo, hali duni ya maisha, tamaa na ubinafsi miongoni mwa maudhui. Maudhui hayo pia yanaonyesha hali halisi katika jamii kwa kiasi kikubwa.

## 1.3 Madhumuni ya Utafiti

1. Kutathimini matukio makuu ya kijamii katika vipindi vya kuteuliwa na kutahiniwa kwa tamthilia kwa *Mstahiki Meya* (Arege, 2009)na *Kigogo* (Kea, 2016).
2. Kubainisha maudhui makuukatika tamthilia ya *Mstahiki Meya* (Arege, 2009 na *Kigogo* (Kea, 2016).
3. Kulinganisha maudhui yanayoibuliwa na tamthilia ya *Mstahiki Meya* (Arege, 2009 na *Kigogo* (Kea, 2016) na matukio halisi ya jamii wakati wa vipindi husika.
4. Kubaini ufaafu wa tamthilia: Mstahiki *Meya* (Arege, 2009)na *Kigogo* (Kea, 2016)kwa kutumia kigezo cha maudhui, wanafunzi na walimu wa shule za upili kama kiwakilishi cha jamii kwa mwongozo wa nadharia ya uhalisia kuchunguza uhalisi wa maudhui makuu katika tamthilia hizi.

## 1.4 Maswali ya Utafiti

1. Ni maudhui yapi makuu yanayojitokeza katika tamthilia za *Mstahiki Meya (*Arege, 2009) na *Kigogo* (Kea, 2016)?
2. Ni masuala yapi makuu ya kijamii yaliyosheheni katika kipindi cha kuteuliwa kwa tamthilia za *Mstahiki Meya (*Arege 2009) na *Kigogo* (Kea 2016)?
3. Je, kuna ulinganifu wa uhalisi kati ya maudhui ya tamthilia na maudhui katika jamii katika kipindi husika (2013-2019)?

## 1.5 Upeo na Mipaka

Utafiti ulitumia tamthilia mbili za karne ya ishirini na moja; *Mstahiki Meya (*Arege, 2009) na *Kigogo*(Kea, 2016*).* Tamthilia hizi za karne mpya na zinalenga mambo

halisi katika jamiiKipindi cha miaka ya kutahiniwa kwa (2013-2019). Utafiti ulilenga maudhui makuu na sawa katika tamthilia teule *Mstahiki Meya* (Arege, 2009) na *Kigogo* (Kea, 2016). Utafiti pia ulitathimini uhalisi wa maudhui hayo katika jamii ya karne ya ishirini na moja. Mtafiti alipata data kutoka kwa walimu na wanafunzi wa kidato cha tatu na nne, shule za upili za kata ndogo ya Nzambani kaunti ya Kitui kama kiwakilishi cha jamii. Sababu ya kuchagua eneo hili ni vile shule nyingi katika eneo hili ni za mseto. Wanafunzi na walimu walichukuliwa katika kidato cha tatu na nne kwasababu wanaingiliana moja kwa moja kazi za tamthilia hivyo walisaidia kutoa data iliyohitajika. Data iliyopatikana hapa ilikuwa na maoni ya jinsia tofauti katika jamii.

## 1.6 Sababu za Kuchagua Mada

Uteuzi wa mada ulichochewa na sababu kuwa waandishi Arege (2009) na Kea (2016) ni miongoni mwa waandishi wa karne ya ishirini na moja hivyo basi kazi hizi zina mambo mengi ya kutafitiwa kama vile kusoma na kuchambua maudhui katika tamthilia hizi kwa kuyalinganisha na kuyalinganua ili kupata maudhui ambayo ni sawa. Aidha, tamthilia hizi zimegusia mambo muhimu yanayoiathiri jamii ya karne ya ishirini na moja na hivyo kupitia maudhui ya kazi za tamthilia malengo ya elimu kwa jamii yatakuwa yameafikiwa kwa kuielimisha jamii.

Pili, tamthilia zilipata nafasi ya kuteuliwa kama vitabu vya kutahiniwa katika mitihani ya kitaifa ya kidato cha nne: *Mstahiki Meya* (Arege, 2013) na ile ya *Kigogo* (Kea, 2018). Ni kwa sababu hii basi utafiti huu uliazimia kujua zaidi uhalisi wa maudhui na mojawapo wa vigezo vilivyotumiwa kuchagua tamthilia hizi katika karne hii ya ishirini na moja na ufaafu wa maudhui kwa wanafuzi wa shule za upili kama kiwakilishi cha jamii nzima katika kipindi cha kuteuliwa kwa tamthilia hizi.

Tatu, kazi yoyote ya fasihi hulenga kupitisha ujumbe kwa hadhira kupitia kwa dhamira ya msanii wa kazi ya fasihi. Maudhui yale yanastahili kuwa na manufaa kwa jamii. Mada ilichaguliwa ili kubaini maudhui makuu na sawa ya tamthilia teule na kisha kuyalinganisha na masuala makuu katika jamii katika kipindi cha utahini. Lengo lilikuwa kubaina ufaafu wa maudhui yale kwa jamii na kama maudhui ya kazi za tamthilia yanaelimisha.

## 1.7 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utasaidia katika kutoa maelekezo kwa uteuzi unaofaa wa vitabu vya kutahiniwa kwa kuoanisha maudhui makuu na sawa ya tamthilia za *Mstahiki Meya* (Arege, 2009) na ile ya *Kigogo* (Kea, 2016*)* na masuala makuu katika jamii katika kipindi hiki cha utahini wa tamthilia hizi. Pili utafiti utasaidia katika kuzifahamu zaidi kazi za fazihi hasa tamthilia za Kiswahili na nafasi yake katika jamii kwa kuangazia uhalisi wa maudhui katika jamii na kuyalinganisha na yale ya tamthilia teule. Tatu utafiti utasaidia waandishi wa tamthilia kuandika kazi zenye maudhui yanayoisawiri jamii husikakihalisia.Wanafunzi na watafiti wa baadaye katika taaluma za fasihi watautumia utafiti huu kama sehemu ya marejeleo ya kuwasaidia kupata tatizo la utafiti na kuimarisha mapitio ya kazi tangulizi za tamthilia za Kiswahili.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDISHI

## 2.0 Utangulizi.

Sura hii ilishughulikia tafiti za awali kuhusiana na mada hii ya utafiti huu ili kupata msingi na maelekezo ambayo yalisaidia kukamilisha utafiti huu. Mtafiti pia alifafanua nadharia ya uhalisia pamoja na mihili yake ambayo ndiyo iliyoongoza utafiti.

## 2.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Suala la maudhui katika tamthilia limeshughulikiwa kwa wingi japo kwa namna tofauti. Utafiti huu ulitathmini maudhui makuukatika tamthilia teule za *Mstahiki Meya* (Arege, 2009) na ile ya *Kigogo* (Kea, 2016*)* na uhalisi na ufaafu wa maudhui yale katika jamii hii ya karne ya ishirini na moja. Utafiti ulitumia walimu na wanafunzi wa shule za upili kama kiwakilishi cha jamii n katika kuangalia ufaafu wa maudhui yale shuleni na iwapo wanafunzi wanaweza kubaini maudhui yale katika muktadha halisi wa kijamii.

Utafiti wa Fridah (2017), kuhusu Uhakiki wa Mtindo katika Tamthilia za Arege*: Kijiba cha Moyo*(2009), *Chamchela*(2007)na *Mstahiki Meya*(2009) ulisaidia sana utafiti huu kuelewa zaidi kumhusu mwandishi Timothy Arege. Tofauti ya utafiti huu na wa Fridah ni kwamba huu ulichunguza maudhui kwa kulinganisha kazi za wasanii tofauti kwa nyakati tofauti lakini yeye alichunguza tamthilia za Timothy Arege pekee.

Utafiti wa Syekei  (2017), kuhusu nafasi na athari ya kiongozi wa kike katika tamthilia teule za kiswahili;*Kilio cha Haki* (Mazrui, 1981), *Sudana* (Mazrui na Njogu, 2006), *Posa za Bikisiwa* (Mohamed na King'ei, 2008), na *Pango* (Wamitila; 2003) ulisaidia mtafiti kuelewa dhana ya tamthilia kwa jumla katika utafiti. Tofauti ya utafiti huu na wake ni kuwa yeye alishughulikia maudhui ya nafasi ya mwanamke katika uongozi lakini utafiti huu ulitathimini maudhui kwa jumla kwa lengo la kujua ufaafu na Uhalisia wake katika tamthilia tahiniwa.

Ngesa na wengine (2015), walichunguza Mwingilianomatini katika Tamthilia za Kiswahili:*Mashetani* (Hussein 1971) na *Kijiba cha Moyo* (Arege 2009). Tathmini hii

inaongozwa na nadharia ya mwingilanomatini .Utafiti wao ulimfaa mtafiti kuelewa dhana ya matini na haswa maudhui ambayo ndiyo nguzo kuu ya utafiti huu. Zaidi mtafiti alisaidika kumwelewa mwandishi Timothy Arege ambaye ni mwandishi wa tamthilia ya *Msitahiki Meya* (Arege 2009)**.**

Bosire (2016), alitafitia mwingilianomatini katika kati ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (Gogol 1971) na *Mstahiki Meya* (Arege 2009). Bosire kwa kuongozwa na nadharia ya mwingiliano matini alilinganisha matini ya tamthilia mbili teule za zilizondakikwa na waandishi katika vipindi tofauti. Utafiti wake ulinisaidia kuelewa dhana ya maudhui na kutafiti mada tofauti ya utathimini wa maudhui, uhalisia na ufaafau wa maudhui yale katika karne ya ishirini na moja.

Senkoro (1988), alihakiki maudhui na mtindo katika mashairi ya watunzi mbalimbali akiongozwa na nadharia ya Umaksi. Katika utafiti wake, alishughulikia maudhui tofautipamoja na vipengele mbalimbali vya kimtindo na kuonyesha jinsi mtindo unavyosaidia kuwasilisha mawazo ya msanii. Tofauti ni kuwa yeye alitafitia mashairi kwa kutumia nadharia ya umaksi kinyume na utafiti huu ambao ulitathimini maudhui katika tamthilia za karne ya ishirini na moja na uhalisi wa maudhui katika jamii kwa kutumia nadharia ya uhalisia.

King’ei (2012), kwenye tahakiki ya *Mstahiki Meya*,wameelezea mukhtasari wa maonyesho, uhusika, maudhui, dhamira, na mtindo wa tamthilia ya *Mstahiki Meya*(2009). Hata hivyo, tahakiki yake ni ya kijumla na ililenga kuwaongoza watahiniwa wa shule za upili kujiandaa kwa mitihani ya fasihi kwa vile tamthilia hii ni mojawapo ya tamthilia za utafiti. Mwongozo wake ulimfaa mtafiti kuelewa dhana ya maudhui, ufaafu na uhalisi wake katika jamii ya karne ya ishirini na moja.

Salem (2013) alitafiti kuhusu maudhui na fani katika tamthilia za Kiswahili kwa kulinganisha tamthilia ya *Mashetani* (E. Hussein 1971) na *Kivuli kinaishi* (S.Mohamed 1990). Utafiti huu ulilinganisha na kulinganua maudhui na fani katika tamthilia teule tofauti na huu wa sasa ambao ulilinganisha maudhui tu kisha kutathimini uhalisia na ufaafu wake katika jamii.

Okwena (2013) alitafiti matumizi ya jazanda katika tamthilia tatu teule za Arege: *Kijiba cha Moyo* (2009), *Chamchela* (2007)na *Mstahiki Meya* (2009). Alichanganua aina mbalimbali za jazanda alizotumia mwandishi huyu kuwasilisha maudhui yake. Utafiti wake ulisaidia kuelewa dhana ya maudhui katika tamthilia teule tamthilia za *Mstahiki Meya* (Arege, 2009) na ile ya *Kigogo* (Kea, 2016*)* ambazo ni miongoni mwa tamthilia za utahini karne ya ishirini na moja katika shule za upili nchini Kenya.

Ongarora (2007),alishughulikia hadithi fupi ya Mohamed, S.A*Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine*(2005). Mtafiti huyu alishughulikia mtindo katika uwasilishaji wa maudhui akiongozwa na nadharia ya kimtindo.Tofauti ni kuwa utafiti wake ulishughulikia kipera cha hadithi fupi ilhali utafiti huu umeshughulikia tamthilia. Hata hivyo tafiti wake ulisaidia katika kuelewa maana ya mtindo na vipengele vyake na jinsi vinavyosaidia kukuza maudhui.

Kwa upande mwingine, Muthoni (2014) kuhakiki mtindo na maudhui katika riwaya ya *Tikitimaji* ya Wamitila (2013). Muthoni alichunguza maudhui na matumizi ya lugha katika riwaya hii na kubainisha kuwa ujumbe wa mwandishi hueleweka kwa utegemezi wa mbinu za lugha alizotumia. Utafiti wa Muthoni ulifaidi huu pakubwa kuelewa dhana yamaudhui. Tofauti ya utafiti huu na wake ni kwamba yeye yuko alitafiti kipera cha riwaya ilhali huu ulilenga kutathimini maudhui sawa katika tamthilia za *Mstahiki Meya* (Arege, 2009) na*Kigogo* (Kea, 2016) ambazo ni kiwakilishi cha tamthilia za karne ya ishirini na moja na zilizoteuliwa kutahiniwa katika vipindi tofauti.

Maoni haya yaliyotolewa na wataalamu na wahakiki mbalimbali katika tafiti zao yaliupa utafiti huu maelezo kuhusu nadharia ya uhalisia na vipengele mbalimbali vya kutathmini maudhui katika tamthilia teule za *Mstahiki Meya* (Arege, 2009) na *Kigogo* (Kea, 2016).Maoni yao yaliusukuma utafiti huu mbele hadi kiwango cha kukamilika kwa kuupatia maelezo kuhusu vipengele vya kutathmini maudhui, uhalisia wa maudhui katika tamthilia za karne ya ishirini na moja *Mstahiki Meya* (Arege, 2009) na *Kigogo* (Kea, 2016*).*

## 2.2 Yaliyoandikwa kuhusu Maudhui

Maudhui katika kazi ya fasihi ni jumla ya mawazo yote yanayozungumzwa pamoja na mtazamo wa mwandishi juu ya mawazo hayo. Maudhui hujumuisha mawazo pamoja na mafunzo mbalimbali yanayomsukuma msanii hadi akatunga kazi fulani ya kifasihi. Vipengele vya maudhui ni pamoja na dhamira, migogoro, falsafa, ujumbe na msimamo wa mwandishi wa kazi za fasihi kwa mujibu wa muktadha wa jamii).

Kulingana na Gatakaa (2012), maudhui ni ujumbe muhimu unaojitokeza katika kisa kizima cha kazi ya fasihi. Yaani, kile kitu, mtu, sifa ya kibinadamu au hali ya maisha inayozungumziwa hadithini. Tamthilia za *Mstahiki Meya* (Arege, 2009) na *Kigogo* (Kea, 2016*)* zinashughulikia maudhui kwa upana kwa kuzingatia uhalisi na ufaafu wa wa maudhui haya katika jamii.

Mbatiah (2010), anaeleza maudhui kama jumla ya masuala yanayoshughulikiwa katika kazi ya fasihi. Kwa kauli hii ya Mbatiah, ni kweli kwa kuwa maudhui ni maswala makuu yanayojitokeza katika kazi yoyote ya fasihi na hufafanuliwa kadri ya uwezo wa mwandishi kwa kutumia mihimili yote yakuyaendeleza maswala hayo makuu. Wasanii Arege (2009) na Kea (2016) wamefanikiwa kuendeleza maudhui wakilenga jamii pana katika tamthilia teule za utafiti huu.

Wamitila (2008),anasema kuwa maudhui ni dhana pana inayoweza kuelezwa kwa jinsi mbili ambazo kimsingi zinahusiana. Mwanzo ni kuwa maudhui ni jumla ya maswala au mambo yanayoshughulikiwa katika kazi ya fasihi. Maswala haya ni yale yanayotokana na jinsi mwandishi au mtunzi anavyoikuza mada ambayo ni msingi wa utunzi wa kazi yake. Jinsi ya pili, Wamitila anayatumia maudhui kukirejelea kiwango cha maana cha matini au kazi ya fasihi. Maelezo ya Wamitila kuhusu maudhui yaliupa utafiti huu msingi wa kuelewa maudhui katika tamthilia teule na kisha kuyalinganisha na maudhui ya kijamii.

Kwa maoni ya Njogu na Chimerah (1999), maudhui ni mawazo ya mtunzi kwa mkabala wa muktadha.Maudhui ya kazi ya kifasihi yanastahili kuwa halisi na yanayolenga jamii ya leo.Kauli hii ya Njogu na Chimera ilisaidia utafiti huu kuelewa dhana ya maudhui kimuktadha na kwa kuongozwa namaudhui ya tamthlia za *Mstahiki*

*Meya* (Arege, 2009) na *Kigogo* (Kea, 2016*)* maoni ya waandishi hawa yanaonyesha wazi mawazo ya mtunzi kimuktadha na kwa hali ya Uhalisi wa kijamii hasa katika karne ya ishirini na moja.

Owallah (2013), ameshughulikia suala la mandhari na maudhui katika *Utenzi wa Nabii Isa*(1977).Anasema kwamba mtunzi anaporejelea mahali panapotendekea jambo fulani pamoja na wakati wa kutendeka kwa tendo hilo basi anarejelea mandhari. Basi mandhari hurejelea mahali na wakati ambapo matukio hutokea katika kazi za kifasihi. Kutokana na maelezo hayo maudhui huongozwa na mandhari au hali inayomzunguka mwanadamu kuathiri maisha yake kupitia kwa maudhui ilikuwa rahisi kwa mtafiti kuelewa maudhui katika kazi teule na kuyalinganisha na maudhui halisi ya kijamii.

Ntarangwi (2004), anadai kwamba wakati mwingi wahakiki hushughulikia mambo mawili makuu katika fasihi yale yanayozingatiwa na kuendelezwa (maudhui) na jinsi yanavyoendelezwa (fani). Kwa kawaida, maudhui ni ujumbe muhimu unaojitokeza katika kisa kizima katika kazi ya fasihi. Kazi moja ya fasihi yaweza kuchukua maudhui mbalimbali pia. Ni nadra kupata kazi ya fasihi ambayo haizungumzi jambo fulani, na kama ipo, basi itakuwa vigumu kukubalika kama kazi halisi ya fasihi. Hivyo basi, kile kinachozungumziwa katika kazi ya fasihi ndicho tunachokiita maudhui. Huenda ikawa ni ukoloni mamboleo, ufisadi, dhuluma, ukoloni, tamaa na ubinafsi. Mtafiti kwa maelezo hayo alisaidika kuelewa dhana ya maudhui kwa upana.

Ni dhahiri kwamba maudhui huchukua hali mbalimbali za maisha lakini aghalabuutapata hayo maudhui yanachukuana na hali ya kisiasa, kiuchumi au kijamii, katika jamii husika na katika wakati maalum wa kihistoria. Tamthilia za *Mstahiki Meya* (Arege, 2009) na *Kigogo* (Kea, 2016)zinamulika kwa kina hali halisi ya maisha katika jamiii ya leo kwa kupiga darubini ya maswala halisi yanayozunguka wanajamii.

Mohammed (1984) (akinukuliwa na Preston, 2014) anamithilisha mtiririko wa maudhui katika fasihi na mtiririko wa mto anaposema; mtiririko wa maudhui na dhamira ya fasihi waweza kumithilishwa na mtiririko wa mto mkubwa. Kutokana na

mawazo hayo ya Mohammed, ni wazi kwamba kazi yoyote ya fasihi huzingatia kipembe fulani cha maisha, kwani kazi hiyo sawa na mto haiwezi kutambaa kila eneo la maisha. Ni muhimu kutaja kwamba mambo anayoyazungumzia mtunzi, yanapaswa kuafikiana na hali ya maisha ya wanaolengwa na kazi hiyo.

Maudhui katika fasihi yanachotwa kutoka kwa hali halisi ya maisha ya jamii lengwa, na kwa sababu mtunzi pia ni mwanajamii, ataandika kuhusu jamii husika kwa kuegemea maisha ya jamii hiyo kisiasa, kiuchumi na kijamii katika wakati maalum wa kihistoria. Mtunzi ana uhuru wa kuchagua jambo lolote lile bora tu liwe litachukuana na matarajio na tajiriba za hadhira yake.

Mtunzi vilevile anapaswa kutunga kuhusu mambo yanayohusu jamii. Lakini mtunzi hawezi kushughulikia kila kitu maishani, yeye huchagua ni mkondo gani wa maisha atakaozingatia; na hufanya hivyo kwa mpango fulani. Mathalan, katika kazi za kifasihi za *Mstahiki Meya* (Arege, 2009) na *Kigogo* (Kea, 2016)ambapo watunzi wameangazia hali halisi ya kijamii kupitia maudhui yao haswa katika karne hii ya ishirini na moja.

Waandishi Timothy Arege na Pauline Kea wamefanikiwa kuyakuza maudhui katika tamthilia zao kwa hali ya upana kwa kuzingatia hali ya uhalisia wa maudhui yale kijamii. Maelezo hayo ya maudhui yalimsaidia mtafitikuweza kuelewa usimulizi wa waandishi wa tamthlia za *Mstahiki Meya* (Arege, 2009) na *Kigogo* (Kea, 2016*)* na kuweza kubaini maudhui ya kazi hizi na kishakutathimini uhalisi wa wake katika jamii kwa kipindi hiki cha karne ya ishirini na moja.

## 2.3 Nadharia ya Uhalisia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhalisia. Kulingana na Mwangi (2018), nadharia hii iliasisiwa katika karne ya kumi na tisa na kufafanuliwa zaidi na Goffman (1952). Lucaks (1963) anaeleza kuwa mwandishi anasukumwa na njia ya kuusawiri uhalisia katika ukamilifu na wakati wake maalumu. Mwandishi anapaswa kupenya chini ya picha za kijuujuu na kudhihirisha mifanyiko ya mabadiliko yaliyopo. Uhalisia wa maisha katika jamii unapewa msingi mkubwa wa uandishi kuhusu

uhalisia. Tukio, mhusika au mandhari huelezwa kama vya kihalisia ikiwa vinafanana na sura fulani ya maisha.

Wamitila (2002) anaeleza kuwa uhalisia unasisitiza usawiri wa maisha ya jamii kwa uaminifu na usahihi mkubwa.Waaandishi wa kazi za tamthilia teule wanatoa picha za wahusika, matukio na mandhari ambayo kwa kiasi kikubwa na uhalisia wa jamii ya mwandishi anayehusika. Fasihi yoyote lazima ionekane kama kioo cha jamii. Hivyo basi, lazima jamii iweze kujitazama na kujiona kupitia fasihi ambayo ni zao la jamii. Msingi wa nadharia hii ni kuwa sanaa iwakilishe ukweli na kuwakilishwa kwa maneno halisi, iwe aminifu na ionyeshe hali halisi ya mazingira.

Kulingana na Ntarangwi (2004), nadharia hii katika upana wake, humaanisha uwakilishi wa uhalisi wa mambo katika fasihi. Nadharia hii ilizuka katika karne ya kumi na tisa kwa sababu za kupinga mkondo wa ulimbwende. Mhalisia huamini katika matokeo ya mambo na ukweli anaouzingatia ni ule unaoweza kuonekana na kuthibitishwa kwa tajiriba. Vilevile, wahalisia huiamini demokrasia kama hali ya maisha, na malighafi anayochagua kueleza maisha ni yale ya kawaida, ya kadiri na ya kila siku. Hivyo basi uhalisia hujikita katika mambo yaliyopo, tukio mahsusi na matokeo yanayoweza kuthibitika.

Imani ya mhalisia ni kwamba kazi ya fasihi yapaswa kuwaweka wanajamii husika katika ulimwengu wao wa kawaida, wa kweli, na halisi. Hivyo basi hata picha za ulimwengu atakazoumba msanii, zapaswa kudhihirisha hali hiyo. Kama ilivyotajwa awali, uhalisia ulizuka ili kupinga ulimbwende ambao ulizingatia mambo ya kihisia na halisi maishani.

Wahalisia wanaona kwamba kazi ya fasihi yapaswa kuwa sahihi, iliyo wazi na inayozingatia maswala halisi moja kwa moja bila kupiga chuku. Maswala ya kati maishani huhusu maadili na hivyo basi msanii hana budi kuyazingatia kwa kiwango fulani cha uteuzi. Wahalisia wanashikilia kwamba msanii anapaswa kuteua kazi yake akiwa na nia ya kuendeleza maswala yake kama yanavyowahusu watu katika hali halisi za maisha. Mwelekeo huu wa uhalisi katika utunzi unamfanya mhalisia

kumwona mhusika kama kiungo muhimu sana katika kazi ya fasihi. Hivyo basi anazingatia saikolojia ya wahusika katika hadithi.

Mhakiki anayezingatia nadharia hii ya uhalisia, hupembua namna mtunzi alivyodhihirisha uhalisi wa mambo kupitia maudhui aliyoyazingatia na wahusika aliowasawiri. Hivyo basi, mhakiki hutazama jinsi ukweli ulivyodhihirishwa katika juhudi za mtunzi za kuchora hali halisi ya mambo katika wakati maalum.

Kwa muhtasari basi msanii anatarajiwa kusawiri wahusika, matukio na mandhari yanayokubalika na kuaminika katika jamii ya wakati wake. Ufahamu wa mazingira na maisha anayoyalenga mtunzi ni nguzo muhimu kwa mhakiki wa kihalisia. Shida inayoletwa na nadharia hii ni kuchukulia kwamba uhalisi na maana yake hauna utata wowote katika jamii yoyote; ni kwamba unachukulia kuwa watu wote katika jamii hiyo waona uhalisi mmoja na kuwa na fasili sawa kuhusu maisha yao.

Katika utafiti huu kwa kutumia tamthilia teule ulitathimini maudhui katika tamthilia teutahiniwa katika shule za upili nchini Kenya uhalisina ufaafu wa maudhui hayo kwa kuyalinganisha na kuyalinganua na maudhui halisi ya kijamii katika karne hii ya ishirini na moja. Mtafiti atatumia wanafunzi na walimu wa Kiswahili katika shule za upili kama kiwakilishi cha jamii ya leo.

## 2.4 Misingi ya Kinadharia

a) Kazi ya fasihi inajitosheleza. Tamthilia ni kazi ya sanaa kwa vile ina msuko, mtindo, wahusika na ujumbe. Mhimili huu ulisaidia kuonyesha kuwa tamthilia teule ni kazi ambazo zinajitosheleza kama kazi ya fasihi. Hii ni kwa sababu zina sura, ploti, maudhui, wahusika na zinatumia mitindo ya kisanii. Kwa msingi huu tamthilia teule zinajitosheleza kwa vile zina maudhui halisi na wazi katika jamii ya leo. Kupitia kwa msuko, mtindo, wahusika na ujumbe wa tamthilia hizi ni bayana kwamba kazi hizi zinajitosheleza na zinafaa katika jamii ya karne ya ishirini na moja.

b) Kazi ya fasihi inapaswa kuwasilisha ukweli kama ulivyo katika mazingira yake. Uhalisia sharti ujihusishe na mambo halisi yanayotokea katika mazingira halisi kupitia kwa wahusika. Mhimili huu ulisaidia katika uchanganuzi wa masuala

ibuka katika tamthilia za kisasa na halisi katika jamii.Tamthilia teule ziliongozwa na msingi kwa vile zina maudhui halisi na wazi katika jamii ya leo. Kupitia kwa wahusika na ujumbe wa tamthilia hizi ni bayana kwamba kazi hizi zinajitosheleza na zinafaa katika jamii ya karne ya ishirini na moja kwa sababu zinawakilisha ukweli kama ulivyo katika jamii ya leo.

c) Wahusika ni vielelezo yakini vya binadamu wa kawaida kwa vile wao hutumia lugha ya binadamu wa kawaida. Hali halisi ya wahusika na lugha wanayoitumia humwezesha mwanadamu kujifafanulia uwezo wake wa kutenda mambo na mtazamo wake kuhusu maisha. Mhimili huu ulitumiwa kuonyesha kuwa wahusika wa tamthilia teule wanaathiriwa na mambo ya kila siku katika jamii.Mhimili huu ulisaidia kuelewa uhalisia wa maudhui katika jamii. Katika kusoma na kuchambua maudhui ya tamthilia teule, wahusika kama vile kiongozi Majoka na Mstahiki Meya na vibaraka wao katika uongozi wao wapo pia katika jamii ya leo.

   Viongozi wabinafsi na fisadi katika mfumo wa uongozi katika karne ya ishirini na moja. Wahusika maskini wanaotawaliwa kiimla na viongozi wabaya kama vile mama Dadavuo Kaole katika *Mstahiki Meya (2009)* na Tunu katika *Kigogo (2016)* vile vile wapo katika jamii ya leo. Kwa msingi huu basi wahusika wa tamthilia teule ni kielelezo cha binadamu halisi katika jamii.

d) Msanii anaangalia matatizo na kuchunguza chanzo chake. Anachunguza mabadiliko ambayo hutokea kwa kipindi fulani cha historia na kuyatumia kuwasawiri wahusika wake. Mhimili huu ulitumiwa kuonyesha kuwa matatizo wanayoyapitia wahusika wa tamthilia teule yana chanzo chake haswa kutokana na mazingira yanayomzunguka katika jamii yake. Kutokana na uchambuzi wa maudhui katika tamthilia teule na kuyaoanisha na maudhui halisi katika jamii ni wazi kwamba wasanii wa tamthilia za *Mstahiki Meya* (Arege, 2009) na *Kigogo* (Kea, 2016*)* wamechunguza chanzo cha matatizo ya jamii kupitia wahusika na maudhui katika kazi zao.

Kutokana na maoni ya wahojiwa wanajamii ndio chanzo kikuu cha matatizo yao haswa kwa kuwachangua viongozi wabaya na kwa upande mwingine viongozi ni adui

wa binadamu wenzao ambao ni wanajamii wanaotawaliwa kwa pindi wanapoingia mamlakani wanawasahau na kutawaliwa na ubinafsi.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.0 Utangulizi

Sehemu hii inahusu muundo wa utafiti ambao ulifuatwa. Hii ni pamoja na maelezo kuhusu eneo la utafiti; idadi lengwa na uteuzi wa sampuli; ufafanuzi wa njia za ukusanyaji data; mbinu za uchanganuzi pamoja na uwasilishaji wa matokeo.

## 3.1 Muundo wa Utafiti

Mtafiti alikusanya data nyanjani kwa kutumia hojaji kwa walimu na wanafunzi wa shule za upili; kata ndogo ya Nzambani kaunti ya Kitui.Muundo wa kimaelezo ulitumika kutokana na usomaji na uhakiki wa vitabu na machapisho mbalimbali, zikiwemo tamthilia zilizoteuliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti, maswali ya utafiti na nadharia ya uhalisia. Mtafiti alisoma na kubaini maudhui kaitka tamthilia teule. Baada ya kusoma mtafiti alichambua maudhui na kubaini maudhui ambayo yanapatikana katika tamthilia zote mbili. Mtafiti aliyaandika maudhui yale kama data ya utafiti akitoa mifano mwafaka ili kusisitiza ukweli kuwa maudhui ya waandishi tofauti na nyakati tofauti ni sawa. Uchanganuzi wa madhui kwenye tamthilia ulikuwa wa kimaelezo tu kuonyesha ukruba wa maudhui kwenye tamthilia teule kwa kuhakiki na kutathimini maudhui makuu ili kubaini uhalisia wake katika jamii hasa katika kipindi cha utahini wa tamthilia za *Mstahiki Meya* (Arege, 2009) na *Kigogo* (Kea, 2016). Ilikupata maudhui ya kijamii mtafiti alikusanya data kutoka kwa vyombo vya

habari kama vile magazeti, kusoma majarida na ripoti za serikali na makundi yasiyo ya kiserikali. Mtafiti pia alipata data kwa kutumia hojaji walimu na wanafunzi wa kidato cha tatu na nne kama kiwakilishi cha jamii ilikubaini uhalisi wa maudhui katika jamii kama yanavyowasilishwa katika kazi za tamthilia.Hii ilimwezesha mtafiti kuchanganua na kufasiri data iliyokusanywa na kufikia malengo ya utafiti.

## 3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti ulifanywa nyanjani katika shule za upili za kata ndogo ya Nzambani kaunti ya Kitui, Kenya.Ukusanyaji data ulifanywa kwa kutumia hojaji zilizojazwa na walimu nawanafunzi katika kidato cha tatu na nne. Eneo hili lilichaguliwa kwa sababu baadhi ya shule za upili hapa ni za mseto na kutwa na hii ingesaidia kupata hali halisi ya jamii kwa kutafitia jinsia zote katika kundi ambalo linatangamana na jamii kila siku. Utafiti pia ulifanywa mtandaoni ili kupata maoni zaidi ya waandishi na watafiti wengine. Mtafiti pia alipata data kutoka kwenye vyombo vya habari kama vile magazeti, ripoti na majaridakuhusu uhalisia wa maudhui katika jamii.

## 3.3 Sampuli Lengwa

Tamthilia mbili zilizoteuliwa ni *Mstahiki Meya* (Arege, 2009) na *Kigogo* (Kea, 2016*)* tamthilia ambazo ni za karne ya ishirini na moja na zimetahiniwa karibuni kati ya mwaka wa 2013-2014 *Mstahiki Meya* (Arege, 2009) na2018- 2021*Kigogo* (Kea, 2016). Utafiti pia ulilenga wanafunzi na walimu wa shule za upili, kidato cha tatu na nneambao waliwakilisha jamii kwani ndio wanaofunzwa na kutahiniwa kuhusu tamthilia. Mtafiti alitumia hojaji kupata data yiliyohitajika kutimiza malengo ya utafiti.

***Jedwali 3.1:Wahojiwa***

| **Shule** | **Wanafunzi** | **Walimu** |
|---|---:|---:|
| Shule ya mseto ya Kyanika | 10 | 2 |
| Shule ya mseto ya Kilonzo | 10 | 4 |
| Shule ya mseto ya Kaluva | 10 | 2 |
| Shule ya mseto ya Kavia | 10 | 5 |
| Shule ya mseto ya Utwiini | 10 | 2 |

| | | |
|---|---|---|
| Shule ya mseto ya Kivumbuni | 10 | 2 |
| Shule ya mseto ya Thua | 10 | 1 |
| Shule ya mseto ya Kanduti | 10 | 2 |
| Shule ya wavulana ya Nzambani | 10 | 2 |
| Shule ya wasichana ya Chuluni | 10 | 1 |
| **JUMLA** | **100** | **23** |

Mtafiti alilenga sampuli ya walimu na wanafunzi wa shule za upili kwa vile kidato cha nne na tatu hufunzwa na kutahiniwa maswala ya tamthilia. Mtafiti alitumia wanafunzi mia katika utafiti wake; wanafuzi watano katika kidato cha tatu na watano katika kidato cha nne jumla ya wanafunzi kumi kila shule kwa shule kumi. Sababu ya kutumia sampuli ya wanafuzi kumi ni kuwa shule nyingi hazikutaka zoezi hili livurunge ratiba ya shule, kwa malengo ya utafiti sampuli ya wanafunzi mia ilifaa kutoa data iliyohitajika kukamilisha utafiti. Walimu ishirini na watatu waliotumika walichaguliwa kwa vile wanafunza kidato cha tatu na nne hivyo walisaidia kukamilisha malengo ya utafiti. Walimu pia walisaidia kulinganisha maudhui ya tamthilia kwani wao wamesoma na kufunza tamthilia ya *Mstahiki Meya* (2009) tofauti na wanafunzi ambao wamesoma tamthilia ya *Kigogo* (2016)tu.Eneo la Nzambani lilichaguliwa kwa vile shule nyingi hapa ni za mseto na kutwa hivyo lengo la kulinganisha maudhui ya tamthilia na maudhui ya kijamii lilitimika kwa ufasaha kwasababu wanafunzi na walimu wanatangamana na jamii mara nyingi. Shule za mseto pia zili saidia kupata maoni ya jinsia tofauti ili kupata picha halisi ya jamii.

## 3.4 Uteuzi wa Sampuli

Kulingana na Bryman (2004),uteuzi wa sampuli ni mchakato wa kuchagua kikundi cha vitu ama watu ili kutumika kama kiwakilishi cha kundi zima linalotafitiwa kwa kuwa ni vigumu kutafitia kundi zima. Hata hivyo uteuzi wa sampuli hutegemea zaidi lengo la mtafiti na habari anazohitaji kuibua (Kothari, 1990). Kwa mantiki hii, sampuli kusudio ndiyo iliteuliwa kwa kutumia mbinu ya kimaksudi kutokana na malengo mahususi ya utafiti. Mtafiti alishughulikia tamthilia za karne ya ishirini na moja mbili pekee *Mstahiki Meya* (Arege, 2009) na *Kigogo* (Kea, 2016*)* tamthilia ambazo zimetahiniwa karibuni kati ya mwaka wa 2013-2017 *Mstahiki Meya* (Arege,

2009) na2018- 2021*Kigogo* (Kea, 2016). Utafiti pia ulilenga wanafunzi na walimu wa shule za upili kidato cha tatu na nne katika kata ndogo ya Nzambani kaunti ya Kitui ambao waliwakilisha jamii.

## 3.5 Ukusanyaji wa Data

Kulingana na Seale (2012) kuna mbinu mbalimbali ambazo mtafiti huweza kutumia ili kukusanya data ya utafiti. Hata hivyo anakiri kuwa hakuna mojawapo ya mbinu hizi ambayo imejitosheleza. Aidha, mbinu hizi hutegemea data anayokusanya mtafiti. Hii ina maana kwamba ukusanyaji data huongozwa na lengo la mtafiti. Utafiti huu ulitumia mbinu ya usomaji maktabani ili kupata data ya kimsingi. Ili kufikia lengo la utafiti huu, mtafiti alisoma na kuhakiki tamthilia mbili zilizoteuliwa. Data pia ilipatikana kwa kusoma vitabu, majarida na machapisho ambayo yanahusiana na malengo ya utafiti ili kupata data ya maudhui halisi katika jamii.. Hojaji kwa walimu na wanafunzi katika shule za upili kwenye kata ndogo ya Nzambani kaunti ya Kitui zilitumiwa kupata data kuhusu ufaafu wa maudhui yanayoendelezwa na tamthilia za *Mstahiki Meya* (Arege, 2009) na *Kigogo* (Kea, 2016).

## 3.6 Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa data uliathiriwa na mbinu za ukusanyaji zilizotumika kupata data husika. Utafiti huu ulitegemea zaidi data iliyokusanywa kutoka kwa usomaji wa maktabani na hojaji kwa walimu na wanafunzi katika shule za upili kwenye kata ndogo ya Nzambani kaunti ya Kitui. Mtafiti alisoma na kubaini maudhui kaitka tamthilia teule. Baada ya kusoma mtafiti alichambua maudhui na kubaini maudhui ambayo yanapatikana katika tamthilia zote mbili. Mtafiti aliyaandika maudhui yale kama data ya utafiti akitoa mifano mwafaka ili kusisitiza ukweli kuwa maudhui ya waandishi tofauti na nyakati tofauti ni sawa. Uchanganuzi wa madhui kwenye tamthilia ulikuwa wa kimaelezo tu kuonyesha ukruba wa maudhui kwenye tamthilia teule kwa kuhakiki na kutathimini maudhui makuu ili kubaini uhalisia wake katika jamii hasa katika kipindi cha utahini wa tamthilia za *Mstahiki Meya* (Arege, 2009) na *Kigogo* (Kea, 2016). Ilikupata maudhui ya kijamii mtafiti alikusanya data kutoka kwa vyombo vya habari kama vile magazeti, kusoma majarida na ripoti za serikali na makundi yasiyo ya kiserikali. Mtafiti pia alipata data kutoka kwa hojaji za walimu na

wanafunzi wa kidato cha tatu na nne kuwakilisha cha jamii ilikubaini uhalisi wa maudhui katika jamii kama yanavyowasilishwa katika kazi za tamthilia.Data kutoka kwa majibu ya walimu na wanafunzi iliwasilishwa kisayansi kwa kutumia njia ya uchanganuzi ya *OriginPro*. Data hiyo iliwasilishwa katika jedwali kupata idadi ya waliotoa jibu la ndio au la kutegemea swali. Idadi ya waliojibu ndio au la zaidi iliwasilishwa katika mchoro wa kisayansi ili kupata picha kamili.

## 3.7 Maadili katika Utafiti

Ili kukidhi na kuzingatia maadili na sheria za utafiti wa nyanjani, mtafiti baada ya kutetea pendekezo lake la utafiti mwezi wa April 2018, alipata barua ikimruhusu kwenda nyanjani kukusanya data. Mtafiti akitumia barua hii alienda kwa kila shule ambazo alikuwa amesampulisha na kuelezea ofisi kuu madhumuni ya utafiti na kuomba aruhusiwe kuonana na walimu wa lugha kidato cha tatu na cha nne katika shule hizo. Mtafiti alieleza walimu dhima ya utafiti wake, na akawapa fomu za kukubali kushiriki katika utafiti wakatia sahihi. Walimu walisaidia kuteua sampuli ya wanafunzi watano katika kidato cha tatu na watano kidato cha nne. Walimu walitumia matokeo ya mjarabu kupata sampuli hii kwa kuteua wawili waliokuwa wamefanya vizuri mmoja wastani na wawili wa mwisho kwa vidoto vyote viwili. Mtafiti aliweza kukutana na sampuli teule ya walimu na wanafunzi, akawapa hojaji na kueleza umuhimu wa utafiti. Mtafiti aliwahakikishia kwamba majibu na maoni yao yatabaki kuwa siri. Baada ya sampuli yake kujaza hojaji mtafiti alizikusanya na kuanza shughuli ya uchanganuzi.

# SURA YA NNE

# MAUDHUI MAKUU KATIKA TAMTHILIA TEULE

## 4.0 Utangulizi

Sura hii ilishughulikia maudhui makuu katika tamthilia teule *Mstahiki Meya* (Arege, 2009) na *Kigogo* (Kea, 2016).Utafiti pia ulichunguza maswala ibuka katika jamii na kuyalinganisha na maudhui makuu katika tamthilia teule ili kubaini uhalisia wake katika jamii.Data iliyokusanywa kutoka kwa hojaji za walimu na wanafunzi wa shule za upili kidato cha tatu na nne katika kata ndogo ya Nzambani Kaunti ya Kitui ilichanganuliwa kisanyasi na kuwasilishwa katika michoro ya kisayansi.

## 4.1 Maudhui Makuu katika Mstahiki Meya (2009)

Sehemu hii imechanganua maudhui makuu katika *Mstahiki Meya* ambayo ni pamoja na Uongozi mnya, umaskini, tamaa na ubinafsi, ufisadi, ukoloni mamboleo, ukiukaji wa haki, miongoni mwa mengine.

### 4.1.1 Maudhui ya Uongozi Mbaya

Maudhui ya uongozi mbaya yanajitokeza kwa namna ifuatayo katika tamthilia; Katika zahanati tunapatana na daktari Siki ambaye ni mwenye wahaka. Wasiwasi ni kutokana na ukosefu wa dawa zahanatini ila wagonjwa ni wengi wanaotaka huduma. Meya amesema wagonjwa waambiwe wasubiri kwani dawa zipo bandarini kuu na zitafika baada ya siku tatu. Siki anashangaa ni vipi ambavyo ugonjwa utaweza kusubiri. Siki anapokerwa na hali mbaya ya maisha anamwendea Meya kumuonya lakini anashikilia kwamba uongozi wake umefanya ya kutosha na kwamba Cheneo ni kisiwa cha kuigwa. Anasema kuwa waliomchagua ni hao watu:

*Meya: …Mara ya ngapi hii kunichagua? ….Tatu. Hata nikitaka nne, tano na sita bado watanipa… (Uk 12)*

Meya anatumia uongozi wake vibaya kuwashawishi wanajamii. Anaamrisha kinara wa uhusiano mwema na mawasiliano kwamba idhaa ya baraza icheze nyimbo za uzalendo kabla na baada ya vipindi maarufu.

Anakosa maadili ya kuaminika kama kiongozi pale anapofisidi wanacheneo ambao wamemchagua. Kwa vile yuko mamlakani, wanawe wanasomea ng'ambo kwa vile elimu ya cheneo ni ya kina yakhe, mkewe atajifungulia ng'ambo kuliko na wakunga wenyewe na pia mtoto apate uraia wa huko. Ili kufadhili elimu ya wanawena kujifungulia ng'ambo kwa mkewe Meya amenyakua vipande nane vya ardhi ya wanacheneo na kuuza vitatu na kumgawia rafikiye Bili vinne *(Uk 27).* Anatumia mamlaka yake vibaya. Mali ya cheneo inatumika kujiburudisha yeye na familia ya Bili katika hoteli ya Kajifahari kwa kutumia *entertainment vote ya Meya (27).*

Kutofanya uamzi wa kibinafsi kama kiongozi ni ishara ya kiongozi mbaya. Yeye na Bili wanapanga njama la kulifisidi baraza kupitia kwa mwanakadarasi. Anafuata ushauri potovu wa Bili kwamba wamwachie mwanakadarasi aende kortini kwa vile mkataba wake ulikatizwa kabla ya muda wa makubaliano. Na kwa vile korti itaamrisha alipwe fidia, Baraza ndilo litalipa kisha yeye akubaliane na mwanakadarasi fungu atakalompa*(uk 29)*

Meya anatumia askari wa baraza kuwatawanya wafanyikazi waliogoma. Vile vile anatumia vitisho kwamba atawafuta kazi na kuwaajiri vijana ambao hawana ajira. Kiongozi huyu anatumia mbinu hasi za uongozi na kushindwa kulidhibiti jiji.Kutokana na migomo ya kila mara, mji wa cheo umejaa uchafu; safari ya wageni imekatizwa kwa sababu wafanyikazi wa uwanja wa ndege wameungana na wengine katika mgomo hivyo hakuna wa kuelekeza rubani ili ndege itue.

#### 4.1.1.1 Umaskini na Hali Duni ya Maisha

Kutokana na uongozi mbaya umaskini ni vazi la kila mwanajamii Cheneo. Zahanatini wagonjwa wanakosa hela za kulipia huduma wanazotaka. Wengine hata hawana karatasi za kunakilia udodosi wao. Kutokana usemi wa Siki nchi ya Cheneo imeshatangazwa kuwa maskini kupitia vyombo vya habari, wanasiasa na hata wasomi.

Siki: *Aliyesema nchi hii maskini nani? …waridi: Nasikia tu! si vyombo vya habari si wanasiasa si wasomi.* (uk 3)

Mama Dadavuo Kaole anadhihirisha umaskini; mwanawe anaugua kutokana na kula chakula cha mbwa wa Meya: Wali na maharage yaliyolala hawakuweza kukitokosa kwani bei ya makaa na mafuta imepanda. Dadavuo Kaole ana tatizo la utapiamlo kwani hapati lishe bora kwa sababu ya umaskini. Umaskini umeduwaza mamake kwani kwake kumlisha mwanawe chakula cha mbwa wa Meya ni kawaida.

*Mama: …siku nyingi tunakula kile kinachopimiwa mbwa wa bwana tusipata dhara hata moja. Nashangaa leo hiki chaleta taabu… (uk 10 )*

Siki anapomtembelea Meya kwake nyumbani, anamfahamisha kuwa hali ya maisha ya wananchi ni duni.

*Siki…Hali yao ya maisha ni ngumu. Wanashindwa kumudu gharama za matibabu na dawa zenyewe hazipo zahanatini. Gharama za maisha zinazidi kupanda…watu wetu wana shida. Wengine wanakufa kwa njaa kwa sababu hawawezi kumudu mahitaji ya kimsingi… (UK10)*

Matamshi ya siki yamejaa uchungu. Anawakilisha jamii maskini na anaelewa hatari iliyopo Lakini kwa Meya ambaye ni kiongozi mpuuzi anapuuza anayoambiwa na kuendelea kujigamba.

*Meya…Ni baraza lipi lenye udhabiti kama letu ambalo linaongozwa na mstahiki Meya sosi?...Wewe tu ndiye huoni tuliyofanya na tunayoendelea kufanya…Huoni kuwa cheneo ni kisiwa cha kupigiwa mfano?... (UK 11).*

Ijapokuwa Siki anaendelea kushikilia msimamo wake kuwa watu wana njaa, watu wanakufa kwa kula mzizi na matunda mwitu, wanakufa kwa kukosa matibabu Meya anaendelea kupuuza, hali hii kwa madai kwamba yeye kama kiongozi amefanya ya kutosha.

### 4.1.1.2 Tamaa na Ubinafsi

Onyesho la pili la tamthilia linaonyesha hali na maisha tofauti ya kijamii. Maelezo ya nyumbani kwa Meya; makochi ya kupendeza, sakafuni kuna zulia lenye ruwaza za kupendeza, Vile vile kuna vyakula vya kila aina mezani. Picha tofauti na ile ya

maskini mama Dadavuo Kaole anayemlisha mwanawe chakula cha mbwa ambacho hakijatokoswa kwa vile bei ya makaa na mafuta ni ghali.

Hali hii inaonyesha ubinafsi wa kiongozi Meya. Anakula na kusaza huku waliomchagua wakifa njaa. Analalamikia udogo wa mayai. Kwa ulafi analibwakia yai moja ambalo linamnyonga, chai nayo inamchoma lakini hajilaumu yeye kwa tabia za ulafi ila lawama ni kwa maskini Gedi.

Anamtetesha Gedi kwa kumruhusu muuza mayai kuuza viyai vidogo na kuamrisha asionekane kwake na viyai vyake. Meya anaonyesha tamaa ya uongozi, amekuwa kiongozi mara tatu, anasema anaweza kuchanguliwa hadi mara ya sita

*Meya: Huna habari kuwa walinichagua hao hao watu... nataka uone mwenyewe kuwa ushawishi na udhabiti wa mambo ninao…Gedi mtumie habari mhazili mwangu amtafute kinara wa uhusiano mwema na mawasiliano mara moja amwambie mstahiki meya wa cheneo anataka idhaa za baraza kucheza nyimbo za uzalendo kabla na baada ya vipindi maarufu… (UK 12, 13)*

Hali hii ya Meya inaonyesha tamaa na ubinafsi wake wa kuongoza na ndio sababu anatumia mamlaka vibaya kuwashawishi wanacheneo kuwa uongozi wake ni bora kwa kuamrisha kuchezwa kwa nyimbo za uzalendo. Wengine waliochini yake wanaendeleza tamaa. Kwa mfano: Baraza la madiwani linaongozwa na tamaa. Diwani 1 anasema jukumu lao ni kutetea baraza la Mstahiki Meya kwani aliwachagua kuwa macho na masikio yake na kwamba wanalipwa kwa hili *(Uk 16)*

Meya anaamrisha nyongeza ya mishahara na marupurupu kwa madiwani na walinda usalama wakati shughuli za kikazi zimelemazwa na migomo ya wafanyakazi kwa sababu ya mishahara duni ya kutolipwa (*Uk 22)*. Zaidi ya kuongezewa mishahara na marupurupu, anawaondolea mzigo wa kulipa kodi.

### 4.1.2 Maudhui ya Ufisadi

Meya kwa uongozi wake mbaya anafisidi wanacheneo ambao wamemchagua. Kwa vile yuko mamlakani, wanawe wanasomea ng’ambo kwa vile elimu ya Cheneo ni ya kina yakhe, mkewe atajifungulia ng’ambo kuliko na wakunga wenyewe na pia mtoto

apate uraia wa huko. Ili kufadhili elimu ya wanawe na kujifungulia ng'ambo kwa mkewe Meya amenyakua vipande nane vya ardhi ya wanacheneo na kuuza vitatu. Kisha amemgawia rafikiye Bili vine *(UK 27).* Anatumia mamlaka yake vibaya. Mali ya cheneo inatumika kujiburudisha yeye na familia ya Bili katika hoteli ya Kajifahari kwa kutumia *entertainment vote ya Meya.*

Yeye na Bili wanapanga njama la kulifisidi baraza kupitia kwa mwanakadarasi. Anafuata ushauri potovu wa Bili kwamba wamwachie mwanakadarasi aende kortini kwa vile mkataba wake ulitatizwa kabla ya muda wa makubaliano. Na kwa vile korti itaamrisha alipwe fidia. Baraza ndilo litalipa kisha yeye akubaliane na mwanakadarasi fungu atakalompa. *(uk 29)*

Meya anaendelea kulifisidi Baraza kupitia kwa mhubiri. Baraza linalazimika kugharamia petroli ya mhubiri na kutoa sadaka ya laki moja kila mwezi kwa kile mhubiri analiombea baraza*(Uk 44).* Meya, Bili diwani wa 1 and II wanakubaliana kuiuza fimbo ya Meya ng'ambo na kudai kwamba ilipotea wakati wa maandamano *(Uk 61-62).*

### 4.1.3 Maandamano na Migomo ya Wafanyikazi

Kwa vile Meya ameshindwa kuudhibiti mji wa Cheneo shughuli za baraza zimelemazwa na wafanyikazi. Maandamano na migomo ya wafanyikazi ni wimbo wa kila siku. Wafanyikazi wanalilia maslahi bora, malipo bora, huduma za afya. Kutokana na sauti za wafanyikazi *(uk 30).* Meya amewapuuza na hajali maslahi yao. Kutokana na hali duni kazini muuguzi waridi anajiuzulu *(Uk 35-36)*. Analalamikia mshahara duni, watu kufia mikoni bila usaidizi.

Meya anatumia askari wa baraza kuwatawanya wafanyikazi waliogoma. Vile vile anatumia vitisho kwamba atawafuta kazi na kuwaajiri vijana ambao hawana ajira. Kutokana na migomo ya kila mara, Mji wa cheo umejaa uchafu; safari ya wageni imekatizwa kwa sababu wafanyikazi wa uwanja wa ndege wameungana na wengine katika mgomo hivyo hakuna wa kuelekeza rubani.

Wageni pia hawawezi kuja kwa kuhofia mkurupuko wa kipindupindu kutokana na maji chafu kwenye mahoteli yanayotekwa mitoni. Mhazili wa Meya pia anatoweka

maji yanapozidi unga. Gedi anamwarifu Meya kuwa mhazili hawezi kurudi kwani shughuli za usafiri zimelemazwa kwa vile wafanyikazi katika bohari la mafuta wagoma na vituo vya kuuzia mafuta havina mafuta tena *(UK 78).*

### 4.1.4 Maudhui ya Unafiki

Meya anatumia mbinu hasi za kuongoza. Kwanza anachagua Baraza la madiwani liwe macho na masikio yake. Baraza ambalo haliwezi kwenda kinyume.

*Diwani 1:*

*Jukumu letu ni kulitetea baraza…Mzee akatutunuku heshima ya kutuchagua sisi kuwa siyo tu macho yake bali pia masikio na sauti yake…* (*Uk 16)*

Huu ni unafiki kwani Meya anajipendekeza kwa madiwani na kuwapumbaza kwa kuwaongezea mishahara na marupurupu na zaidi kuamrisha wasitozwe kodi *(uk 22).* Meya anatumia vishawishi kubakia mamlakani, kwa mfano anaamrisha nyimbo za uzalendo kuchezwa redioni, anamwambia Bwana uhusiano mwema kuandaa tamasha za mashindano ya vijana kubuni, kutunga na kucheza nyimbo zao kisha kupata zawadi ndogo ndogo na kuonyeshwa kwenye vyombo vya habari *(Uk 20).*

Anawatisha wafanyikazi wanaogoma kwamba watafutwa kazi mara moja na kuwaajiri vijana kutoka vyuo vikuu ambao hawana ajira *(Uk 21).*Meya anaonyesha unafiki wakati wa maadalizi ya kuwapokea wageni wake. Mwenyewe anajua hali si hali hivyo atajaribu kuficha aibu kwa kuwapa maandilizi na mapokezi ya kupigiwa mfano.

*Meya: …Nitawapa mapokezi ya kupigiwa mfano. Hoteli ya kifahari. Mvinyo kutoka Urusi na divai kutoka Ufaransa…Wajue cheneo si mji hivi hivi….wajue kuwa ufadhili wao kwa baraza unadhaminiwa… (UK 25)*

Zaidi anamtumia mhubiri kuwapumbaza watu kuwa yeye ni mcha Mungu. Hii ni njia tu ya kuficha uovu wake. Meya anawatumia askari kuwafurusha wafanyikazi wanaogoma.

### 4.1.5 Uchafuzi wa Mazingira

Kutokana na uongozi wa kiimla wa Meya hali ya mazingira ni chafu. Watu hawapati lishe bora; wanakula kiporo cha Mbwa, mizizi na matunda mwitu. Zahanatini mazingira ya kazi si bora; wauguzi wanakosa vifaa vya kimsingi kama glavu za kufanyia kazi. Mji wa Cheneo umejaa uvundo na uchafu kwani wafanyikazi wamegoma *(Uk 50-51).* Kutokana na hali ya uchafu. Wageni wanasitisha safari yao kwa kuogopa kuwa huenda ugonjwa wa kipindupindu ukazuka.

*Diwani III: Wanaogopa mkurupuko wa kipindupindu maana mji mzima hauna maji safi…Mahoteli hayana maji yanayoweza kufikia viwango vya kimataifa…Mahoteli yananunua maji kutoka mtoni ambayo yanasombwa na Punda. (UK 77)*

### 4.1.6 Ukoloni Mamboleo

Ni bayana kwamba japo jamii ya Cheneo ilipata uhuru kutoka kwa wakoloni, bado uhuru kamili haujapatikana. Kiongozi wao Meya amesaliti uhuru wa wanacheno kupitia uogozi wake hasi. Uongozi wake wa kiimla ni namna ya ukoloni mamboleo. Kama kiongozi anatumia mamlaka yake kuwakandamiza wanacheneo. Anatumia mbinu za kikoloni kutawala kwa mfano; anatumia mbinu ya tenga utawale. Ameteua baraza la madiwani ambao ni macho na masikio yake. Anawaadaa kwa nyongeza ya mishahara na marupurupu ili waendelee kumuunga mkono wanaojaribu kumtenga kama diwani wa tatu wanamtenga.

Baraza la Cheneo bado linategemea ufadhili wa kigeni ili kujiendeleza kiuchumi. Meya anathamini elimu na matibabu ya ng’ambo. Anasema wanawe wanasomea ng’ambo kwenye elimu ya maana kwani elimu ya Cheneo ni duni. Anasema pia mkewe ameenda kujifungulia ng’ambo kwenye matibabu bora na pia ili mwanawe apate uraia wa huko. Meya anatumia pesa nyingi kuagiza vyakula na vileo kutoka urusi na ufaranza. Anadhamini bidhaa za ng’ambo kuliko za Cheneo *(UK 25).*

Maandamano na migomo ya wafanyikazi ni dalili za kikoloni. Wakati wa ukoloni wafanyikazi waligoma kulilia maslahi bora, malipo bora na huduma za afya. Meya amewapuuza na hajali maslahi yao. Kutokana na hali duni kazini muuguzi waridi

anajiuzulu *(Uk 35-36)*. Analalamikia mshahara duni, watu kufia mikononi bila usaidizi.

Kuwanyima wanacheneo haki na uhuru wa kuandamana ni mbinu ambayo ilitumiwa na wakoloni. Kiongozi Meya anatakaa kuwasikiliza wafanyikazi na kutumia askari kuwatawanya wanacheneo wanapoandamana.

### 4.1.7 Ukiukaji wa Haki za Kibinadamu

Wanacheneo wanakosa haki ya uongozi bora na wenye uwazi. Viongozi wao ni fisadi na wanafiki. Meya kiongozi mkuu anaendeleza uongozi mbaya. Matibabu bora ni haki yao lakini haipatikani. Kuna ukosefu wa dawa hospitalini hata wengine wanafia mikononi ya daktari kwa kukosa matibabu.

Wanacheneo wanakosa haki ya lishe bora. Jamii nzima inaishi kwa ukosefu wa chakula. Dadavuo kaole anaugua utapiamlo, anaugua kwa kula makombo ya mabaki ya chakula cha mbwa wa Meya. Wengine wanakufa kwa kula mizizi ya matunda mwitu. Wanacheneo, wananyimwa haki ya hali safi ya mazingira. Mji mzima una uvundo, hakuna maji safi hakuna vifaa vya kazi kuna hata tishio la mkurupuko wa kipindupindu.

Haki ya uhuru wa kuandamana inakiukwa. Meya anakataakuwasikiliza wafanyikazi. Anatumia askari kuwatawanya. Wanacheneo pia wanakosa ajira. Kuna vijana wengi ambao wamehitimu na hawana kazi. Meya anawatumia tu kipropaganda kujiendeleza kwa kuwashirikisha kwenye mashindano ya mziki na kuwazubaisha kwa kupeperusha mashindano hayo kwenye vifaa vya habari. Wale ambao wameajiriwa wanalipwa mishahara duni tena kwa kucheleweshwa.

Haki ya kisheria imekiukwa. Utaratibu wa kupeana kadarasi haufuatwi. Bili anamshauri Meya amwache mwanakadarasi aende kortini ashitaki ili alipwe fidiakisha ampe Meya mgao wake. Huu ni ufisadi na ukiukaji wa sheria za haki.

## 4.2 MAUDHUI MAKUU KATIKA TAMTHILIA YA *KIGOGO.*

Sehemu hii imechanganua maudhui makuu katika *Mstahiki Kigogo* ambayo ni pamoja na uogozi, umaskini, ukatili na udhalimu, unafiki na propaganda, ubadhirifu, uchafuzi

wa mazingira, tamaa na ubinafsi, ufisadi, ukiukaji wa haki za kibinadamu, ukoloni mamboleo na mengineo.

### 4.2.1 Uongozi Mbaya

Maisha ya jamii yoyote hutegemea hali yake ya kiuchumi. Mfumo mbaya wa uchumi ni chanzo cha maisha duni na mfumo thabiti hupunguza uzito wa hali ya maisha. Suala la uchumi ndilo linalojenga mgogoro mkuu katika tamthilia ya *Kigogo*. Mwandishi ametumia kufungwa kwa soko kama msingi wa migogoro yote katika jamii ya Sagamoyo. Kufungwa kwa soko la umma kunaashiria kuzimwa kwa tegemeo la kiuchumi la wanajamii.

Jamii ya Sagamoyo ina matabaka mawili makuu kwa msingi wa kiuchumi; walalahoi na walalaheri. Walalahoi ni maskini sana huku walalaheri ni matajiri wenye mali nyingi kupita kiasi. Tabaka la walalahoi linawakilishwa na familia ya kina Sudi. Licha ya jitihada za Susi na mkewe za kielimu, uongozi mbaya na ukosefu wa ajira huwafanya kuishi katika hali ya umaskini.

Suala hili linamfanya Sudi kutochagua kazi na kuambulia kazi ya uchongaji yenye mapato duni ya kubahatisha tu. Mke wake, Ashua, anauza maembe sokoni licha ya kuhitimu chuoni na shahada ya ualimu *(uk 25).* Kupitia kwa maisha yao, tunaona namna wananchi maskini wanavyojitahidi juu chini kutafuta riziki katika uchumi wa kibepari bila mafanikio.

Watawala wanajilimbikizia mali kwa njia za udanganyifu na kwa kuwakandamiza wananchi. Haya yanafanyika huku watawaliwa wakinyanyaswa kwa kutozwa kodi za juu kupita kiasi. Kwa mfano, Majoka analifunga soko la Chapakazi linalousaidia umma wa Sagamoyo na kupanga, kwa ushirikiano na Kenga, kunyakua ardhi yake ili ajenge hoteli ya kifahari ambayo inanuiwa kumfaidi yeye na familia yake *(uk 25*)

Kampuni ya Majoka ya kutengeneza sumu ya nyoka inawakandamiza wafanyikazi. Anapandisha bei ya vyakula maradufu kusudi watengeneze pesa zaidi kutoka kwao. Malalamishi ya wafanyakazi hayatiliwi maanani. Wanapigwa na kuuliwa kinyama. Viongozi wanatumia utajiri kuendeleza uozo wa kimaadili. Majoka ana mtazamo wa kibepari kwamba yeye ana kila kitu katika himaya yake isipokuwa Ashua kwa hivyo

anamshawishi Ashua amtaliki mumewe maskini ili amwoe *(uk 20)*. Majoka anawawakilisha viongozi wa Kiafrika ambao mizani yao ya maisha bora ni wingi wa mali na pesa wala sio utu.

Mwandishi ameuangazia pia uhusiano baina ya mataifa yenye matabaka mawili tofauti kiuchumi; wakopeshaji na wakopaji. Wakopeshaji ni mataifa ya magharibi na mashariki. Wanafadhili shughuli za utawala dhalimu. Yanayakopesha mataifa yanayoendelea madeni ili kuifanikisha miradi isiyo na manufaa kwa wananchi wa kawaida. Kwa mfano, yanafadhili mradi wa uchongaji wa vinyago vya mashujaa na kuipa Sagamoyo miaka mia moja kulipa deni hilo *(uk 11)*. Katika kipindi hicho cha miaka mia moja, Sagamoyo bado itakuwa ikitawaliwa na mataifa hayo kimawazo na kiuchumi. Wafadhili wanataka kujibandika katika kumbukumbu zao daima kiasi cha wanasagamoyo kutoweza kuyashughulikia masuala mengine ya kimandeleo.

Kuna ubadhirifu wa viongozi wa Sagamoyo. Wanapokea mikopo kutoka katika mataifa ya kigeni kisha wanazifuja kwa kugharimia sherehe zisizo za manufaa. Kwa mfano, Sagamoyo inatumia pesa kujiandaa kwa sherehe ya maadhimisho ya uhuru ilhali wananchi wa kawaida hawajaona manufaa yoyote ya uhuru huo. Mbali na hayo, wanafuja pesa zilizotengwa kusafisha soko.Tunatambua ufujaji huu wakati Kenga anapompasha Majoka habari kuhusu malalamishi ya Tunu kwa waandishi wa habari kwamba serikali ya Sagamoyo imezifuja pesa zilizotengewa usafishaji wa soko la Chapakazi *(uk 32).*

Uchumi wa Sagamoyo umezorota kiasi kwamba baadhi ya Wanasagamoyo wanatumia njia zozote kupata kadarasi za serikali. Asiya (Mamapima) anapata kadarasi ya kuoka keki za uhuru kwa kula uroda na Ngurumo *(uk 64*). Boza pia anajaribu kuwaficha mafundi wenzake kadarasi za uchongaji vinyago licha ya kuwa yeye hana uhodari wa kuchonga vinyago vya kuvutia kama Sudi.

Kuzorota kwa uchumi wa Sagamoyo kunamchochea Asiya (Mamapima) kutafuta riziki kwa njia haramu. Anavunja sheria na kukiuka matakwa ya katiba anapowauzia vijana pombe haramu. Bi Husda, anapata kibali cha kuuza pombe haramu kwa wananchi ili kustahimili hali ngumu ya uchumi wa Sagamoyo.

Mfumo mbaya wa uchumi unasababisha ukosefu wa ajira hata kwa watu waliosoma hadi katika viwango vya juu vya elimu. Tunu hana kazi na kutokana na hali yake, Kenga anamdhihaki kwa kumwambia Majoka kwamba shahada za siku hizi hazina manufaa *(uk 32).*

Mwandishi ana ujumbe kwa viongozi wa kiafrika kwamba wanafaa kuacha ubinafsi na wajitahidi kuyapa kipaumbele maslahi ya watawaliwa. Endapo wataendelea kuongozwa na ubinafsi basi utawala wao utaisha upesi kama moto wa mshumaa uishavyo *(uk 83).*

### 4.2.2 Maudhui ya Umaskini

Umaskini ni hali ya mtu au jamii kushindwa kuyakimu mahitaji yake ya kimsingi kama vile chakula, makazi na mavazi katika hali ya kawaida ya maisha. Umaskini umekithiri katika jamii ya tamthilia hii. Mwandishi ametuchorea taswira ya matapo mawili kwa msingi wa mapato yao; matajiri wanaozidi kujitajirisha kutokana na ufujaji wa pesa za umma na maskini wazidio kudidimia kimapato kwa kudhalilishwa na kukandamizwa na viongozi. Asilimia kubwa ya Wanasagamoyo ni maskini ingawa serikali inatumia fedha nyingi katika maandalizi ya sherehe za uhuru. Maudhui haya, yamejitokeza hasa katika familia ya Sudi.

Wafanyabiashara katika Soko la Sagamoyo ni watu wenye elimu na talanta kochokocho, kama vile Sudi, japo wangali wanaishi katika umaskini licha ya bidii zao. Soko la Chapakazi ni mahali pa biashara ya watu maskini. Mawazo haya ya Sudi yanaonyesha ukweli wa kuwepo kwa hali ya umaskini:

Sudi…*Mshauri Mkuu na binamuye Majoka amelitembelea soko la walalahoi, lo!.. (Uk9)*

Kauli hii hudhihirisha kwamba Sudi pamoja na Kombe, Boza na wote wafanyao kazi katika soko hilo chafu ni maskini hohehahe.

Boza anasema kuwa Sudi *ana kijirununu cha pesa nane*…*Maskini akipata*… (uk 7). Kupitia kwa Boza, tunafahamu kuwa Sudi ni maskini asiyeweza kununua simu ya thamani. Tunaona pia Sudi na mkewe wakimudu tu chai ya mkandaa ambayo ni

ishara ya umaskini. Watoto wao wachanga wanalala njaa na kukosa hata kiamshakinywa kutokana na umaskini.Soko linapofungwa, Ashua anamkimbilia Majoka kumwomba msaada kwa wanawe waliolala njaa. Majoka anamuuliza, *'Hivyo vichekechea vyenu viwili vimewashinda?'(uk 22).*

Wafanyakazi wa umma ni maskini wenye mishahara duni. Wauguzi na walimu wanafanya maandamano kushinikiza serikali iwaongeze mishahara. Hata hivyo, nyongeza ya mishahara ambayo wanapigania kupewa haitawanufaisha kwa sababu ni ndogo nayo serikali itapandisha kodi ili kuyapunguza na kujirudishia hayo mapato yao *(uk 36).* Walimu na wauguzi wataendelea kuishi wakiwa maskini.

Ingawa Bi Hashima anakuza mipunga kupata mazao ya matumizi ya nyumbani, yeye bado ni maskini ambaye anausikitikia ukame unaolikumba jimbo lao. Anadhihirisha wasiwasi wake kwa Siti kuhusu chakula watakachokula baada ya mchele aliovuna msimu uliopita kuisha. Wasiwasi wake unajitokeza katika maneno haya;

Bi Hashima:..*Kichele hiki tu, hata hakipikiki mkate wa sinia. Sijui tutakula nini tukingoja soko kufunguliwa…(uk 52).*

Ukame huu unawaathiri zaidi maskini ambao hawawezi kujichimbia visima. Matajiri wamechimba visima kwao *(uk 53).*Wafanyakazi katika kampuni inayomilikiwa na Majoka wanafanya maandamano kupinga kuongezwa kwa bei ya chakula katika kioski cha kampuni. Hii inadhihirisha kuwa hawawezi kumudu gharama ya chakula.

Bali na uongozi mbaya, uzembe wa baadhi ya Wanasagamoyo umechangia kuukuza umaskini. Kunao waliozama kwa ulevi Mangweni kwa Mamapima. Ulevi huathiri afya zao na kuwafanya wapoteze pesa na muda ambao wangeutumia kuyachuma mapato. Mtu yeyote mwenye afya iliyodhoofika hawezi kufanya kazi ipasavyo ili kuendeleza uchumi wa jimbo ama nchi.

Viongozi wa Sagamoyo wana tamaa ya kujiimarisha kiuchumi kwa hivyo hawajali kulitatua tatizo la umaskini miongoni mwa wananchi. Tunatambua hili kupitia kwa kauli ya Babu anaposema,

*Babu…kwa sababu ya tamaa mtu amependa kula kuku huku nduguze wakila kama kuku…* (*uk 84)*

Anamwonya Majoka dhidi ya kuishi maisha ya starehe matumbo ya watawaliwa yakinyukuliwa na njaa kutokana na umaskini.Mwandishi anatushauri kuvichunguza na kuvibaini fika vyanzo vya tatizo tulilo nalo la umaskini. Je, umaskini wetu hutokana na uzembe wetu ama ubadhirifu wa viongozi

### 4.2.3 Ukatili na Udhalimu

Ukatili na udhalimu ni kuwatendea watu matendo ya kinyama kwa kukosa huruma. Ukatili hutokea pale ambapo mtu au kundi la watu linawanyanyasa, kuwapiga na kuwaua wengine kwa sababu zao za kibinafsi. Ukatili umekithiri katika jamii hii ya Wanasagamoyo. Viongozi wanadhulumu wapinzani kama mbinu ya kuwanyamazisha na kuwatia wengine uoga.Viongozi hutumia vitisho na kuwanyang'anya wafanyabiashara mali zao. Haya yanadhihirika katika kauli ya Sudi anaposema kuwa

*Sudi… si haki kuchukua kilicho chetu na kututisha... (uk 3)*

Watu wanaoandamana wanauliwa. Vijana watano waliokuwa wakifanya mandamano ili kupanda kwa bei ya chakula katika kampuni ya Majoka wanauawa nao wachuuzi sokoni wanaumia *(uk 16).*

Viongozi wa upinzani wanaopinga utawala wa kiimla wa Majoka wanalemazwa kisiasa na hata kuuawa. Viongozi wanatumia mbinu za kisiri kuwaua washindani ili kuficha ukatili wao. Kwa mfano, Jabali, kiongozi wa upinzani ambaye alikuwa na chama chake cha Mwenge, aliuliwa katika ajali ya barabarani na chama cha Mwenge kusambaratishwa *(uk 35).*

Tunu anavamiwa na wahuni wanaomjeruhi muundi wa mguu. Nia ya wavamizi ilikuwa kumuua kwa vile Kenga anamfahamisha Majoka,

*Kenga Hawakumvunja mguu wa kitamathali. Tunu bado yuko!.. (uk 68).*

Uvamizi huu unaonyesha udhalimu wa viongozi kwa sababu wahuni waliomvamia walitumwa na viongozi wenyewe.Watu wanyonge ambao hawana hatia wanapigwa na

kutiwa mbaroni hasa wanawake ambao wanakataa kujihusisha kimwili na viongozi. Kwa mfano, Ashua licha ya hayo anatiwa mbaroni na kupigwa bila kosa.

Watu wanaishi kwa hofu kutokana na uvamizi wa mara kwa mara. Kwa mfano, Hashima na Siti hawana utulivu kwa sababu ya hali mbaya ya usalama jimboni.Ni wazi kuwa viongozi katika jamii hii wanatumia ukatili na udhalimu kuwatia hofu na kuwanyamazisha wapinzani wanaothubutu kufunua na kupinga udhalimu wao.

### 4.2.4 Unafiki na Propaganda

Unafiki ni hali ya mtu kujifanya mwema kwa lengo la kuyaficha maovu. Propaganda kwa upande mwingine ni kueneza habari za uongo kwa nia ya kuwadanganya watu na kutimiza malengo fulani ya hila. Viongozi wanatumia unafiki kuyaficha maovu yao. Mambo wanayoyatenda ni kinyume na wanayosema.

Majoka anasema kuwa Wanasagamoyo wasiruhusu watu wachache waliojazwa na kasumba za kikoloni kuwarejesha katika utumwa. Pia, anadai kuwa hawawezi kukubalikutawaliwa kidhalimu tena ilhali yeye anayatenda mambo yayo hayo anayoyakashifu. Anawadhulumu kutoka mashariki na magharibi.Wimbo wa uhuru unatumiwa kumsifu Majoka. Unammiminia sifa kiongozi ambaye anawakandamiza wananchi. Kupitia kwa wimbo huo, Majoka na familia yake inajitia sifa bandia ili wazidi kupendwa nao umaarufu wao uenee zaidi.

Soko linafungwa ili kina Sudi wakose riziki kisha walazimishwe kuyatimiza matakwa ya viongozi. Njaa inamsukuma Ashua kwa Majoka akienda kutafuta msaada. Majoka anamwita mkewe ofisini ili itokee rabsha. Baadaye, Ashua anatiwa ndani ili kumlazimisha Sudi achonge kinyago.

Viongozi wanapanga kuongeza mishahara ya walimu na wauguzi kisha wapandishe kodi ndipo pesa hizo ziwarejee walimu na madaktari wasinufaike na nyongeza ya mshahara. Naye Kenga anasema kuwa hiyo ni mbinu ya kutia kwa kushoto na kutoa kwa kulia *(uk 36).* Hii ni mbinu ya watawala ya kuhakikisha kuwa wanapata sifa nzuri kwa kuongeza mshahara na wakati huo watumishi wa umma wanazidi kuwa maskini kwa kulimbikizwa kodi ili wawe mbioni kujitafutia riziki na wasiyatilie maanani maovu yanayotendeka.

Utawala unajaribu kutumia hila kuwatenganisha Tunu na Sudi ili kudhoofisha upinzani. Kwanza, Majoka anapendekeza Tunu aolewe na Ngao Junior. Tunu anapokataa, anamshauri aachane na Sudi kwa sababu wana ajenda mbili tofauti. Anamwambia amtafute mume amwoe. Mbinu hiyo inapokosa kufaulu, anatuma wahuni kumuua Tunu lakini wanamvunja tu mguu. Wahuni hao wanaeneza propaganda kwa kusema kuwa Sudi na Ashua ndio wanaowinda roho ya Tunu ili atengane na Sudi (*uk 54).*

Baada ya kifo cha Ngurumo, Majoka anapendekeza kuuliwa kwa chatu moja kama njia ya kuwafanya watu wasitilie maanani kifo cha Ngurumo, badala yake wafanye maandamano wakilalamikia kuuliwa kwa Chatu. Kwa njia hiyo, kamera zote zitaelekezwa kwa waandamanaji ili watu wasione namna makaburi yalivyojaa.

Viongozi wanakopa pesa kutoka kwa wafadhili kukidhi miradi inayowafaa ama wanayokubali wafadhili ambao wanaunga serikali mkono. Hata hivyo, wanapanga njama ya kuwafukuza wafadhili ambao wanapinga utawala wa kiimla kwa kuwafadhili wapinzani wanaozipigania haki za wengi. Wanadai kuwa wanajiweza wenyewe huko Sagamoyo *(uk 33).* Nia yao ni kuzisambaratisha shughuli za wapinzani.

Viongozi wanatumia vyombo vya dola kama vile televisheni na askari kueneza propaganda. Kwa kuwa wameshindwa kutekeleza majukumu yao, inawabidi kutumia mbinu za udanganyifu ili kuonekana wema mbele ya umma na kuficha maovu yao.

Wana mazoea ya kuwasafirisha wafuasi kwa mabasi kuhudhuria mikutano yao. Kenga anajua kuwa iwapo wangejua kwamba watu hawatahudhuria mkutano wao, wangekodisha mabasi kuwasafirisha vijana na kina mama kuja kuuhudhuria. Hii ni mbinu ya kuwapumbaza wananchi kwamba viongozi wao bado wana umaarufu wakati ambapo ni dhahiri kwamba watu hawawapendi tena.

### 4.2.5 Ubadhirifu

Ubadhirifu ni kutumia mali kwa fujo. Utawala wa Majoka unafuja rasilimali za umma. Viongozi wanatumia pesa na rasilimali za umma kwa manufaa ya kibinafsi. Kwa pesa zilizotengewa usafishaji wa soko zinafujwa na Majoka.Serikali inakopa

pesa nyingi na kuziwekeza katika miradi isiyofaa wananchi. Pesa zinakopeshwa kutoka katika mataifa ya kigeni na kutumiwa katika mradi wa kuchonga vinyago badala ya miradi ya maana kwa wananchi kawaida.

Serikali imeshindwa kuwalipa watumishi wa umma mshahara bora kama vile walimu na wauguzi. Hata hivyo, serikali hiyo hiyo inaahidi kutumia pesa nyingi kuwatuza watakaochonga vinyago visivyokuwa na manufaa kwa wananchi. Sudi anaahidiwa kupelekwa likizo ya ughaibuni pamoja na familia yake ikiwa atakubali kuchonga kinyago cha Marara bin Ngao *(uk 11).*

Kiongozi ambaye anastahili kuangamiza umaskini ndiye anayefunga soko ambalo ndilo tegemeo la pekee la Wanasagamoyo kwa madai kuwa uchafu uliopo sokoni utaharibu sifa ya Jimbo la Sagamoyo. Punde tu soko linapofungwa, serikali hiyo hiyo inalifuga soko na kubomoa vibanda ili kujenga hoteli ya kifahari *(uk 25).*Ardhi ya sokoni inagawiwa washiriki wa karibu wa Majoka. Majoka anamwambia Kenga,

*Majoka: Si unajua kipande chako sokoni tayari kimetengwa? (uk 69).*

Serikali inashiriki katika biashara ya kukata na kuuza miti badala ya kutunza mazingira. Ukataji wa miti unasababisha ukame. Wakulima kama Hashima wanapata mavuno duni nayo mito inakauka.Badala ya kuchimba mabwawa ya maji ya kufaidi wananchi wote, viongozi wanajichimbia visima katika maboma yao huku wananchi wakikosa maji baada ya mito na maziwa kukauka.Hoja hizi ni dhihirisho tosha kuwa sera za viongozi wanalenga kujilimbikizia mali huku wananchi wakididimia katika umaskini.

### 4.2.6 Uchafuzi wa Mazingira

Mazingira ni eneo au hali inayomzunguka mtu au kiumbe.Mwandishi ameyashughulikia maudhui haya kwa kumulika hali ya uchafu wa maeneo mbalimbali katika jimbo la Sagamoyo, namna viongozi wanavyoyapuuza mazingira, madhara ya mazingira machafu kwa wanasagamoyo na harakati za baadhi ya wanasagamoyo za kutunza mazingira.

Licha ya wanasagamoyo kupandishiwa kodi, soko la Chapakazi limechafuka kupita kiasi. Mitaro inayapitisha maji machafu ambayo yamechanganyika na kemikali *(uk 2).* Hali hii imesababishwa na mambo kadhaa. Kwanza; viongozi wanauacha uchafu kujaa sokoni kisha wanalifunga soko kwa lengo la kunyakua ardhi yake ili kujijengea hoteli ya kifahari *(uk 25)*

Uchafuzi wa mazingira pia umetokana na ufujaji wa pesa za umma. Viongozi wa Sagamoyo wamefuja pesa hadi hawawezi kusafisha soko. Kenga anamwambia Majoka kwamba Tunu analalamika kuhusu ufujaji huo *(uk 32).*

Uchafuzi na uharibifu wa mazingira umewasababishia Wanasagamoyo magonjwa mbalimbali. Kombe anapolalamikia hali hii, Sudi anachangia kwa kusema, *'Ndiyo maana watu wanamenyana na ndwele zisizo majina hapa.*' *(uk 2).* Wanasagamoyo wanaishi tu kwa Mwenyezi Mungu.

Maji machafu ya mtaro yanafudikiza harufu mbaya inayowachafua roho na kuwakirihi wenyeji. Boza anatematema mate kazini kwa sababu ya harufu hiyo licha ya kuwa yeye mwenyewe haungami ukweli huo. Kenga pia anashindwa kuvumilia uvundo maana anatoa kitambaa mfukoni na kuitemea mate. Tendo hilo la Kenga linadhihirisha unafiki wa viongozi kwani anajifanya kuwa anajali usafi wa mazingira na eti hawezi kuyatema mate ovyoovyo ilhali wenyewe ndio walioutelekeza wajibu wao wa kulisafisha soko.

Hatua ya Majoka ya kuwaruhusu watu kukata miti ovyo ovyo inachangia uharibifu wa mazingira ambao unaishia kuleta ukame Sagamoyo *(uk 53).* Ukataji miti umesababisha ukosefu hadi wakulima hodari kama Hashima wanashindwa kuelewa kile watakachokula baada ya kuishiwa na mavuno machache waliyoyapata katika msimu uliopita. Wanakisia kwamba hata maji ya kunywa yatapotea hadi wayaagizwe kutoka ng'ambo, jambo ambalo litawawia walalahoi wa Sagamoyo muhali kulimudu.

Harakati za kuhifadhi mazingira zinadhihirika wakati Sudi anamwambia Boza kwamba viongozi wanafaa kusafisha mazingira.Tunu pia anawahutubia wanahabari akimshutumu Majoka kwa kufunja pesa zilizotengewa usafishaji wa soko. Mwandishi anawahimiza viongozi kuwajibika katika jukumu la kutunza mazingira. Tendo lao la

kuharibu mazingira ni hatari kwani limewaathiri sana wakazi wa Sagamoyo. Wamekumbwa na maradhi mengi na bado wanakisia kwamba watakuwa na ukame utakaowafanya kuagiza hata maji kutoka ng'ambo.

### 4.2.7 Tamaa na Ubinafsi

Tamaa ni hali ya mtu kutaka kitu sana kiasi cha kuwa radhi kutumia njia yoyote ili kukipata. Tamaa huweza kuwa mbaya au nzuri. Mwandishi amezishughulikia aina hizi mbili za tamaa katika tamthilia ya *Kigogo.*Tamaa nzuri hudhihirika miongoni mwa watu kadhaa. Kwamfano, Tunu ana tamaa ya kuleta mabadiliko ya kijamii katika jimbo la Sagamoyo. Anawatetea wachuuzi ili wafunguliwe soko kwa kuyafikisha malalamiko yao kwa Majoka.

Viongozi wa Sagamoyo wana tamaa mbaya. Majoka ana tamaa ya kusalia uongozini ili aendelee kuwadhulumu wananchi. Anamuua Jabali, mpinzani wake kisiasa na kuwatuma kina Ngurumo kumpiga Tunu ili asipate mpinzani wa kisiasa.Majoka ana tamaa ya kimapenzi. Ijapokuwa ana mke, anamtamani Ashua. Hata mwenyewe anakiri hivyo anaposema,

*(uk 76)*

*Majoka: 'Kusema nampenda ni kudanganya, ni zaidi ya kumpenda, naweza kumfia.'*

Tamaa humchochea Majoka kujaribu kumshawishi Ashua amtaliki mumewe lakini hafanikiwi.Majoka na Kenga wana tamaa ya mali. Badala ya kuwahudumia raia, wanawafungia soko na kupanga kunyakua ardhi ya umma ili waijenge hoteli ya kifahari sokoni (*uk 69).* Kenga anaahidiwa kupata kipande cha ardhi sokoni naye anafurahia jambo hilo. Tamaa ya mali pia inasababisha viongozi kuwatoza watawaliwa kodi kupita kiasi bila kuwahudumia ipasavyo.Walimu na madaktari wanapogoma, viongozi wanawapumbaza kwa nyongeza kidogo ya mshahara kisha wanapandisha kodi.Mwandishi amewaonya viongozi kwamba uongozi hauwezi kudumu kwa tamaa bali kwa kujali masilahi ya wananchi. Ukweli wa kauli hii unadhibitika Tunu anapowaambia Wanasagamoyo kwamba wanafaa kumchagua kiongozi anayewafahamu na kuwajibika kazini si wenye ubinafsi kama Majoka *(uk 90).*Wanasagamoyo wanaitikia ombi la Tunu kwa shangwe na nderemo, kuonyesha

kuwa wameshazinduka na wapo tayari kuondoa viongozi waovu mamlakani kuonyesha kuwa wanatamani viongozi bora.

### 4.2.8 Maudhui ya Ufisadi

Ufisadi ni matumizi mabaya ya mamlaka kwa kujifaidi au kuwafaidi wengine. Kuna visa kadhaa vinavyodhihirisha kwamba Majoka na wafuasi wake ni mafisadi wanaostahili kuhukumiwa kisheria.

Wafanyabiashara wanatozwa kodi ya kiwango cha juu kupita kiasi. Kombe anamweleza Boza,

*Kombe: 'Kodi tunayolipa si kodi tu…ni kodi na kitu juu yake.' ( uk 3)*

Isitoshe, hata baada ya wao kutozwa kodi ya kiasi hicho, soko lao halisafishwi. Hatimaye, linafungwa kwa kisingizio kwamba lina uchafu unaoliharibia Jimbo la Sagamoyo sifa *(Uk 25*). Ukweli wa mambo ni kuwa pesa za kulisafisha soko zimefujwa jinsi inavyobainika wakati Kenga anapoeleza madai ya Tunu kwa vyombo vya habari (*uk 32).*

Majoka ananuia kujenga hoteli ya kifahari katika ardhi ya soko kama anavyomweleza Ashua *(uk 25).* Vibanda vinabomolewa sokoni ili mradi huo wa ujenzi uweze kufanikiwa na hata Kenga apate kipande chake cha ardhi huko huko sokoni *(uk 69).*Kwa hivyo ni wazi kwamba kina Majoka wameinyakua ardhi hiyo ya umma ili kujinufaisha wao wenyewe.

Majoka amekopa pesa kutoka nchi za magharibi na mshariki ambazo zitalipwa kwa miaka mia moja ijayo. Pesa hizo haziwekezwi kwa miradi ya manufaa kwa umma bali zinanuiwa kufadhili uchongaji vinyago vya Marara bin Ngao, Ngao mwenyewe na mashujaa wengine. Anachofanya Majoka ni kutumia pesa za mkopo ambazo ni pesa za umma kuendeleza miradi ambayo iwapo ina manufaa basi ni kwake mwenyewe, yaani kuwalimbikizia babuye na babaye sifa kochokocho.

Kandarasi zaserikali hazipatikani kwa wazi. Inambidi mtu awe anamjua mtu mwingine serikalini ama amhonge mwenye ushawishi ndipo azipate. Asiya anatumia

mwili wake kumhonga Ngurumo aliye na ushawishi kumwezesha kupata kadarasi ya kuoka keki. Pia, huenda aliipata kwa sababu yeye ni mkoi wa Husda, mke wa Majoka ambaye ni kiongozi wa Sagamoyo.

Majoka anawaruhusu wafuasi wake kuvunja sheria. Asiya amepewa kibali cha kuuza pombe haramu ingawa kufanya hivyo ni kinyume na sheria imekithiri jimboni hadi ikawavimbisha baadhi ya watawaliwa kichwa kiasi cha kujipiga kifua wakisema kwamba katiba na serikali ni mambo mawili tofauti, yaani mtu halazimiki kufuata sheria mradi yuko upande wa serikali. Mbali na hayo, wafuasi wa Majoka wameruhusiwa kukata miti ovyo ovyo na kuiuza kwa manufaa ya kibinafsi *(uk 53).*

Majoka hajali madhara ya uharibifu wa mazingira. Labda biashara hii ya miti inamnufaisha kwa njia fiche.Yawezekana kwamba Majoka anashiriki wizi wa kura. Anapoona kwamba watu wamempuuza na wanamuunga mkono Tunu, anawaambia:

*Majoka: 'Pigieni huyo Tunu wenu kura tuone, hata msiponipa kura moja nitashinda!' (uk 91).*

### 4.2.9 Ukiukaji wa Haki za Binadamu

Mwandishi ameyashughulikia maudhui haya kwa kuchora matapo mawili katika jamii ya Sagamoyo. Kuna tapo la wanaofuata sheria na wasiofuata sheria. Kwa mfano, Mamapima anapewa kibali cha kuuza pombe haramu na Majoka licha ya madhara chungu nzima ya pombe hiyo kwa wananchi. Pombe hiyo imewaua watu wengi Sagamoyo na kuwapofusha wengi mno.

Wapo wanaohimiza kufuatwa kwa katiba na wasiofuata sheria zilizoko kwenye katiba. Tunu hapendezwi na hatua ya Majoka ya kumpa Mamapima kibali cha kuuza pombe haramu. Siti na Hashima pia wanakerwa na uamuzi wa Majoka wa kuwaruhusu watu kukata miti ovyoovyo. Kwa upande mwingine, Ngurumo anafurahia kuwa Mamapima amepata kibali kinyume na sheria (*uk 61).*

Kenga anamshauri Majoka kutumia uwezo wake kuharamisha maandamano na kuwaamuru maafisa wa polisi watumie nguvu katika kuwatawanya

waandamanaji.Majoka anajaribu kumfuta kazi Kingi bila kufuata utaratibu uliowekwa katika katiba.

Utelekezaji wa majukumu hutokea viongozi wanapotenda mambo kinyume na matarajio. Hivyo, wao huisaliti imani ya wapiga kura. Viongozi wa Sagamoyo wanakiuka haki za binadamu kwa kutotekeleza majukumu na kuwasaliti Wanasagamoyo. Kwa mfano, wamewasaliti wapiga kura kwa kuyapuuza majukumu yao. Soko linanuka uvundo kutokana na uchafu na majitaka ilhali viongozi wanajishasha tu kukusanya kodi bila kujali kulisafisha.

Badala ya kupiga vita pombe haramu, serikali inatoa kibali kwa wauzaji wa pombe kinyume na sheria. Mamapima anauza pombe haramu inayowapofusha na kuwaua watu na kudai kuwa ana kibali kutoka kwa serikali *(uk 61).* Pombe hiyo inaishia kuwapofusha wengi na hata kuwaua wengine.

Serikali inakiuka katiba. Ngurumo anamwambia Tunu*, 'Huku ni Sagamoyo, naomba kukukumbusha kuwa serikali na katiba ni mambo mawili tofauti kabisa!'(uk 61)*

Badala ya kulinda usalama, polisi wanatumiwa kuwatawanya na kuwapiga watu wanaofanya maandamano ya amani. Askari kama vile Mwango wanawalinda na kusalimu amri za viongozi wachache vipofu badala ya kuuhudumia umma.Ni wazi kuwa mambo wanayoyatenda viongozi ni kinyume na matarajio ya umma. Wapiga kura waliowachagua viongozi wamesalitiwa hivyo viongozi wamekiuka haki za binadamu za uongozi bora.

## 4.3 MAUDHUI MAKUU KATIKA JAMII

Sehemu inachanganua maudhui halisi katika jamii ya leo mintarafu maudhui yaliyoshighulikiwa katika Mstahiki Meya na Kigogo kama yalivyoshughulikiwa katika sehemu iliyotangulia.

### 4.3.1 Maudhui ya Ukoloni Mamboleo

Kulingana na Colin(1975), Kenya iko katikati ya ukoloni mamboleo kuliko taifa lingine lile barani Afrika. Hii ni kwa sababu Kenya inatawaliwa na viongozi fisadi ambao wanaulemaza uchumi wa nchi na kuchangia umaskini wa jamii. Hii

inaonyesha ukoloni mamboleo kupitia kwa viongozi ambao wanaiga mtindo wa ukoloni na kuuendeleza katika jamii ambayo inastahili kuwa huru kimaendeleo.Wanajamii katika nchi ya Kenya wanahisi kwamba japo walipata uhuru bado wanaendelea kutawaliwa na wageni kiuchumi, kiakademia na kisiasa.

Mumbi(2014), alitafiti juu yaukoloni mamboleo katika elimu. Anatoa mifano katika uchapishaji wa vitabu na majarida kuhusu nchi ya Kenya ambayo waandishi wake wengi ni wa nchi za kigeni. Wakenya pia wanadhamini elimu ya kigeni kuliko ya kwao. Hali hii imeendelezwa kikamilifu kwenye tamthilia za utafiti. Kupitia kwa dhana hii ya kuwepo kwa ukoloni mamboleo katika elimu, tunakubali kuwepo kwa uhalisi wa maudhui katika jamii.

Nchi ya Kenya pia ilionyesha kuchangia ukoloni mamboleo kupitia uongozi wake wakati ilipanga mitakakati ya kuagiza mahindi kutoka Mexico, ili kupambana na hali ya kupanda kwa bei ya unga. Mnamo Disemba 2017, Kenya, kupitia kwa waziri wa kilimo, ilifikia mkataba na nchi ya Mexico kununua mahindi kwa bei nafuu.Ni ukweli wa kimsingi kuwa mataifa yanayoendelea yana tabia ya kutegemea vyakula na vinywaji kutoka ng'ambo. Hii imeendelezwa pia kwenye tamthilia ya *Mstahiki Meya* ambapo meya anaagiza vinywaji kutoka Urusi ili kuwafurahisha wageni. Uhalisi wa maudhui kupitia tamthilia na masuala ya kijamii unabainika wazi.

Nasibo (2019) anasema kuwa, kwa upande wa afya, nchi ya Kenya inaonyesha kudhamini huduma za kigeni pale ambapo inaajiri wahudumu kutoka Cuba. Kundi la kwanza la madaktari wa Cuba lilifika nchini mwaka 2018. Mwaka 2019 serikali ilipanga kuongeza madaktari zaidi kutoka Cuba.

Kulingana na takwimu za Benki Kuu ya Kenya (Central Bank of Kenya, 2018), nchi ya Kenya inadaiwa zaidi ya trilioni tano kutoka kwa mataifa ya kigeni, ishara kwamba Kenya inaendelea kutawaliwa na mataifa ya kigeni kiuchumi. Kulingana na takwimu, nchi ilikuwa imekopa trilioni 5.1 kwa muda wa miaka mitano. Makopo wa Eurobond wa shilingi bilioni 210 umesabisha madeni ya taifa kupanda. Deni hili ni mzigo kwa wanajamii na kila mmoja atalipa zaidi ya shilingi 117,000.

Maundu (2017), alitafitia ukoloni mamboleo nchini Kenya kupitia kilimo cha kahawa kwenye kazi yake. Ukoloni mamboleo katika kilimo cha kahawa Kenya unadhirika kupitia kwenye bei yake katika soko ya kimataifa inayopelekea uzalishaji wa chini wa kahawa.Utafitihuu umeonyesha kwamba kilimo cha kahawa nchini kimeadhirika pakubwa kutokana na ushidani mkubwa kwenye soko ya kimataifa kutoka kwa mataifa kama vile Brazil na Vietnam ambayo yanapita ufadhili mkubwa kutoka kwa benki kuu ya dunia. Kuadhirika kwa uzalizaji wa kahawa nchini Kenya kumechangiwa pakubwa na benki kuu ya dunia na ni hali wazi ya kuwepo kwa ukoloni mamboleo katika nchi ambayo inastahili kuwa huru kuamua mikakati yake ya kilimo bora.

### 4.3.2 Maudhui ya Uongozi Mbaya

Shirika la the Society for International Development (SID) (2012), katikaripoti yakeya *ABaseline Survey 2012,* inatoa maelezo kuhusu matatizo ya uogozi nchini Kenya. Ripoti hii inahusisha matokeo ya utafiti uliofanywa na mashirika ya Uraia Trust, UN-Women, Amkeni Wakenya na Society for International Development kuhusu maridhiano na kusamehana baada ya vita vya baada ya uchaguzi 2007-2008. Wakenya walikuwa na maoni tofauti kuhusu waliohusika katika vita hivi asilimia na 35 walisema hatawasamehe washukiwa walisababisha vita hivi lakini watakubali matokeo na maamzi ya koti ya jinai,19.5% walisema watasamehe baada ya fidia na kuhukumiwa kwa washukiwa, 9.5% walisema hawatawasamehe kabisa.Kutokana na data ya majibu yaliyokusanywa ni bayana kwamba nchi hii inaishi na chuki ambayo ilisababishwa na tamaa ya uongozi iliyopelekea kukiukwa kwa haki za binadamu na kupelekea dhuluma na muuaji wa wakenya wasio na hatia. Zaidi matokeo ya utafiti yalionyesha kwamba viongozi wa nchi ya Kenya wanakwamisha shughuli ya maridhiano nchi kwa matamshi yao ya chuki na kuunga mkopo makundi ya kikabila. Hii inaonyesha wazi kuwepo kwa uongozi hasi, miongoni mwa viongozi ambao wanapaswa kuchangia kuunganisha jamii.

Baadhi ya viongozi nchini Kenya wamekashifiwa kwa uongozi wao mbaya kupitia ukosefu wa uongozi bora kwenye mashirika na kampuni za kiserekali. Omosa (2014) katika utafiti wake ameonyesha kuwa viongozi wa serikali wamekosa kuongoza

kampuni hizi na hivyo viongozi wa kampuni kuvunja pesa na kulegea kazini. Utafiti pia umeonyesha utepetevu wa serikali kwa kukosa kuhakikisha kwa sheria na mapendekezo ya bunge yametizwa mara moja baada ya kupitishwa.

### 4.3.3 Kupanda kwa Gharama ya Maisha

Maudhui ya kupanda kwa gharama ya maisha yamejadiliwa na tamthilia zote mbili. *Mstahiki Meya (2009)* kwa mfano: Mwandishi Arege anaonyesha vile hali ya maisha imepanda na wanacheneo wanazidi kutozwa ushuru hata mama muuza mboga. Wananchi wanashindwa kumudu hali ghali ya maisha. Hali hii pia inajitokeza katika tamthilia ya *Kigogo (2016).* Wananchi wanatozwa kodi na hali ya maisha ni ghali mno.

Kulingana na Njoroge (2019), gharama ya maisha imepanda zaidi mwaka wa 2019, kipita kiwango cha asilimia sita kwa kipindi cha miezi kumi na tisa. Bidhaa za chakula zimepanda kwa asilimia nane kutoka asilimia sita nukta themanini na sita ya mwaka jana. Bei ya vinywaji na vyakula ndiyo imepanda zaidi kwa asilimia 36.04 na kupelekea gharama ya juu ya maisha.

Kulingana na Samuel (2017) serikali inalaumiwa juu ya kupanda kwa gharama ya maisha na kuionya dhidi ya ufisadi na mikopo kutoka kwa mataifa ya kigeni. Hali hii ya kupanda kwa gharama ya maisha inatokana na ufisadi ambapo serikali hupoteza kiwango kikubwa cha pesa kila mwaka kupitia ufisadi (1/3= 608 milioni) kiwango hiki kikubwa cha ufisadi kimelemaza kukua kwa uchumi wa nchi na hivyo serikali inategemea mikopo kukopo na ufadhili wa kigeni ambayo hatimaye ni mzigo kwa walipa ushuru hivyo hali ya maisha hupanda kupitia kupandishwa kwa bidhaa za kimsingi ili kulipa madeni.

Kulingana na ripoti ya Benki Kuu ya Kenya ya 2018 (Central Bank of Kenya 2018), kutokana na hali ngumu ya maisha, serikali imeongeza asilimia ya ulipaji wa ushuru kama ifuatavyo.

***Jedwali 4.1: Kupanda kwa Gharama ya Maisha***

| BIDHAA | ASILIMIA |
|---|---|
| Mafuta | 8% |
| Ada za kupiga simu | Kutoka 10% hadi 20% |
| Huduma za kutuma pesa kwa simu na benki | 20% |
| Wafanyikazi wote | 1.5% ya mishahara yao |
| Pesa za ushindi wa Kamari | 15% |

Kulingana na ripoti hiyo, kulikuwa na hofu ya Kenya kushindwa kulipa deni la mikopo kutoka nje. Hii ni tishio kwa ukuaji wa uchumi wa nchi kwani mapato yake yatatumika kulipia madeni.

Kulingana na ripoti ya *Corruption Perceptions Index 2017* (Transparency International 2018), Kenya iliorodheshwa nambari 143 kati ya jumla 180katika viwango vya ufisadi duaniani. Sakata nyingi za ufisadi na matumizi mabaya ya pesa za umma yamechangia kupanda kwa gharama ya maisha na kulemaza uchumi wa nchi. Nchi inatumia pesa nyingi kuliko mapato yake kulipa madeni jambo ambalo linamuumiza mtoa ushuru.

Hali ya kupanda kwa gharama ya maisha inaangaziwa na waandishi Timothy Arege na Pauline Kea katika kazi zao. Kwa mfano, katika *Mstahiki Meya* Siki analalamika kuwa hali yao ya maisha ni ngumu. Wanashindwa kumudu gharama za matibabu na dawa zenyewe hazipo zahanatini. Gharama za maisha zinazidi kupanda, watu wetu wana shida na wengine wanakufa njaa kwa sababu hawawezi kumudu mahitaji ya kimsingi. Katika kigogo hali si tofauti Sudi na mkewe wakimudu tu chai ya mkandaa ambayo ni ishara ya umaskini wanashindwa hata kuwalisha wao wawili. Watoto wao wachanga wanalala njaa na kukosa hata kiamshakinywa kutokana na umaskini.Soko linapofungwa, Ashua anamkimbilia Majoka kumwomba msaada kwa wanawe waliolala njaa. Majoka anamuuliza, 'Hivyo vichekechea vyenu viwili vimewashinda?'(uk 22). Kulingana na UNICEF (2018) aslimia arobaini na sita ya wakenya ni maskini. Ripoti ya Benki kuu ya Kenya (Central Bank of Kenya, 2018), asilimia kubwa ya wakenya haiwezi kupata bidhaa za kimsingi.

### 4.3.4 Unyakuzi na Matumizi Mabaya ya Mali ya Umma

Kulingana na Wily (2018), hata baada ya ukoloni ya ukoloni, haijakuwepo sheria kuhakikisha kuwa milki ya ardhi ya wanajamii imehalalishwa. Kwa vile jamii nyingi Kenya zinaishi katika ardhi ambayo haijamilikiwa kisheria, mzozo juu ya ardhi baina ya wanajamii imekuwa tatizo sugu. Kutokuwepo kwa sheria inayofafanua vizuri ardhi ya jamii Kenya kumesababisha mzozo wa ardhi kupitia unyakuzi haswa kwa jamii za mifugo. Walio mamlakani na wanaoelewa katiba ndio wananyakua ardhi za umma kwa sababu pia wao wanadai kuwa wanajamii na sharia haija baini idadi ambayo inastahili kuishi katika ardhi ya jamii.

Viongozi wa Kenya wanaendeleza unyakuzi wa mali ya umma. Kulingana na ripoti ya tume ya kupambana na maadili na tume ya kitaifa ya ardhi 2018, eneo la Kibarani Mombasa lilikuwa limenyakuliwa na watu wasiojulikana. Maudhui haya yanaendelzwa na kiongozi Mstahiki Meya pale anaponyakua vipande nane vya ardhi kwa manufaa ya kibinafsi.

### 4.3.5 Tamaa na Ubinafsi

Tamthilia za *Mstahiki Meya* na *Kigogo* zimeendeleza maudhui ya tamaa na ubinafsi. Hali hii ni wazi nchini Kenya. Kulingana na ripoti ya shirika la Transparency International 2018, wabunge wa Kenya walionyesha hali ya tamaa na ubinafsi kwa kutaka nyongeza ya mishahara, nyumba za bure na bima ya juu ya afya. Pendekezo hili lilikuwa kinyume na sheria na ni mzigo kwa walipa ushuru.

Njoroge (2017) alisema kuwa tamaa na ubinafsi miongoni mwa wakurungezi wakuu wa makampuni umewafanya kukosa Imani kutoka kwa watu. Hali hii ya tamaa na ubinafsi imewafanya wawekezaji wa kigeni uongopa kushiriki biashara na wakenya. Maduka makuu ya Nakummat na uchumi, benki ya Chase na kiwanda cha sukari cha Mumias ni mifano ya adhari za tamaa na ubinafsi uliopelekea kuporomoka kwake.

Otieno (2019) aliripoti tamaa na ubinafsi miongoni mwa wabunge kwa kujilipa marupurupu ya nyumba ya shilingi elfu 250.000 kwa kila mbunge na seneta. Wakenya walishangazwa na kuudhishwa na ubinafsi huu wa viongozi ambao

wanaelekea kutowajali wakenya ambao tayari wametwikwa mzigo mkuu wa kulipa ushuru na gharama ya juu ya maisha.

### 4.3.6 Ufisadi

Kulingana na ripoti ya EACC (2018), asilimia 63 ya wahojiwa katika ripoti ya*National Ethics and Corruption Survey, 2017,* walitafuta huduma za kiserikali mwakani, zaidi ya asilimia 38.9 walishuhudia ufisadi. Asilimia 27 walifisidiwa kwa uwazi, 9.8% kwa njia isiyo wazi na asimilia 2.1 walifanya ufisadi kwa hiari. Idadi hii ya takwimu za vitendo vya ufisadi, katika ofisi za umma ilikuwa imeongezeka sana hadi asilimia 62.2 kutoka asilimia 46 kulingana na ripoti ya mwaka wa 2016.

Shirika lisilo la kiserekali la Transparency International 2018; linafafanua ufisadi kama matumizi mabaya ya uongozi kwa manufaa ya kibinafsi. Kuna aina tatu za ufisadi mkuu haswa kwenye serikali, ufisadi wa viwango vya chini (ufisadi wa kisiasa). Aina hizo zote za ufisadi zipo nchini Kenya, kwa miongo nne iliyopita na zinaadhiri ustawi wa uchumi wa nchi ya Kenya.

Kimeu na Maina (2018) walionyesha hali ambapo wakenya uvurushwa kutoka kwa makaazi yao kwasababu ya ufisadi au ukuikaji wa haki za kibinadanu.Wakenya wanefurushwa na hata nyumba zao kubomolewa bila kujali haki zao. Kiini cha kufurushwa na kubomolewa kwa majumba ni ufusadi ambao umekithiri nchini.

Kulingana na ripoti ya Ethics and Anti-corruption Commission 2018, nchi ya Kenya hupoteza takriban shilingi bilioni 608 kwa ufisadi kila mwaka ambayo ni asilimia 78 ya ustawi wa nchi.Kulingana na ripoti ya Open Africa nchi ya Kenya ina historia mrefu ya ufisadi tangu kupatikana kwa uhuru kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali lifuatalo.

*Jedwali 4.2: Madai ya Ufisadi miaka 2009-2018*

| MWAKA | MADAI/KESI | KIWAGO |
|---|---|---|
| 2009 | Sakata ya mahidi kigeni | Kshs. 150.0 milioni |
| 2009 | Sakata ya mafuta ya Triton | Kshs. 7.6 bilioni |
| 2009 | Sakata ya ardhi ya makaburi ya Nairobi | Kshs. 160 milioni |
| 2010 | Sakata ya chickengate | Kshs. 50 milioni |
| 2010 | Sakata ya ardhi ya Ubalozi wa Japan | Kshs. 1.4 bilioni |
| 2013 | Sakata ya maduka ya KAA | Kshs. 11.0 bilioni |
| 2014 | Sakata ya Eurobond | Kshs. 215.0 bilioni |
| 2015 | Sakata ya NYS | Kshs. 791 milioni |
| 2015 | Sakata ya Benki ya chase | Kshs. 34 bilioni |
| 2015 | Sakata ya ardhi ya Karen | Kshs. 8.0 bilioni |
| 2015 | Sakata ya ununuzi wa rukwama Bugoma | Kshs. 1.0 milioni |
| 2016 | Sakata ya ufisadi kaunti ya Kilifi | Kshs. 2.0 bilioni |
| 2016 | Sakata ya wizara ya afya | Kshs. 5.0 bilioni |
| 2016 | Sakata ya NSSF | Kshs. 1.6 bilioni |
| 2016 | Sakata ya pesa kwa vijana | Kshs. 180 milioni |
| 2018 | Sakata ya NYS | Kshs. 9.0 bilioni |

| | | |
|---|---|---|
| 2018 | Sakata ya wizara ya afya | Kshs. 11.0 bilioni |
| 2018 | Sakata ya mahindi NCPB | Kshs. 1.9 bilioni |
| 2018 | Sakata ya ufisadi ya kawi nchini | Kshs. 470 milioni |

Katika tamthilia zote mbili ufisadi ni kati ya maudhui makuu. Mstahiki Meya kwa mfano anaendeleza ufisadi kupitia kwa matumizi mabaya ya mali ya umma. Majoka, pia katika *Kigogo* hali si tofauti.

### 4.3.7 Uchafuzi wa Mazingira

Hali ya uchafuzi wa mazingira na tishio la mkurupuko wa maradhi ni halisi nchini Kenya. Maudhui haya pia yamejadiliwa katika tamthilia za *Mstahiki Meya (2009)* na *Kigogo 2016*. Ripoti ya Shirika la Afya ulimwenguni 2007,iliibua adhari kubwa ya mazingira kwa afya ya binadamu. Ripoti hii ilionyesha vifo zaidi ya milioni 13 vinaweza kizuiwa kupitia uhifadhi wa mazingira. Zaidi ya asilimia thelathini ya magonjwa pia yanaweza kuzuiwa kupitia uhifafhi wa mazingira. Kulingana na shirika la afya ulimwenguni watu 19000 hufariki dunia kutokana na hewa chafu. Shirika la mazingira na umoja wa mataifa mji wa Nairobi una asilimia kumbwa ya uchafuzi wa mazingira. Hali hii inajitokeza katika tamthilia za *Mstahiki Meya* na *Kigogo.*

Utafiti wa Okebiro na wengine (2014), kuhusu uchafuzi wa mazingira Kenya katika miji kumi ambayo ni Lodwar, Kitale, Garissa, Kisumu, Nyeri, Nakuru, Mombasa, Nairobi, Narok na Kisii unaonyesha kwa kwamba wakenya hawapuuzi uhifadhi wa mazingira. Utafiti unaonyesha kwamba wakenya upuuza sharia za uhifadhi wa mazingira na hivyo kuyachafua. Uchafuzi wa mazingira Kenya unadhihirika kupitia kutapakazwa kwa makaratasi na vyupa vya plastiki bila kujali madhara yake. Wakenya kutofuata au kuvunja sheria ya uhifadhi wa mazingira kunaonyesha utepetevu wa serikali kuhakikisha sheria imefuatwa. Hiini hali ya uongozi mbaya unaopelekea uchafuzi wa mazingira.

Utafiti wa Omanga na wengine (2014), zaidi unaonyesha kuwepo kwa uchafuzi wa mazingira kutoka viwandani.wahojiwa hata hivyo walionyesha kutambua kuwepo kwa uchafuzi huu lakini hawahusishwi kutafuta suluhu kwa changamoto hii.

Kutokana na utafiti huu pia hakuna sharia mwafaka au she ria za uhifadhi wa mazingira nchini hazifuatwi.

### 4.3.8 Migomo na Maandamano

Munene (2014), ameangazia migomo ya wafanyikazi Kenya. Ametoa mfano wa mgamo wa walimu 2012. Mgomo huu uliteka makini ya mataifa ya kigeni kwa kuwa hata baada ya kutagazwa haramu na koti ya viwanda walimu waliendelea kugoma kwa mujibu wa katiba mpya 2010. Ambayo inawaruhusu wakenya kushiriki maadamano na mgomo. Katiba ya Kenya (2010), chini ya kipengee 41 juu ya mahusiano ya kazi) inamruhusu mkenya haki ya malipo bora, kujiunga na kundi la utetezi wa masilahi kazini na kushiriki migomo.

Baada ya mgomo wa walimu madaktari nao walifuatia kugoma kwenye hospitali za umma. Mogomo wao ulichukua wiki tatu baada ya mgomo serekali ilitishia kuwaadhibu walioshiriki mgomo. Mifano hii miwili ya migomo hili ilisaidia kulinganisha mifano ya migomo ambayo imeendelezwa na waandishi wa tamthilia za *Mstahiki Meya* (2009) na *Kigogo* (2016). Kupitia kwa mifano hii maudhui ya migomo na maadamano ni halisi katika jamii.

Maudhui haya yameshughulikiwa na waandishi Arege (2009) na Kea (2016). Migomo na maandamano ni maudhui makuu katika tamthlia hizi. Maudhui haya yanajitokeza kwa uhalisia mkubwa katika jamii ya Kenya. Migomo na maadamano ya wafanyikazi imekuwa ikishuhudiwa kila uchao nchini wafanyikazi kuandamana na kugoma kulalamikia kucheleweshwa kwa mishahara yao. Kulingana na *World report 2019* (Human Rights Watch,2019)kutochukuliwa hatua kwa madai ya ukiukaji wa haki za binadamu ni swala nyeti. Polisi nchini Kenya wanatumia nguvu kupita kiasi haswa wakati wa maandamano. Baada ya uchaguzi 2017-2018 polisi walitumia nguvu kupita kiasi kutawanya waandamanaji na hata kuuwa wengine kwa kuwapiga risasi. Waliwadhulumu wanawake kimapenzi na hata kuwabaka.

## 4.4 UCHANGANUZI WA DATA

### 4.4.1 Utangulizi

Sehemu hii ya utafiti ili changanua data iliyokusanywa nyanjani kutumia hojaji kwa walimu na wanafuzi wa shule za upili katika kata ndogo ya Nzambani kaunti ya kitui.Sampuli na eneo la utafiti zilichanguliwa kwa vile wanafunzi wa shule za upili haswa kidato cha tatu na cha nne wanafunzwa na kutahiniwa katika tamthilia. Eneo hili lina shule nyingi za mseto hivyo maoni ya jinsia zote yalipatikana.Walimu walisaidia kulinganisha maudhui katika tamthilia kwani wao wana tajriba ya kufunza.

Maudhui makuu katika tamthilia teule na kisha kuyalinganisha na maudhui makuu katika jamii, utafiti ulikusanya data kwa kujazwa kwa hojaji na kuichanganua kisanyansi kwa kutumia *OriginPro.*

### 4.4.2 Uchanganuzi wa Hojaji za Wanafunzi

Data katika kiwango hiki imechanganuliwa kwa kurejelea migao ifuatayo: kidato cha mtafitiwa, jinsia, uelewa wa maudhui, manufaa ya maudhui na tofauti za kimaudhui.

#### 4.4.2.1 Kigezo Kidato cha Mtafitiwa


Hojaji za wanafunzi zililenga wanafunzi wa kidato cha nne na tatu katika shule za upili katika kata ndogo ya Nzambani kwa lengo la kutathimini maudhui katika tamthilia. Wanafunzi mia moja walihojiwa kama ifuatavyo kwenye jedwali. Kigezo hiki cha kidato cha mtafitiwa kilitumiwa kwa sababu kazi za tamthilia zinaaza kufundishwa katika kidato cha tatu na kutahiwa katika kidado cha nne. Mtafiti alilenga kubaini uelewa wa maudhui kutegemea kidato. Idadi ya wahojiwa katika kigezo hiki cha kidato cha watafitiwa imewasilishwa katika jedwali lifuatalo.

*Jedwali 4.3: Kidato cha Mtafitiwa*

| **Shule** | **Kidato cha Tatu** | **Kidato cha Nne** |
|---|---:|---:|
| Shule ya mseto ya Kyanika | 05 | 05 |
| Shule ya mseto ya Kilonzo | 05 | 05 |
| Shule ya mseto ya Kaluva | 05 | 05 |
| Shule ya mseto ya Kavia | 05 | 05 |
| Shule ya mseto ya Utwiini | 05 | 05 |
| Shule ya mseto ya Kivumbuni | 05 | 05 |
| Shule ya mseto ya Thua | 05 | 05 |
| Shule ya mseto ya Kanduti | 05 | 05 |
| Shule ya wavulana ya Nzambani | 05 | 05 |
| Shule ya wasichana ya Chuluni | 05 | 05 |
| **JUMLA** | **50** | **50** |

Kwa jumla wanafunzi hamsini walihojiwa katika kidato cha tatu na wanafunzi hamsini kutoka kidato cha nne. Lengo na sababu ya kuchagua kuhoji wanafunzi wa kidato cha nne na cha tatu ni kwa sababu wanafunzi hawa hupata mafunzo ya tamthilia teule kwa kina na hata kutahiniwa. Hivyo ilikuwa rahisi kwao kuelewa na kujibu maswali ya utafiti huu.

***Mchoro 1: Majibu ya Kidato cha Wanafunzi***




Kutokana na uwasilishaji wa jedwali la 4.2, visaduku vinavyowakilisha idadi ya wanafunzi vinaonyesha kuwa wanafuzi watano katika kidato cha tatu na cha nne walihojiwa.Jumla ya wanafunzi kumi kutoka kila shule hivyo wanafunzi mia moja kwa shule zote kumi. Idadi ya wanafunzi wa kutahiwa ilielekezwa na walimu wa shule zilizotumika.

### 4.4.2.2 Jinsia ya Mtafitiwa

Swali hili la hojaji lililenga kubaini jinsia za wanafunzi kwani baadhi ya shule kwenye kata ndogo hii ya Nzambani ni za mseto. Pili uelewa na utambuzi wa mambo hutofautiana kutegemea mambo kama jinsia. Kwa sababu hii basi hojaji iliongozwa na kigezo cha jinsia kubaini uelewa wa maudhui miongoni mwa wanafunzi tofauti

kwa misingi ya jinsia majibu yao yalikuwa kama ilivyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo.


***Jedwali 4.4: Matokeo ya Jinsia ya Mtafitiwa***

| **Shule** | **Jinsia ya Kike** | **Jinsia ya Kiume** |
|---|---|---|
| Shule ya mseto ya Kyanika | 5 | 5 |
| Shule ya mseto ya Kaluva | 5 | 5 |
| Shule ya mseto ya Kilonzo | 5 | 5 |
| Shule ya mseto ya Kavia | 5 | 5 |
| Shule ya mseto ya Utwiini | 5 | 5 |
| Shule ya mseto ya Kivumbuni | 5 | 5 |
| Shule ya mseto ya Thua | 5 | 5 |
| Shule ya mseto ya Kanduti | 5 | 5 |
| Shule ya wavulana ya Nzambani | 00 | 10 |
| Shule ya wasichana ya Chuluni | 10 | 00 |
| **JUMLA** | **50** | **50** |

Walimu walisaidia kusampulisha jinsia tofauti katika kidato cha tatu na cha nne ili kusaidia utafiti huu kupata maoni tofauti. Kwa kuhoji jinsia zote mtafiti aliweza kupata hali halisi ya uelewa wa maudhui kijinsia kwa kuzingatia usawa kwa jinsia katika jamii.

Idadi ya watafitiwa katika kategoria hii ya jinsia pia imewakilishwa kwa mchoro ufuataoo.

*Mchoro2: Matokeo Kuhusu Kigezo cha Jinsia ya Mtafitiwa*




Mchoro 2 unaonyesha jinsia tofauti za wanafunzi ambao walihojiwa ili kufanikisha utafiti huu.Rangi nyeusi inaonyesha idadi ya wasichana waliohojiwa kuwa hamsini na nyekundu inaonyesha kuwa wavulana hamsini pia walihojiwa. Kigezo cha jinsia kilisaidia kubaini uelewa wa maudhui miongoni mwa wanafunzi tofauti kwa misingi yakijinsia.

### 4.4.3 Kigezo cha Uelewa wa Maudhui

Kwenye swali hili wanafunzi alitoa jibu la ndio au la kisha kutoa ufafanuzi wa sababu zao. Ili kupata maoni tofauti mtafiti alitumia hojaji kwa kidato cha tatu na cha nne na majibu yalikuwa kama ifuatavyo. Umuhimu wa swali hili ulikuwa kuonyesha kuwa kiwango cha uelewa wa maudhui hutegemea kiwango cha elimu. Matokeo ya majibu ya wanafunzi wa kidato cha tatu waliohojiwa kuhusu uelewa wao wa maudhui katika tamthilia rejelewa yamewakilishwa katika jedwali lifuatalo.

*Jedwali 4.5: Kidato cha Tatu*

| **Shule** | **Jibu-Ndio** | **Jibu-La** |
|---|---|---|
| Shule ya mseto ya Kyanika | 2 | 3 |
| Shule ya mseto ya Kaluva | 1 | 4 |
| Shule ya mseto ya Kilonzo | 1 | 4 |
| Shule ya mseto ya Kavia | 0 | 5 |
| Shule ya mseto ya Utwiini | 1 | 4 |
| Shule ya mseto ya kivumbuni | 0 | 5 |
| Shule ya mseto yaThua | 3 | 2 |
| Shule ya mseto ya Kanduti | 2 | 3 |
| Shule ya wavulana ya Nzambani | 2 | 3 |
| Shule ya wasichana ya Chuluni | 4 | 1 |
| **JUMLA** | **16** | **34** |

Majibu ya wanafunzi thelathini na wanne katika kidato cha tatu walionyesha ugumu wa kutambua maudhui na kuyaelewa kwa urahisi wanapoanza kufunzwa katika kidato cha tatu. Wanafunzi kumi na sita tu ndio walioonyesha kwamba wanayaelewa maudhui kwa urahisi. Katika kidato cha tatu swali hilo lilijibiwa ifuatavyo na sampuli ya wanafunzi hamsini pia.Mfano wa majibu ya wanafunzi kidatao cha tatu;


Swali: Je, maudhui ya kazi za tamthilia za fasihi mnazosoma shuleni yanaeleweka kwa urahisi?

Ndio ☐

La ☐

Fafanua: maudhui ya kazi za fasihi ni vigumu kueleweka kwa sababu ndio mwanzo tunapatana nayo kwenye kazi za fasihi. Jibu la “ndio” au “la” limewasilishwa kisayansi kwenye mchoro3. ufuatao.

*Mchoro 3: Idadi ya Wanafunzi*




Kutokana na mchoro huu idadi kubwa ya wanafunzi katika kidato cha tatu walionyesha kutoyaelewa maudhui katika hatua za kwanza za utangulizi wa maudhui. Hata hivyo kuna wachache ambao wanaelekea kuyaelewa maudhui katika kidato hiki pengine kutokana na kiwango cha umilisi cha juu.

Matokeo ya majibu ya wanafunzi wa kidato cha nne waliohojiwa kuhusu uelewa wao wa maudhui katika tamthilia rejelewa yamewakilishwa katika jedwali lifuatalo.

*Jedwali 4.6: Kidato cha nne*

| **Shule** | **Jibu-Ndio** | **Jibu-La** |
|---|---|---|
| Shule ya mseto ya Kyanika | 4 | 1 |
| Shule ya mseto ya Kaluva | 5 | 0 |
| Shule ya mseto ya Kilonzo | 3 | 2 |
| Shule ya mseto ya Kavia | 3 | 2 |
| Shule ya mseto ya Utwiini | 4 | 1 |
| Shule ya mseto ya Kivumbuni | 3 | 2 |
| Shule ya mseto ya Thua | 2 | 3 |
| Shule ya mseto ya Kanduti | 4 | 1 |
| Shule ya wavulana ya Nzambani | 5 | 0 |
| Shule ya wasichana ya Chuluni | 5 | 0 |
| **JUMLA** | **38** | **12** |

Wanafunzi thelathini na nane walijibu kwamba hawana tatizo kuyaelewa maudhui katika kidato cha nne. Wanafuzi kumi na wawili walitoa sababu ya kuwa huwa wamesoma na kuzichambua kwa undani hivyo maudhui yanaweza kubainika wazi. Walisema pia kuwa wanafanya mitihani na mazoezi kuhusiana na maudhui katika tamthilia. Kutokana na majibu yao pia wengi walisema kwamba walimu wao huanza kufunza kazi za fasihi kwa tamthilia katika kidato cha tatu.

Hata hivyo kuna idadi ya wanafunzi kumi na sita ambao walisema wanapata changamoto kidogo hasa kuelezea maudhui na kutoa mifano mwafaka. Kulingana na maoni yangu majibu yaliyotolewa ni sawa kwani uelewa wa maudhui hutegemea umilisi wa wanafunzi, hivyo hatuwezi jumlisha kwamba wanafunzi wote watayaelewa maudhui kwa usawa. . Mfano wa majibu ya wanafunzi kidatao cha nne;


Swali: Je, maudhui ya kazi za tamthilia za fasihi mnazosoma shuleni yanaeleweka kwa urahisi?

Ndio ☐

La ☐

Fafanua: Maudhui ya kazi za fasihi ni rahisi kueleweka kwa sababu huwa tayari tumeyasoma kaitka kidato cha tatu.Jibu la “ndio” au “la’ limewasilishwa kisayansi kwenye mchoro4 ufuatao.

***Mchoro 4: Idadi ya Wanafunzi Kidato cha Nne***




Mchoro huu unaonyesha majibu ya wanafunzi wa kidato cha nne ya uelewa wa maudhui. Mstari rangi nyekundu unawakilisha wanafunzi tthelathini na nane wa kidato cha nne ambao hawana tatizo kuyaelewa maudhui kwasababu huwa

wameyasoma katika kidato cha tatu. Hata hivyo kuna idadi ya wanafunzi kumi na sita ambao walisema wanapata changamoto kidogo hasa kuelezea maudhui na kutoa mifano mwafaka. Majibu yaliyotolewa ni sawa kwani uelewa wa maudhui hutegemea umilisi wa wanafunzi, hivyo hatuwezi jumlisha kwamba wanafunzi wote watayaelewa maudhui kwa usawa.

### 4.4.4 Manufaa ya Maudhui ya Tamthilia

Swali hili lililenga kubaini iwapo wanafunzi wanaweza kutambua uhalisia wa maudhui wanayosoma katika kazi za tamthilia na hali halisi katika jamii. Wanafunzi themanini waliosema ndio walitoa sababu kwamba maudhui yanayoendelezwa na wahusika wa kazi za tamthilia huwapa taswira za moja kwa moja za viongozi na wanajamii kwa jumla.


Walisema kuwa kupitia kwa maudhui na tabia za wahusika wanapata maelekezo ya namna ya kuishi hata baada ya shule kwani tayari kupitia kwa tamthilia walihisi kama wao wanaishi katika ulimwengu halisi. Kuna idadi ya wanafunzi ishirini ambao walisema maudhui ya kazi za tamthilia hayawafai baadaye. Walitoa sababu kwamba baada ya shule kidato cha nne, wao huanza ukurasa mpya wa maisha. Walisema wao hukazana kuelewa maudhui kwa lengo la kupasi mtihani tu. Kulingana nao wakitoka wanaanza hali mpya ya maisha yenye maudhui mpya kwa mujibu wa jamii. Kwa maoni yangu majibu yote yaliyotolewa ni sawa, lakini ni kweli kwamba kazi za tamthilia hasa *Mstahiki Meya (2009*) na *Kigogo (2016)* ni tamthilia ambazo zinatupa taswira ya jamii, hivyo mwanafunzi anaposoma kazi za tamthilia atakuwa na manufaa kutambua na kuoanisha mambo katika jamii baadaye. Mfano swali na majibu ya watafitiwa: Maudhui ya kazi za tamthilia mnazosoma yanaufaafu yoyote katika maisha ya leo?

Ndio ☐

La ☐

Fafanua: Maudhui yana ufaafu kwasababu maudhui ni wazi na tunaweza kuyatambua katika jamii baada ya kufunzwa. Matokeo yalikuwa kama inavyowakilishwa katika mchoro ufuatao.

*Mchoro 5: Manufaa ya Maudhui ya Tamthilia*




Mchoro huu ulibainisha asilimia themanini ya wanafuzi wanaweza kutambua manufaa ya maudhui wanayosoma shuleni baadaye katika maisha yao. Walisema kuwa kupitia kwa maudhui na tabia za wahusika wanapata maelekezo ya namna ya kuishi hata baada ya shule kwani tayari kupitia kwa tamthilia walihisi kama wao wanaishi katika ulimwengu halisi. Kuna asilimia ishirini ya wanafunzi ambao walisema maudhui ya kazi za tamthilia hayawafai baadaye. Walitoa sababu kwamba baada ya shule kidato cha nne, wao huanza ukurasa mpya wa maisha. Walisema wao hukazana kuelewa maudhui kwa lengo la kupasi mtihani tu.

### 4.4.5 Kigezo cha Tofauti za Kimaudhui Katika Kazi za Fasihi Teule

Swali hili lililenga wanafunzi wa kidato cha nne kwa sababu katika kidato hiki huwa wamesoma kazi zingine za fasihi kama Riwaya na hadithi fupi. Wanafunzi arobaini walisema kuwa maudhui makuu ni sawa katika kazi hizi za fasihi tofauti na ufafanuzi na mbinu za uandishi. Walitoa mifano ya maudhui ambayo utayapata katika kila kazi ya tamthilia kwa mfano, ufisadi, uongozi mbaya, maandamano na migomo, ukoloni mambo leo umasikini, kudorora kwa huduma za afya, dhuluma, ukatili na ubinafsi.

Wanafunzi kumi walikuwa na maoni tofauti kuwa maudhui ni tofauti kutegemea lugha ya mwandishi na dhamira yake. Mfano wa majibu;


Swali: Kuna tofauti za maudhui kati ya kazi za fasihi teule mnazosoma shuleni?

Ndio ☐

La ☐

Eleza: Maudhui hata kwenye kazi zingine mbali na tamthilia yanakuwa sawa kama vile maudhui ya ukoloni, uongozi mbaya, ufisadi, tamaa, migomo na maadamano.Idadi ya jibu ndio au la imeonyeshwa kwenye mchoro 6.

***Mchoro 6: Tofauti Za Kimaudhui Katika Kazi Za Fasihi Teule***




Katika jedwali hili asilimia ya wanafunzi themanini waliweza kutambua usawa wa maudhui katika kazi zingine za fasihi bali na tamthilia.Asilimia ishirini walisema maudhui huwa tofauti kutegemea lugha na mtindo wa waandishi tofauti.

### 4.4.6 Kigezo cha Uhalisi wa Maudhui

Swali hili la hojaji lililenga kupata ufafanuzi zaidi juu ya uhalisi wa maudhui katika jamii na iwapo wanafunzi wa shule za upili wanaweza kutambua uhalisia huu. Wanafunzi walitoa majibu ya ndio au la kwa maudhui matano makuu ambayo mtafiti alikuwa amepeana.

#### 4.4.6.1 Maudhui ya Uongozi Mbaya

Idadi kubwa ya wanafunzi walijibu ndio kwamba maudhui ya uongozi mbaya yapo katika jamii. Walisema kwamba viongozi wengi hawajawajibika wengine wanatumia mamlaka yao vibaya kuwadhulumu wanajamii. Kutokana na ufafanuzi wao uongozi hasi au chanya ni jambo ambalo mwanajamii yeyote hawezi kulifumbia macho. Kwa hivyo wanafunzi waliotumika kama kiwakilishi cha wanajamii wanaweza kutambua maudhui ya uongozi mbaya.

Swali: Je, maudhui yafuatayo yapo katika jamii?

1. Maudhui ya uongozi mbaya

Ndio ☐

La ☐

Tetea kauli yako: kwasababu maswala ya uongozi mbaya yanaripotiwa kila siku kwenye vyombo vya habari yanaendelezwa na viongozi waotumia mbinu hasi za uongozi.

#### 4.4.6.2 Maudhui ya Ukoloni Mambo Leo

Wanafunzi walikubali kuwepo kwa vitendo vya ukoloni mambo leo katika jamii huru.Waliweza pia kutoa mifano ya namna ukoloni mambo leo unavyoendelezwa nchini. Kwa mfano walisema kwamba wanajamii wanadhamini mtindo wa kigeni katika mavazi, mijengo na vyombo vya usafiri, pili waliweza kutambua kwamba jamii huru bado inategemea nchi za kigeni kupata elimu na matibabu bora, tatu waliweza kutambua kwamba nchi huru za Kiafrika zinategemea mikopo kutoka mataifa ya

kigeni. Wanafunzi kumi na tano walitoa jibu la la. Wanafunzi hawa pia walionekana kutoelewa dhana ya ukoloni mambo leo katika maelezo yao.

2. Maudhui ya ukoloni mambo leo

Ndio ☐

La ☐

Tetea kauli yako: Haya ni kupitia mikopo, masomo ya nje, na kudhamini wakoloni.

#### 4.4.6.3 Ufisadi

Kutokana na majibu ya wanafunzi asilimia kuwa inaweza kutambua kuwepo kwa ufisadi katika jamii. Wanafunzi sabini na tano walitoa sababu ya ufisadi kuwa ni uongozi mbaya ubinafsi wa viongozi katika jamii. Wanafunzi ishirini na tano walielekea kutoelewa maudhui ya ufisadi.Kutokana kwa ufafanuzi wao wanafunzi walionyesha kulielewa suala hili la ufisadi kama donda sugu la maendeleo katika jamiiwaliweza hata kutoa mifano ya ufisadi katika jamii kama vile unyakuzi wa mali ya umma.

3. Maudhui ya ufisadi

Ndio ☐

La ☐

Tetea kauli yako: Ufisadi unaonekana wazi kupitia uongozi mbaya na kupora mali ya umma.

#### 4.4.6.4 Hali Ngumu ya Maisha

Wanafunzi sitini na tano waliohojiwa walitoa jibu la ndio kwamba wanajamii wa kawaida wanakabiliwa na hali ngumu maishani mwao. Walitoa sababu za ushuru wa juu, kukosa kazi na kupanda kwa bei ya bidhaa za kimsingi. Wanafunzi thelethini na tano ijapokuwa walikubaliana na hali hii walisema wanajamii wa tabaka la chini ndio

tu walio na ugumu wa maisha. Walisema viongozi na matajiri walio wa tabaka la juu hawajui hali hii.

4. Maudhui ya ugumu wa maisha

Ndio ☐

La ☐

Tetea kauli yako: Kutaokana na umaskini, uongozi mbaya hivyo kupanda kwa gharama ya maisha wanainchi wanaishi kwa umaskini.

#### 4.4.6.5 Umaskini

Wanafunzi tisini waliweza kubaini kuwepo kwa umaskini katika jamii. Walisema idadi kubwa ya wana jamii ni maskini wenye pato la chini. Wanafunzi kumi walisema sio watu wote katika jamii ambao ni maskini kwani kuna tabaka la juu la viongozi na matajiri ambao ndio wenye nchi. Kulingana na maoni ya wahojiwa kuhusu maudhui makuu elekezi ni wazi kuwa kuna uhalisia wa maudhui katika jamii kwa kiasi kikubwa sana.


5. Maudhui ya umaskini

Ndio ☐

La ☐

Tetea kauli yako: Baadhi ya wanajamii ni maskini na hawawezi kumudu maisha kwasababu ya hali ngumu ya maisha. Majibu ya ndio au la yamewasiliswa kisayansi kwenye mchoro 7.

*Mchoro 7: Uhalisi wa Maudhui*




Jedwali hili lilijumuisha sampuli ya maudhui matano makuu ambayo pia yameangaziwa na waandishi wa tamthilia za *Mstahiki Meya* (Arege, 2009) na *Kigogo* (Kea, 2016). Idadi kubwa ya wanafuzi iliweza kutambua kuwepo kwa maudhui ya umaskini, ugumu wa maisha, ufisadi, ukoloni mamboleo na uongozi mbaya katika jamii. Wanafunzi tisini na tano walijibu kwamba maudhui ya uongozi mbaya yapo katika jamii nao kumi wakasemakwamba hakuna uongozi mbaya. Waliosema ndio waliweza kutetea jibu lao kwa kutoa mifano kama viongozi wengi hawajawajibika wengine wanatumia mamlaka yao vibaya kuwadhulumu wanajamii. Wanafunzi kumi waliosema hakuna uongozi mbaya walitetea kauli yao kwamba viongozi walio mamlakani si wabaya, wananchi wanaowachagua ndio wabaya kwani wametawaliwa na tamaa kwa hivyo wanatekwa upesi kuwachagua viongozi waovu.

Wanafunzi themanini na watano kulingana na jedwali walikubaliana na kuwepo kwa ukoloni mambo leo katika jamii ya leo.Walitoa mifano ya waafrika kudhamini elimu, matibabu na lugha za kigeni kuliko zile za nchini kwao. Wanafunzi kumi na watano ambao walipinga kuwepo kwa ukoloni mambo leo walisema kilichopo si ukoloni

mamboleo lakini wanajamii hudhamini huduma za ugenini kwa kukosa huduma bora kwao nchini.

Kulingana na jedwali wanafunzi sabini na watano walikubaliana na kuwepo kwa ufisadi katika jamii.kutona na majibu yao ni bayana kwamba ufisadi ni halisi katika jamii ukichangiwa na uongozi mbaya na tamaa na ubinafsi miongoni mwa viongozi na wanajamii. Wanafunzi ishirini na watano walielekea kutobaini hali ya ufisadi katika jamii.

Kulingana na maoni ya wanafunzi kuhusu kuwepo kwa hali ya umaskini katika jamii, Walisema idadi kubwa ya wanajamii ni maskini wenye pato la chini. Wanafunzi kumi walisema sio watu wote katika jamii ambao ni maskini kwani kuna tabaka la juu la viongozi na matajiri ambao ndio wenye nchi. Kulingana na maoni ya wahojiwa kuhusu maudhui makuu elekezi ni wazi kuwa kuna uhalisia wa maudhui katika jamii kwa kiasi kikubwa sana.

### 4.4.7 Uchanganuzi wa Hojaji za Walimu

Data katika kiwango hiki imechanganuliwa kwa kurejelea migao ifuatayo: jinsia za wanafunzi, uelewa na utambuzi wa maudhui, jinsia katika kutambua maudhui, miaka ya kufunza tamthilia n kulinganisha na kulinganua maudhui ya tamthilia.

#### 4.4.7.1 Kigezo cha Jinsia za Wanafunzi

Kigezo hiki kilitumiwa kwa walimu pia lakini kwa lengo la kutaka kupata maoni ya walimu kuhusu umuhimu wa jinsia katika kuelewa maudhui. Kulingana na majibu yao idadi kubwa ya wanafunzi katika kata ndogo ya Nzambani ni wa shule za mseto. Kulingana na majibu ya walimu idadi ya wasichana katika baadhi ya shule hizo ni ya juu kiasi kuliko ya wavulana katika kidato cha nne na tatu shule mbili pekee katika kata ndogo hii ni za wasichana na wavulana pekee ambazo ni shule ya wavulana ya Nzambani na shule ya wasichana ya Chuluni. Kulingana na maoni ya walimu idadi tofauti ya wasichana na wavulana katika kidato cha nne na tatu kwa wanafunzi wa shule za mseto hutegemea usajili wa wanafunzi kutoka shule za msingi.Kigezo hiki

kilisaidia kupata majibu kutoka kwa jinsia zote.idadi ya wahojiwa katika kategoria ya jinsia imewasilishwa katika jedwali lifuatalo.


***Jedwali 4.7: Jinsia za Wanafunzi***

| **Shule** | **Jinsia ya Kike** | **Jinsia ya Kiume** |
|---|---:|---:|
| Shule ya mseto ya Kyanika | 6 | 4 |
| Shule ya wassichana Chuluni | 10 | 00 |
| Shule ya mseto ya Kilonzo | 5 | 5 |
| Shule ya wavulana ya Nzambani | 10 | 00 |
| Shule ya mseto ya Kavia | 7 | 3 |
| Shule ya mseto ya Kaluva | 6 | 4 |
| Shule ya mse to ya Kivumbuni | 5 | 5 |
| Shule ya mseto ya Kanduti | 8 | 2 |
| Shule ya mseto ya Thua | 6 | 4 |
| Shule ya mseto ya Utwiini | 7 | 3 |
| **JUMLA** | **70** | **30** |

Kutokanana jedwali hili wanafunzi sabini wa jinsia ya kike na themanini wa jinsia ya kiume walihojiwa hivyo utafiti uliangazia jinsia zote kutimiza malengo yake.

Data hii pia imewasilishwa kwa kutumia mchoro 8. Unaofuata hapa chini.

*Mchoro 8: Jinsia za Wanafunzi*




Katika jedwali hili wanafunzi hao walisampuliwa na walimu kujaza hojaji. Sababu ya kutaka kujua jinsia za wanafunzi na idadi ya kijinsia katika shule za mseto ni kutaka kubaini, uelewa na utambuzi wa wanafunzi wa maudhui katika kazi za tamthilia na changamoto wanazopata kuelewa kazi hizi na kupata picha halisi ya jamii kupitia usawa wa maudhui.

#### 4.4.7.2 Uelewa na Utambuzi wa Maudhui

Walimu walitoa majibu ya ndio na la kujibu swali la namna wanafunzi wao wanavyoelewa maudhui katika kazi za tamthilia. Walimu walieleza kwamba kazi za tamthilia huanza kufunzwa katika kidato cha tatu. Kutokana na majibu ya walimu idadi kubwa ya wanafunzi huweza kutambua maudhui kwa urahisi katika kazi za tamthilia teule. Hata hivyo kuna baadhi yao ambao hupata ugumu wa kuyaelewa na kuyatambua maudhui haswa katika kidato cha tatu katika utangulizi. Hata hivyo uelewa na utambuzi wa maudhui huegemea jinsia ile ya kike ikiwa na wepesi wa

kutambua maudhui na kuyaelewa kwa urahisi. Kutokana na maoni ya walimu inawachukua muda wanafunzi kuelewa maudhui. Walimu waliotoa jibu la ndio na la wameonyeshwa ifuatavyo;

Swali: Je wanafunzi wako wanaelewa na kutambua maudhui katika tamthilia vizuri.

Ndio ☐

La ☐

Fafanua: Wanafunzi katika kidato cha nne wanaweza kuelewa maudhui vizuri baada ya kuanaza kufunzwa katika kidato cha tatu. Uelewa hutemea umilisi.

***Jedwali 4.8: Kigezo cha Uelewa wa Maudhui na Wanafuzi***

| **SHULE** | **NDIO** | **LA** |
|---|---:|---:|
| Shule ya  mseto ya kyanika | 1 | 1 |
| Shule ya wasichana Chuluni | 3 | 1 |
| Shule ya mseto ya Kilonzo | 0 | 2 |
| Shule ya wavulana ya Nzambani | 2 | 3 |
| Shule ya mseto ya Kavia | 1 | 1 |
| Shule ya mseto ya Kaluva | 1 | 1 |
| Shule ya mseto ya Kivumbuni | 0 | 1 |
| Shule ya mseto ya Kanduti | 1 | 1 |
| Shule ya mseto ya Thua | 1 | 1 |
| Shule a mseto yaUtwiini | 0 | 1 |
| **JUMLA** | **10** | **13** |

Kutokana na ufafanuzi wa majibu ya walimu kuhusiana na swali hili uelewa na utambuzi wa maudhui pia hutegemea kiwango cha ufahamu wa wanafunzi kwenye shule nyingi za mseto kwenye kata ndogo hii. Baadhi ya wanafunzi huwa na alama za

chini sana wakati wa kujiunga na shule za upili. Hivyo huwa ni vigumu kwao kusoma na kutambua maudhui bila kuelekezwa.


Swali: Wanafunzi wa jinsia tofauti wanauelewa sawa na maudhui?

Ndio ☐

La ☐

Fafanua: Uelewa wa maudhui hutegemea jinsia.Ni rahisi kwa kwa wasichana kuelewa maudhui.Katika shule za mseto wasichana hufanya vizuri katika fasihi kuliko wavulana.

***Jedwali 9: Uelewa wa Maudhui na Wanafuzi***




Katika wasilisho la jedwali hili uelewa na utambuzi wa maudhui pia hutegemea kiwango cha ufahamu wa wanafunzi kwenye shule nyingi za mseto kwenye kata ndogo hii baadhi ya wanafunzi huwana alama za chini sana wakati wa kujiunga na shule za upili. Hivyo huwa ni vigumu kwao kusoma na kutambua maudhui bila kuelekezwa.

#### 4.4.7.3 Jukumu la Kijinsia Katika Kutambua Maudhui

Swali hili liliwataka walimu kutambua namna wanafunzi katika kazi za tamthilia ambazo uteuliwa kutahiniwa. Kutokana na mchango wao jinsia ya kike huweza kutambua na kuyaelewa maudhui kwa urahisi na hata kuweza kuyaoanisha na hali halisi kwa kuyatolea mifano mwaka kinyume na jinsia ya kiume ambapo mara nyingi, baadhi ya wanafunzi vijana hawajibidiishi kuvisoma vitabu vya kifasihi. Majibu yao yalikuwa kama ifuatavyo.

***Jedwali 4.9: Jukumu la jinsia katika kutambua Maudhui***


| SHULE | NDIO | LA |
|---|---:|---:|
| Shule ya mseto ya Kyanika | 2 | 0 |
| Shule ya wasichana ya Chuluni | 4 | 0 |
| Shule ya mseto ya Kilonzo | 2 | 0 |
| Shule ya wavulana ya Nzambani | 4 | 1 |
| Shule ya mseto ya Kavia | 1 | 1 |
| Shule ya mseto ya Kaluva | 1 | 1 |
| Shule ya mseto ya Kivumbuni | 1 | 0 |
| Shule ya mseto ya Kanduti | 2 | 0 |
| Shule ya mseto ya Thua | 1 | 1 |
| Shule ya mseto ya Utwiini | 1 | 0 |
| **JUMLA** | **19** | **4** |

Kulingana na maoni ya walimu na tajriba yao ya kufunza kazi za fasihi huwa ni rahisi kwa wasichana kuelewa na kutambua maudhui katika kazi teule kuliko wavulana. Hali hii hupelekea hata kuwepo kwa matokeo tofauti katika mtihani wa somo la Kiswahili kwa jumla.

Kutokana na wasilisho la jedwali hili ni wazi kwamba uelewa na utambuzi wa maudhui kati ya wavulana na wasichana ni tofauti.Kutokana na majibu ya wanafunzi

umilisi na utambuzi wa maudhui kwa  wasichana  ni kiwango cha juu. Kutokana na wasilisho la jedwali hili ni wazi kwamba uelewa na utambuzi wa maudhui kati ya wavulana na wasichana ni tofauti.

***Mchoro 10: Jukumu la Kijinsia Katika Kutambua Maudhui***




Kutokana  na wasilisho la jedwali hili ni wazi kwamba uelewa na utambuzi wa maudhui kati ya wavulana na wasichana ni tofauti.kutokana na majibu ya wanafunzi umilisi na utambuzi wa maudhui kwa  wasischana  ni wa kiwango cha juu.

### 4.4.8 Kigezo cha Miaka ya Kufunza

Swali hili lililenga kubaini muda ambao walimu wahojiwa wamefunza tamthilia teule za utahini shuleni za upili. Lengo kuu la swali hili ni kutaka kubaini iwapo kuna tofauti


za kimaudhui katika miaka tofauti ya utahini. Swali hili pia lilisaidia kulinganisha maudhui ya *Mstahiki Meya* na *Kigogo* kwasababu wanafuzi hawajasoma *Mstahiki Meya*.

***Jedwali 4.10: Jedwali ya Majibu ya Miaka ya Kufunza***

| **MIAKA** | **WALIMU** |
|---|---|
| Mwaka 1 - miaka 4 | 08 |
| Miaka 4 - miaka 8 | 10 |
| Miaka 8 na Zaidi | 05 |

Swali hili la miaka lililenga la kubaini iwapo maudhui ni tofauti, walimu wengi walitoa maoni kwamba maudhui makuu huwa sawa katika tamthilia tofauti ambazo wanafunza tofauti huwa ni maelezo, majina ya wahusika na mbinu za uwasilishaji wa maudhui hayo.

*Mchoro 11: Majibu ya Miaka ya Kufunza*




Kwa mujibu wa wasilisho la mchoro huu,walimu wengi wamefunza na kutahini kati ya miaka nne na nane (43.48%),mwaka mmoja hadi minne (34.7%) na miaka nane na Zaidi (21.74%) katika ulinganisho na ulinganuzi wa majibu yao ya kufafanua tofauti za maudhui wengi walitoa maoni ya kutokuwepo kwa tofauti za kimaudhui katika vipindi tofauti . Walimu walikuwa muhimu kwa swali hili kwani wao wamesoma tamthilia ya *Mstahiki Meya* kinyume na wanafunzi wao.

### 4.4.9 Kigezo cha Changamoto za Kufunza Tamthilia za Utahini Shuleni.

Manufaa ya kigezo hiki yalikuwa ni kusisitiza uelewa wa maudhui kwa wanafunzi na walimu wa shule za upili.Kutokana na maoni ya walimu kuhusu changamoto za kufunza tamthilia teule shuleni, baadhi ya walimu ambao wanauzoefu wa kufunza kazi za tamthilia walionyesha kutokuwa na ugumu wa kusoma, kufunza na kuzichambua kazi za tamthilia teule za utahini kwa wanafunzi. Ufafanuzi ambao wale

hawana changamoto walitoa ni kwamba hata kabla ya kusoma kitabu cha tamthilia ambacho kimeteuliwa kutahiniwa tayari wanaweza kubashiri maudhui makuu ambayo yanaendelezwa pale. Wanasoma vitabu hivi kupata majina ya wahusika na mbinu za uandishi.

Walimu ambao walisema kwamba kuna changamoto walitetea jibu lao na kusema kwamba changamoto hutokea pale ambapo wanafunzi wengine hawawezi kutambua maudhui na kuonyesha uhalisia wake katika jamii. Pia inakuwa vigumu kuwaambia wanafunzi kwamba maudhui ni sawa katika tamthilia moja na nyingine kwani wao husoma tamthilia moja tu kwa wakati wa kipindi teule cha utahini. Ufahamu wa mfanano wa maudhui basi hufaidi tu walimu.

Swali: Kuna changamoto za kufunza tamthilia za utahini shuleni?

Ndio ☐

La ☐

c) Fafanua: Kwa vile huwa tumefunza na kusoma tamthilia awali huwa ni rahisi kufunza tamthilia teule mbila utata.

***Jedwali 4.11: Majibu ya Changamoto za Kufunza Tamthilia***

| Ndio-Kuna changamoto | La-Hakuna Changamoto |
|---|---|
| Walimu saba (07) | Walimu kumi na sita(16) |

Kutokana na majibu ya wahojiwa kumi na sita hakuna changamoto nyingi za kufunza maudhui ya tamthilia, basi ni bayana kwamba maudhui ya kazi za tamthilia yanafanana kwa pakubwa yaani maudhui ni yale yale tofauti ni maendelezo. Hata wahojiwa waliosema ipo changamoto hawakupinga ukweli kuwa maudhui ni sawa, tatizo ni kuwa mfanano ule humfaidi mwalimu tu ambaye amevisoma vitabu vingi vya tamthilia.

#### 4.4.9.1 Kulinganisha na Kulinganua Maudhui ya Tamthilia.

Swali hili lilimwelekeza mtafiti kupata mawazo ya walimu ambao wamefunza kazi za fasihi katika vipindi tofauti vya utahini, swali hili liliongozwa na vigezo vya usawa wa maudhui. Hulka za wahusika na mbinu za uwasilishaji.

***Jedwali 4.12: Kulinganisha na Kulinganua Maudhui ya Tamthilia***

| KIGEZO | NDIO | LA |
|---|---|---|
| Maudhui sawa | 23 | 00 |
| Sifa za wahusika sawa | 20 | 03 |
| Mbinu za uandishi | 18 | 05 |

Swali: Je, ulinganisho wako wa maudhui ya tamthilia ambazo zimetahiniwa awali na tamthilia teule sasa ni upi?

Maudhui sawa

Ndio ☐

La ☐

Fafanua: Maudhui ya kazi za fasihi ni sawa. Mudhui kama vile uongozi mbaya, ufisadi, ukoloni mamboleo, umaskini miongoni mwa mengine.

1. Sifa za wahusika sawa

Ndio ☐

La ☐

Fafanua: kutegemea wanavyoendeleza maudhui.

2. Mbinu za uandishi sawa


Ndio ☐

La ☐

Fafanua: Kutegemea mtindo na dhamira ya mtunzi.

Kutokana na majibu yao, Maudhui, Sifa za wahusika na hata mbinu za uandishi ufanana kwa kiasi kikubwa. Tofauti huwa katika maelezo. Kwa kigezo hiki mtafiti alifaidika kutambua kwamba maudhui ni sawa katika tamthilia.

***Mchoro 12: Kulinganisha na Kulinganua Maudhui ya Tamthilia***




Kutokana na wasilisho la jedwali hili idadi kubwa ya walimu walikubali kwamba maudhui katika tamthilia teule huwa sawa tofauti huwa katika maelezo na majina ya wahusika. Kwa jumla tamthilia teule zinafanana kwa kiasi kikubwa kimaudhui

### 4.4.10 Kigezo cha Ufaafu wa Maudhui

Kwenye swali hili ambapo lengo huu ni kubaini iwapo maudhui yanawafaa wanafunzi, walimu waliohojiwa walionyesha kuridhika na maudhui hayo. Kulingana nao maudhui hayo huwafaa wanafunzi kwa kuwadaa kwa maisha yao ya usoni. Walimu ishirini kati ya walimu ishirini na tatu waliohojiwa waliunga mkono ufaafu wa maudhui. Watatu walikuwa na maoni tofauti na kauli hii. Walidai kuwa baadhi ya mwanafunzi hawezi kuyaoanisha maudhui yanayoyasoma na yaliyopo nje ya shule zao kwa sasa. Kulingana na walimu hawa wanafunzi wengi husoma kazi za kifasihi

shuleni kwa minajili ya kupasi mtihani tu. Wengine hata husahau waliyoyasoma pindi tu wanapotia kitone cha mwisho kwenye karatasi la tatu. Kulingana na wahojiwa kunao wanafunzi ambao hawafaidikina mafunzo ya tamthilia hizi siku za usoni. Je, maudhui ya tamthilia zinazoteuliwa yana ufaafu gani kwa wanafunzi na jamii kwa jumla?

### 4.4.11 Kigezo cha Uhalisia wa Maudhui

Wahojiwa walikuwa na maoni tofauti pia. Wengi waliunga mkono na kusema kwamba maudhui makuu yanayoendelezwa na kazi za waandishi tofauti ni taswira ya jamii ya leo. Kwa vile fasihi ni kioo cha jamii, basi waandishi wa kazi za tamthilia wakiwepo Timothy (2009) na Kea (2016) wamefanikiwa kwa kiasi kikubwa kukuza uhalisi wa maudhui katika kazi zao. Kulingana walimu waliohojiwa mwanafunzi ambaye amesomo kazi ya tamthilia hana ugumu wa kubaini mambo halisi katika jamii yanayotendeka na ambayo yanaendelezwa na kazi ya tamthilia.

Hata hivyo wahojiwa wengine watatu kati ya ishirini na tatu waliohojiwa walikuwa na dhana tofauti. Kwao waliutazama uhalisi kwa namna mbili tofauti. Kulingana nao mwalimu ambaye amesoma kazi za tamthilia tofauti ataweza kuona uhalisia wa maudhui katika jamii. Pili walisema kwamba mwanafunzi ambaye yuko shuleni huenda asielewe dhana ya uhalisia wa maudhui. Tatu mwanafunzi ambaye anasoma ili apite mtihani huyasahau maudhui aliyoyasoma mara tu akikamilisha mtihani hivyo itakuwa vigumu kwake kuuona uhalisia wa maudhui katika jamii baadaye.

Swali: Kulingana na maoni yako maudhui katika tamthilia yana uhalisia katika jamii ya leo?

Ndio ☐

La ☐

Fafanua: Waandishi wa kazi za tamthilia wamefanikiwa kuonyesha maudhui halisi katika jamii hivyo kazi zao zinawafaa wanafunzi.

## 4.5 Hitimisho

Sura hii ilijadili maudhui makuu katika tamthilia teule *Mstahiki Meya (2009)* na *Kigogo (2016*).Sura hii imebaini maudhui makuu katika jamii na kuyalinganisha na maudhui makuu katika tamthilia teule ili kubaini uhalisia wake katika jamii. Data iliyokusanywa kutoka kwa hojaji za walimu na wanafuzi ili kufanikisha utafiti ilichanganuliwa na kuwasilishwa kisanyasi.

# SURA YA TANO

# MUKHTASARI, MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Katika sura hii utafiti umeshughulikia mukhtasari wa sura zote za utafiti huu. Sura hii pia imejadili matokeo, mapendekezo na matatizo ya utafiti huu.

## 5.1 Mukhtasari

Utafiti huu ulilenga kutathmini maudhui katika tamthilia tahiniwa katika shule za upili nchini Kenya. Hili kufanikisha zoezi hili, utafiti ulilenga tamthilia mbili ambazo zimetahiniwa kwa kidato cha nne. Tamthilia ya *Mstahiki Meya (2009)* ilifunzwa na kutahiniwa kati ya miaka ya (2013-2017). Tamthilia ya *Kigogo (2016)* iliteuliwa kufunzwa na kutahiniwa kuanzia mwaka wa 2018 hadi 2022.

Katika sura ya kwanza utafiti ulibaini wazi tatizo la utafiti kwamba, pana haja ya kuchunguza uhalisia wa maudhui katika kazi za tamthilia zinazoteuliwa kutahiniwa shuleni za upili. Kwa vile ni wazi kuwa baadhi ya maudhui kama vile ukoloni mamboleo, ufisadi, umaskini, uongozi mbaya, dhuluma,nk.yanapatikana katika kazi nyingi za kifasihi tofauti ikiwa ni mbinu za uwasilishaji na majina tofauti ya wahusika utafiti ulilenga kubaini vigezo vya kuteua kazi hizi ili kutahiniwa na zaidi kuchunguza uhalisi wake katika jamii na kama kazi hizi zinawafaa wanafunzi shuleni na baadaye.

Utafiti uliongozwa na malengo matatu ambayo ni;Kutambua ufaafu wa maudhui katika tamthilia za *Mstahiki Meya (2009)* na *Kigogo (2016)* na kisha kuyalinganisha na kuyalinganua.Pili kutathmini masuala makuu katika jamii ambayo pia yanaangaziwa na *Mstahiki Meya* na *Kigogo*.Tatu ubaini ufaafu wa tamthilia za kutahiniwa kwa wanafunzi kama kielelezo cha jamii kwa kutumia nadharia ya uhalisia.

Upeo wa mipaka wa utafiti ni pamoja na miaka ya kuteuliwa kufunzwa na kutahiniwa kwa tamthilia za *Mstahiki Meya (2009)* na *Kigogo (2016)*. Tamthilia hizi zilifunzwa na kutahiniwa kati ya 2013-2022 katika tamthilia hizi mbili utafiti ulijikita kwenye maudhui makuu pekee. Mada hii ilichaguliwa kwa sababu tamthilia zinazolengwa na utafiti ni kazi za wanafasihi chipukizi ambao ni zao la jamii ya leo hivyo ipo haja ya kuzitathimini kazi zao kimaudhui kuona iwapo kuna kazi nyingi za tamthilia hizi mbili ni za kipekee kwani zilipata kuteuliwa kutahiniwa kati ya mwaka wa 2018 hadi mwaka wa 2021. Sababu hii ilitupa maudhui na uhalisia wake katika jamii, na zaidi ufaafu wa maudhui hayo kwa wanafunzi wakati wa masomo na baadaye katika jamii.

Sura ya pili iliangazia tafiti za awali kuhusiana na mada ya utafiti huu. Kwa kuongozwa na tafiti na maadishi ya awali kuhusu kazi za tamthilia utafiti huu ulipata msingi wa kujibu maswali ya utafiti ambayo ni pamoja na; Kubaini maswala makuu yanayojitokeza katika tamthilia za *Mstahiki Meya (2009) na Kigogo (2016).* Pili kubaini maswala makuu ya kijamii yaliyosheheni katika kipindi cha kuteuliwa kufunzwa na kutahiniwa kwa tamthilia hizi.Kubaini uhalisi wa maudhui na ufaafu wake kwa wanafunzi wakiwa shuleni na baadaye.

Sura hii pia iliweka wazi nadharia ya kuongoza utafiti-nadharia ya uhalisia. Kupitia kwa misingi ya nadharia ifuatayo mtafiti aliweza kufanikisha malengo yake.

Kazi ya fasihi inajitosheleza. Utafiti ulichunguza maudhui ya tamthilia mbili *Mstahiki Meya (2009)* na *Kigogo (2016).* Kwa kutumia mhimili huu utafiti ulibaini kwamba kazi hizi mbili zinajisimamia na kujitosheleza kimaudhui, wahusika na mtindo.

Kazi ya msanii inapaswa kuwasilisha ukweli kama ulivyo katika mazingira yake. Mhimili huu ulisadia utafiti huu kutathmini uhalisia wa maudhui ya tamthilia za *Mstahiki Meya (2009*) na *Kigogo (2016)*. Waandishi Timothy Arege na Pauline Kea, wamefanikiwa kujadili mambo halisi katika jamii.

Wahusika ni vielelezo yakini vya binadamu wa kawaida kwa vile wao hutumia lugha ya binadamu wa kawaida. Msingi huu ulisaidia utafiti huu kubaini dhana ya uhalisi wa maudhui. Waandishi Timothy Arege (2009) na Pauline Kea (2016) wamefanikiwa kutumia wahusika halisi japo kwa majina ya kimajazi ili kuangazia maudhui ambayo ni halisi katika jamii ya leo.

Msanii anaangalia matatizo na kuchunguza vyanzo vyake. Wasanii Timothy Arege na Kea Pauline kupitia tamthilia zao *Mstahiki Meya (2009) na Kigogo (2016)*,wamezungumzia mambo ambayo japo kwenye jamii. Maudhui ambayo yanajadiliwa ni mambo halisi katika jamii leo na vyanzo vyake ni kuchagua viongozi wasiofaa na viongozi wenyewe kutowajibikia kazi yao.

Katika sura ya tatu ya utafiti mambo yafufuatayo walichunguzwa ili kufanikisha malengo ya utafiti huu. Utafiti ulichukua muundo wa kimaelezo baada ya kusoma na

kuchanganua tamthilia za *Mstahiki Meya (2009)* na *Kigogo (2016).* Utafiti ulilenga usomaji wa maktabani na hojaji kwa wanafunzi wa kidato cha tatu na cha nne na walimu katika kata ndogo ya Nzambani. Vitabu vya tamthilia teule *Mstahiki Meya (2009) na Kigogo 2016* ni sampuli za kazi za tamthilia ambazo ni za waandishi chipukizi na ambao baada ya utafiti na uchanganuzi wa maudhui katika tamthilia zao wameendeleza uhalisia wa maudhui kwa mujibu wa jamii ya leo. Sampuli ya wanafunzi na walimu ambao walihojiwa ni kiwakilishi cha jamii ya leo. Sampuli hii ilisaidia kubaini ufaafu na uhalisia wa maudhui ya kazi za tamthilia katika jamii.

Sura ya nne ya utafiti ilichanganua maudhui makuu katika tamthilia za *Mstahiki Meya* na *Kigogo*. Kwenye sura hii utafiti ulijadili maudhui ya uongozi mbaya, umaskini tamaa, ufisadi, migomo na maadamano, matumizi mabaya ya mamlaka, uchafuzi wa mazingira, unafiki, ukoloni mamboleo na ukiukaji wa haki. Katika tamthilia za Mstahiki *Meya (2009)* na *Kigogo (2016).*Maudhui haya yalilinganishwa na kulinganuliwa na baadaye mtafiti alitathimini ufaafu wa maudhui hayo na uhalisia wake kwa kuangazia maudhui hayo katika jamii. Kupita kwa majibu ya hojaji za walimu na wanafunzi maudhui ya tamthilia teule yana uhalisi na kazi za tamthilia na fasihi kwa jumla ni kioo cha jamii.

Kutokana na asilimia kubwa ya walimu na wanafunzi kuhusu ufaafu wa tamthilia teule ni wazi kwamba kigezo kikuu cha uteuzi wa kazi za tamthilia ni kwamba lazima zijadili hali halisi katika jamii na zaidi ziwafae walimu wanafunzi na hata wasomi wa waandishi wengine. Kupitia kwa magazeti na vyombo vingine vya habari utafiti ulibaini kuwa maudhui makuu yanayoendelezwa na waandishi Timothy Arege na Kea Pauline ni sawa na yale yaliyoko kwenye jamii.

## 5.2 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kutimiza malengo yafuatayo: Lengo la kwanza lilikuwa kutathmini maswala makuu ya kijamii katika vipindi vya kuteuliwa na kutahiniwa kwa tamthilia za *Mstahiki Meya* (Arege, 2009) na *Kigogo (*Kea, 2016)

Utafiti huu ulibainisha kuwa tamthilia teule zinaendeleza maudhui makuu sawa na yaliyoko katika jamii husussan uongozi mbaya, ufisadi, ukoloni mamboleo, umaskini,

tamaa miongoni mwa mengine.Kutokana na matokeo ya utafiti huu maudhui ya tamthilia za kisasa ni yale yale tofauti ni jinsi mwandishi anavyoyaendeleza kupitia wahusika wake, mbinu za uwasilishaji na mtindo. Tamthilia za kisasa pia ni kioo cha jamii halisi kupitia maudhui yake ambayo kwa upana yanazungumzia jamii ya leo.

Lengo la pili lilikuwa kubaini ufaafu wa tamthilia za kufunzwa na kutahiniwa kwa wanafunzi na walimu. Kutokana na majibu ya hojaji zao ni bayana kwamba tamthilia zinawafaa kwa kuwapa taswira ya jamii ya leo. Kutokana na kusoma na kusikiliza vyombo vya habari wanaweza kuoanisha yaliyomo kwenye tamthilia teule na yale yanayoangaziwa kwenye jamii. Hivyo hata baada ya shule hawajihisi wageni katika jamii yao kwani huwa wamefunzwa maswala makuu yanayoikuba jamii yao kwa hivyo maudhui ya kazi za tamthilia yanafaa jamii na kuendeleza elimu na maadili.

## 5.3 Mchango wa Utafiti

Kutokana na utafiti huu ni bayana kwamba fasihi haswa tamthilia inaangazia maswala makuu ambayo yanaikumba jamii ya sasa. Watunzi wa tamthilia wanajikita katika uhalisi kujadili maswala halisi katika ulimwengu. Utafiti huu utasaidia wanafunzi kuelewa kwamba yale wafunzwayo ni halisi katika jamii hivyo kuwaandaa kupambana nayo baada ya kuhitimu kidato cha nne. Walimu kupitia kwa utafiti huu watapata urahisi wa kuyafunza maudhui makuu kwa wanafunzi na kusisitiza umuhimu wake katika maisha ya baadaye.

## 5.4 Matatizo

Shughuli ya utafiti huu haikuwa rahisi. Mtafiti alikubwa na changamoto zifuatazo; kwanza uhaba wa vitabu vya kiswahili vinavyoeleza dhana ya tamthilia za kisasa. Pili mtafiti hangeweza kuwapata waandishi wa tamthilia teule kuwahoji kuhusu kazi zao haswa maudhui. Matatizo hayo yaliufanya utafiti hii kukawia kwa muda. Tatizo la uhaba wa vitabu ulimtatiza mtafiti kwani ilimlazimu kutafuta tafsiri ya maneno mengine kutoka kwa kiingireza na vigumu kupata visawe wa maneno. Hata hivyo utafiti ulikamilika.

## 5.5 Mapendekezo

Dhana ya maudhui ni panasana katika kazi za kifasihi na jamii kwa jumla. Uchanganuzi na ufafanuzi wa maudhui unaweza kushughulikiwa kwa namna tofauti kutegemea mtazamo wa mhakiki. Utafiti huu ulilenga maudhui pekee katika tamthilia teule ambazo kwa kipindi kimoja ziliwahi kutahiniwa katika shule za upili. Tafiti za baadaye zinaweza kufanywa kuhusu mambo yafuatayo;

Tofauti za kimtindo na mbinu za uwasilishaji katika tamthilia ambazo zinazungumzia maudhui sawa.

Utafiti wa kina juu ya kazi tofauti za kifasihi kama kulinganisha maudhui katika tamthilia na riwaya au hadithi fupi na tamthilia.

Swala lingine ambalo linahitaji utafiti zaidi ni vigezo vingine ambavyo hutumiwa kuteua vitabu vya tamthilia za kufunzwa na kutahiniwa shuleni bali na ufaafu na uhalisia wa maudhui.

Utafiti huu ulitumia nadharia ya uhalisia kujadili maudhui makuu na halisi katika jamii. Aidha utafiti zaidi unaweza fanywa kwa kutumia nadharia zingine.

# MAREJELEO


Arege, T. M. (2009). *Mstahiki Meya*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Bryman, A. (2004). *Social Research Methods* (2nd edition). Oxford: Oxford UniversityPress.

Central Bank of Kenya (2018). *The year of resilience: Annual Report & Financial Statements 2017/18*. CBK: Nairobi.

Colin, L. (1975).*Underdevelopment in Kenya. ThePolitical Economy of Neo-Colonialism.* London: Heine-mann.

Ethics and Anti-Corruption Commission [EACC]. (2018).*National Ethics and Corruption Survey, 2017*. EACC: Nairobi.

Fridah, G. O. (2017). *Uhakiki wa Mtindo katika Tamthilia za Arege*. (Tasnifu ya uzamili). Chuo Kikuu Cha Maasai Mara, Narok, Kenya.

Gatakaa, G. (2012). *Uhakiki wa maudhui katika Utenzi wa Mikidadi na Mayasa.* (Tasnifu ya uzamili). Chuo Kikuu Cha Nairobi, Nairobi, Kenya.

Human Rights Watch (2019). *World report 2019: Events of 2018*. USA:Human Rights Watch

Kea, P. (2016). *Kigogo*. Nairobi: Story Moja Publishers.

Kimeu B.S. naMaina B. W. (2018). Forceful Evictions: An Intersection between Corruption, Land And Human Rights Case study of the Kenyan perspective.*African Journal of Land Policy and Geospatial Sciences, Special Issue, (2018 )/102-106*

King'ei, K.G. Kyalo, J.M. na Mwangi, L.W. (2012). *Mwongozowa Mstahiki Meya*(Timothy M. Arege).Nairobi: Target Publishers.

Kothari, C. K. (1990). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley.

Lucaks (1963). The meaning of contemporary realism, London: Merlin Press.

Maundu. R.M. (2017). The Impact of Neo-Colonialism on Coffee TradingActivities in Kenya(Tasnifu ya uzamili). Chuo Kikuu Cha United States International University – Africa. Nairobi, Kenya.

Mumbi, Z. N. (2014). Academic neo-colonialism must be fought. Business Daily: Nairobi. Retrieved from: *https://www.businessdailyafrica.com/analysis/ac*

*ademic-neo-colonialism-must-be-fought/539548-2494648-5ueaff/index.html.*

Munene, A. (2014). The Right to Strike - Sustainable Constitutional Reform: Comparative Case Studies of Workers' Strikes in the Kenyan Public Sector. *International Comparative Law Review, 37(1/4).*

Muthoni, M. (2014). *Uhakiki wa Maudhui na Mtindo katika Tikitimaji*. (Tasnifu ya uzamili). Chuo Kikuu Cha Nairobi, Nairobi, Kenya.

Mwangi, J.N. (2018). Uhakiki wa Suala la Dini na Umuhimu Wake Katika Utendi na Al-Inkishafi.*Mara Research Journal of Kiswahili*, 3(1), 79 - 86.

Nasibo, K. (2019). State to Import more Cuban Doctors. Business Daily: Nairobi. Retrieved: *https://www.businessdailyafrica.com news/state to import more Cuban doctors.*

Ngesa, A.K., Matundura, M.naKobia, J. (2015). Mwingilianomatini katika Tamthilia za Kiswahili: *Mashetani* na *Kijiba cha Moyo*. *Swahili Forum 22 (2015), 42-71*

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). Ufundishaji wa Fasihi*: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njoroge, J. (2017). Directors' Greed Eroding Public Confidence in Boards. Business Daily. Retrieved from: *https://www.businessdailyafrica.com/economy/Directors--greed-eroding-public-confidence-in-boards/3946234-4120398-3bomolz/index.html*

Njoroge, M. (2019). Kenyans-cost of Living High Since 2017 Election Period.Business Daily: Nairobi. Retrieved from*: https://business today.co.ke/Kenyans-cost of living high since 2017 election period.*

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Illinois: Augustana College,Rock Island.

Okebiro, G. Nyakundi; Mana, B. na Kiprop, A. (2014). *Environmental Pollution and Waste Management: A Case Study of Ten Towns in Kenya.* Workshop Proceedings: Masai Mara University.

Okwena, S. (2013). *Matumizi ya Jazanda katika Tamthilia Tatu za Timothy Arege*. (Tasnifu ya uzamili). Chuo Kikuu Cha Kenyatta, Nairobi, Kenya.

Omanga, E., Ulme, L. Berhane, Z. na Gatari, M. (2014). Industrial Air Pollution in Rural Kenya: Community Awareness, Risk Perception and Associations between Risk Variables. BMC Public Health, 14:377.

Omosa, J.M. (2014). Failure of Good Corporate Governance in State owned Corporations in Kenya: Towards a more effective Parliamentary Role (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.

Ongarora, S.O (2007) Mtindo katika hadithi fupi ya Mohamed (2005), S.A *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine* (Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi.Kenya.

Otieno, O. (2019). Why Kenyan politicians are wrong to pay themselves a "house allowance". Democracy in Africa. Retrieved from: *http://democracyinafrica.org/kenyan-mps-wrong-pay-house-allowance/*

Owallah, K.O. (2013). *Uhakiki wa maudhui teule katika utenzi wa nabii Isa* (Tasnifu ya uzamili). Chuo Kikuu Cha Nairobi, Nairobi, Kenya.

Preston, B. (2014). *Jinsi Mandhari Yanavyoendeleza Maudhui Katika Tamthilia ya Ebrahim n. Hussein ya Mashetani*(Tasnifu ya uzamili). Chuo Kikuu Cha Makerere, Kampala, Uganda.

Retrieved from https://repository.uchastings.edu/hastings_international_comparative_law_review/vol37/iss1/4

Salem, M .A. (2013). *Maudhui na Fani katika Tamthilia za Kiswahili: Utafiti linganishi wa Tamthilia ya Mashetani (Hussein 1971) na Kivuli kinaishi (Mohamed 1990)*Tasnifu ya Uzamivu Chuo Kikuu Huria cha Tanzania)

Seale, C. (2012). *Researching Society and Culture*.London: Sage Publications Ltd.

Senkoro, F. E. (1988). Ushairi, Nadharia na Tahakiki. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Society for International Development (SID) (2012). *The Status of Governance in Kenya: ABaseline Survey 2012*. SID: Nairobi.

Syekei, M. N. (2017). *Nafasi Na Athari ya Kiongozi wa Kike katika Tamthilia Teule Za Kiswahili.* (Tasnifu ya uzamili). Chuo Kikuu Cha Maasai Mara, Narok, Kenya.

The constitution of Kenya (2010)

Transparency International (2018).*Corruption Perceptions Index 2017*. TI: Nairobi.

UNICEF. (2018). *Kenya at a Glance*. UNICEF: Kenya. Retrieved from: https://www.unicef.org/kenya/overview_4616.html

United Nations Office on Drugs and Crime. (2018). *Global Study on Homicide: Gender-Related Killing of Women and Girls*. Vienna: United Nations.

Wamitila, K. W. (2002): *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

Wamitila, W. (2008). Misingi ya Uchambuzi wa Fasihi. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd

Wily, L. (2018).*Community Property in Kenya*. Retrieved from: *https://www.forestpeoples.org.*

## VIAMBATISHO

***Kiambatisho:1:Kibali cha Kutafiti***



SOUTH EASTERN KENYA UNIVERSITY
OFFICE OF THE DIRECTOR
BOARD OF POST GRADUATE STUDIES

P.O. BOX 170-90200
KITUI, KENYA
Email: info@seku.ac.ke

TEL: 020-4213859 (KITUI)
Email: directorbps@seku.ac.ke

Our Ref: C410/KIT/20670/2015

DATE: 19th July 2018

Muthui Evelyn Kakivi
Reg. No. C410/KIT/20670/2015

*Kiambatisho 2: Fomu A ya Kukubali Kushiriki Utafiti*

**FOMU YA KUKUBALI KUSHIRIKI UTAFITI.**

**CHUO:** CHUO KIKUU CHA SOUTH EASTERN KENYA UNIVERSITY KITUI.

**IDARA:** IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA.

**MADA:** TATHIMINI YA MAUDHUI KATIKA TAMTHILIA TEULE ZA KISWAHILI ZINAZOTAHINIWA SHULENI ZA UPILI NCHINI KENYA: *MSTAHIKI MEYA (2009)* NA *KIGOGO (2016).*

**JINA LA MTAFITI**: EVELYN KAKIVI MUTHUI.

**NAMBARI YA USAJILI:** C410/KIT/20670/2015.

**KIWANGO CHA ELIMU**: UZAMILI KATIKA KISWAHILI.

**MAELEZO YA MATARAJIO.**

Madhumuni ya utafiti huu ni kutathimini maudhui katika tamthilia teule za kiswahili zinazotahiniwa shuleni za upili nchini kenya: *Mstahiki Meya (2009)* Na *Kigogo (2016)* Mtafitiwa

***Kiambatisho 3: Fomu B ya Kukubali Kushiriki Utafiti:***

**FOMU YA KUKUBALI KUSHIRIKI UTAFITI.**

**CHUO:** CHUO KIKUU CHA SOUTH EASTERN KENYA UNIVERSITY KITUI.

**IDARA:** IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA.


**MADA:** TATHIMINI YA MAUDHUI KATIKA TAMTHILIA TEULE ZA KISWAHILI ZINAZOTAHINIWA SHULENI ZA UPILI NCHINI KENYA: *MSTAHIKI MEYA (2009)* NA *KIGOGO (2016).*

**JINA LA MTAFITI:** EVELYN KAKIVI MUTHUI.

**NAMBARI YA USAJILI:** C410/KIT/20670/2015.

**KIWANGO CHA ELIMU:** UZAMILI KATIKA KISWAHILI.

***Kiambatisho 4: Mfano (A) wa Majibu ya Hojaji za Walimu***



**Kiambatisho B: Hojaji Kwa Walimu**

i. Taja jinsia ya wanafunzi wako.

a) Wasichana ☐
b) Wavulana ☑
c) Mseto ☐

ii. Je wanafunzi wako wanaelewa na kutambua maudhui katika tamthilia vizuri.

a) Ndio ☐
b) La ☑
c) Fafanua

Wanafunzi katika kidato cha tatu wana
changamoto za kutambua na kuelewa Maudhui

*Kiambatisho 5: Mfano (A) wa Majibu ya Hojaji za Walimu - Unaendelea*

Ndio ☑

La ☐

Fafanua Maudhui ya kazi za fasihi huwa sawa. Yanaweza kuwa ni kazi za waandishi tofauti kwa nyakati tofauti.

b) Sifa za wahusika sawa

Ndio ☑

La ☐

Fafanua Wahusika ndio hutumika kuendeleza maudhui hivyo kama maudhui ni sawa, sifa pia ni sawa.


*Kiambatisho 6: Mfano (B) wa Majibu ya Hojaji za Walimu*

**Kiambatisho B: Hojaji Kwa Walimu**

i. Taja jinsia ya wanafunzi wako.
   a) Wasichana ☑
   b) Wavulana ☐
   c) Mseto ☐

ii. Je wanafunzi wako wanaelewa na kutambua maudhui katika tamthilia vizuri.
   a) Ndio ☑
   b) La ☐
   c) Fafanua

*Kiambatisho 7: Mfano (B) wa Majibu ya Hojaji za Walimu - Unaendelea*



Ndio ☑

La ☐

Fafanua: Maudhui ya kazi za fasihi ni sawa. Maudhui kama yale uongozi mbaya, ufisadi, ukoloni mamboleo, umaskini miongoni mwa mengine


b) Sifa za wahusika sawa

Ndio ☑

La ☐

Fafanua: Kutegemea maudhui yanayoendelea

*Kiambatisho 8: Mfano (A) wa Majibu ya Hojaji za Wanafunzi*



**Kiambatisho A: Hojaji Kwa Wanafunzi**

(i) Taja kidato chako.

a) Cha tatu ☑

b) Cha nne ☐

(ii) Taja jinsia yako.

a) Kike ☐

b) Kiume ☑

(iii) Je, maudhui ya kazi za tamthilia za fasihi mnazosoma shuleni yanaeleweka kwa urahisi?

a) Ndio

***Kiambatisho 9: Mfano (A) wa Majibu ya Hojaji za Wanafunzi - Unaendelea***

b) La

c) Tetea kauli yako

Kuna nafasi ya maudhui haya katika vyombo vya habari kama mwanajamii ninayaona na kuyasikia mambo ya uongozi mbaya

2. Maudhui ya ukoloni mambo leo

a) Ndio ☑

b) La ☐

c) Tetea kauli yako

Haya ni kupitia kwa mikopo, masomo ya nchi za nje kudhamini wakoloni

***Kiambatisho 10: Mfano (B) wa Majibu ya Hojaji za Wanafunzi***

**Kiambatisho A: Hojaji Kwa Wanafunzi**

(i) Taja kidato chako.


a) Cha tatu ☐
b) Cha nne ☑

(ii) Taja jinsia yako.

a) Kike ☑
b) Kiume ☐

(iii) Je, maudhui ya kazi za tamthilia za fasihi mnazosoma shuleni yanaeleweka kwa

*Kiambatisho 11: Mfano (B) wa Majibu ya Hojaji za Wanafunzi - Unaendelea*



b) La

c) Tetea kauli yako

kwasababu masuala ya Uongozi mbaya yamepatikana kila siku kwenye vyombo vya habari yanaendelezwa na viongozi wanaotumia mbinu hasi za uongozi.

2. Maudhui ya ukoloni mambo leo

a) Ndio ☑

b) La ☐

c) Tetea kauli yako

Ukoloni ~~mbaya~~ mambo leo upo katika jamii kupitia kwa viongozi, mikopo ya kigeni na kandarasi za nchi

*Kiambatisho 12: Ratiba ya Kazi*

| KAZI | DEC 2017 | JAN – MAR 2018 | APR 2018 | MAY – JUN 2018 | JUL – AUG 2018 | SEP – DEC 2018 | JAN – MAR 2019 | MAY 2019 | JUN 2019 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kutafuta mada ya utafiti | | | | | | | | | |
| Kuandika pendekezo | | | | | | | | | |
| Kutetea pendekezo la utafiti | | | | | | | | | |
| Kusoma na kuchambua maudhui ya tamthilia | | | | | | | | | |
| Kukusanya data | | | | | | | | | |
| Kuchanganua data | | | | | | | | | |
| Kuandika ripoti | | | | | | | | | |
| Kutetea na kuandika ripoti ya mwisho | | | | | | | | | |
| Kuchapisha nakala | | | | | | | | | |

***Kiambatisho 13: Shule Zilizohojiwa***

| **ORODHA** | **SHULE** |
|---|---|
| 1. | Shule ya mseto ya Kyanika. |
| 2. | Shule ya wasichana ya Chuluni |

| | |
|---|---|
| 3. | Shule ya mseto ya Kilonzo. |
| 4. | Shule ya wavulana ya Nzambani. |
| 5. | Shule ya mseto ya Kavia. |
| 6. | Shule ya mseto ya Kaluva. |
| 7. | Shule ya mseto ya Kivumbuni |
| 8. | Shule ya mseto ya Kanduti. |
| 9. | Shule ya mseto ya Thua. |
| 10. | Shule ya mseto ya Utwiini. |

***Kiambatisho 14: Makisio ya Bajeti***

| **SHUGHULI/BIDHAA.** | **GHARAMA (Shilingi za Kenya)** |
|---|---:|
| 1. Usafiri. | 50,000/- |
| 2.Vitabu na makala | 20,000/- |
| 3. Uchapishaji wa tasnifu na makala mengine. | 40,000/- |
| 4. Diski, tarakilishi, kalamu. | 50,000 /- |
| 5.Matumizi ya ziada | 15,000 /- |
| **JUMLA** | **175,000 /-** |